

## **BUNGE LA TANZANIA**

---

### **MAJADILIANO YA BUNGE**

---

#### **MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 28 Juni, 2012**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

#### **D U A**

Spika (*Mhe. Anne S. Makinda*) Alisoma Dua

#### **MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge leo ni siku nyingine ya Alhamisi ambayo tunakuwa na nusu saa kwa maswali ya Waziri Mkuu na baadaye maswali mengine ya kawaida.

Namwona Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni kwamba yupo leo, kama kanuni yetu inavyoruhusu yeye ndiye ataanza kuuliza swali la kwanza.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la kwanza kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, wewe ni Kiongozi Mkuu na Kiongozi muhimu katika Serikali na kauli yako ni kauli nzito sana. Siku ya jana ulitoa kauli ambayo kama mzazi ama kama baba imetia hofu kubwa sana katika Taifa, pale ulipokuwa unazungumzia mgomo wa Madaktari na hatimaye ukasema na linalokuwa na liwe.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuanzia jana baada ya kauli yako vilevile zilipatikana taarifa zingine kwamba Rais wa Madaktari Dkt. Ulimboka ametekwa juzi usiku, ameteswa, amevunjwa meno, ameng'olewa kucha na mateso mengine mengi sana na kwa sababu uliahidi Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba mtatoa kauli ya Serikali leo. Jambo hili sasa limechukua sura mpya na katika maeneo mbalimbali ya nchi, tayari Madaktari wengine wako kwenye migomo. Wewe kama Waziri Mkuu unalieleza nini Taifa kuhusu kauli yako ya litakalokuwa na liwe na Serikali inafanya nini cha ziada *ku-address* tatizo hili?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijaribu kutoa ufanuzi kwenye maeneo mawili ambayo Mheshimiwa Mboge ameyazungumza.

Kwanza nikiri kwamba ni kweli nilitamka hivyo jana, lakini inawezekana likapata tafsiri nyingi. Lakini kilichokuwa kinanisumbua kichwani ni kwa sababu nilijua jambo hili liko mbele ya Mahakama Kuu na kwamba kutoa kauli wakati jambo liko Mahakamani ni dhahiri ningonekana mtovu wa taratibu zetu za kikatiba. Ndiyo maana nikafika mahali nikasema katika mazingira yaliyopo inawezekana nikaonekana mtovu

kwa maana ya kutaka kueleza kinachoendelea na tunataka kufanya nini. Ndio maana nikasema aah!!, najua watanilaumu viongozi wa mhimili huo mwingine, lakini *I think, I have got to say something.*

Sasa hiyo *ofcourse* imetafsiriwa na hata hapa niliona dada yangu Halima akajaribu kuhusisha na jambo lingine nikasema ni bahati mbaya. Kwa sababu wakati ule hata habari hizo sikuwa nazo. Kwa hiyo nilichokuwa nasema kilikuwa kinahusiana zaidi na mgomo wa Madaktari na nikaahidi nitatoa kauli Bungeni. Lakini jana kwa bahati nzuri, mpaka jana usiku tumeshauriana pamoja na vyombo vingine vyamihimili ikaonekana bado hatuwezi sisi wakati jambo hili limeahirishwa mpaka mwezi ujao sisi tukaendelea kutaka kulieleza mbele ya Bunge na mimi nika-*respect* huo ushauri. Kwa hiyo, kama ilitafsiriwa vibaya lakini *angle* yangu hasa nilikuwa naitaka kuizungumzia ilikuwa ni kwa sababu nilijua hilo liko mbele yangu. Lakini nikadhani pengine haitakuwa na madhara makubwa. Lakini nimeona ushauri ule mzito nimekubali na si ajabu hata kauli ile hatutaitoa itategemea Spika atakavyoelekeza.

Lakini la pilli, ni hili la yaliyompata Dkt. Ulimboka. Kwanza nionyeshe masikitiko yangu juu ya jambo hili na mimi namtakia kila la kheri apone haraka. *It's unfortunate* kwa sababu *process* ilivyokuwa inakwenda ilikuwa ni nzuri kwa maana ya kwamba tuliamini tungefika mahali tungelewana vizuri sana na nilikuwa nimelenga juu ya mambo mengi.

Lakini baada ya hili tukio tena na nimelipata nikiwa hapa hapa ilitu-*disturb* wote sana. Sasa jana Mheshimiwa Dkt. Nchimbi nimearifiwa kwamba alitoa *press juu ya jambo* hili nadhani atakuwa alilieleza kwa namna ambavyo imeeleweka pengine kwa wananchi. Lakini nataka niseme tu kwamba taarifa ambazo na mimi nililetewa baada ya pale ni mazingira ambayo bado yanahitaji uchunguzi. Tulichoagiza sisi ni kwamba uchunguzi ufanywe haraka ili ukweli wa jambo hili uweze kubainika. Kwa sababu mazingira yake kidogo yana utata mwangi na yanahitaji kwa kweli kufanyiwa uchunguzi wa kina.

Sasa kila mmoja ana hisia zake, mwagine anafikiri hiki, wengine wanafikiri ni Serikali, wengine wanadhani sio hao, pengine ni hili. Sasa hayo yote hatuwezi kukaa hapa Bungeni tukajaribu kuyasema sema.

Lakini nilisema kwamba kwa upande wangu nikasema kama ni Serikali basi tutakuwa ni watu wa ajabu sana, kwa sababu Dkt. Ulimboka tumekuwa naye muda wote, tumeshirikiana naye katika *process* hii wakati tunalizungumza. Tumefika tumekwenda Mahakamani na nilijua kwamba jambo hili liko Mahakamani na vyombo vyote vinajua kwamba tulikuwa Mahakamani.

Sasa ile kidogo inanipa taabu kuona kwamba kama ni Serikali mnataka kufanya ili iweje kwa sababu *process* ilikuwa bado inaendelea. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema pengine njia rahisi tusubiri uchunguzi wa kina. Mimi nimewaambia jana wahakikishe jambo

hili linaharakishwa sana. Kwa ufupi ninayoweza kusema ndiyo maelezo niliyonayo. (*Makofi*)

**MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumesikia tena hapa pengine Serikali inakusudia kutokutoa Kauli juu ya tatizo hili.

**SPIKA:** Tatizo lipi?

**MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA UPINZANI BUNGENI:** Tatizo hili la mgomo wa Madaktari na tunavyozungumza hivi kuna taarifa kwenye vyombo mbalimbali vya habari kwamba Madaktari tayari katika Hospitali ya Muhimbili, Mbeya *Referral Hospital*, Bugando, KCMC na maeneo mengine mengi wameanza mgomo rasmi na hawaendi kazini leo.

Kama Serikali inasubiri kutoa tamko kwa sababu ya kusubiri pengine *process* ya Mahakama kuna hatua gani za makusudi, za ziada zinazochukuliwa na Serikali kutafuta angalau ufumbuzi *temporary* wa tatizo hili kwa sababu ni vifo vya watu vinakwenda kutokea kwa wingi sasa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu mnafanya *intervention* gani katika misingi ya dharura?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwa maana pengine ya hatua ambazo Serikali inafikiria au imeamua kuchukua ni hatua ambazo ni za kawaida. Tulichofanya pale tumezungumza na vyombo mbalimbali ili tuone katika mazingira tuliyonayo ni

namna gani tutawahudumia wagonjwa. Kwa hiyo, kubwa tulilojaribu kufanya tumeomba wenzetu wa Lugalo tutumie hospitali ile kwa ajili ya kuhakikisha wagonjwa hawakosi hiyo huduma.

Lakini kupitia Lugalo vilevile hata hospitali zake nyingine ndogo zote tumeamua tuzitumie kwa njia hiyo. Lakini wakati huo huo tumeona ni vizuri tuone kama kutakuwa na Madaktari wengine *retired doctors*, Madaktari ambao wako Wizarani pale wote tumeomba sasa watafutiwe njia mbalimbali ili warudi waweze kutoa hiyo huduma kwa Watanzania. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kwa maana hatua za kujaribu kuona tufanye nini hilo tunaendelea nalo. Lakini hatujachoka vilevile kuendelea kuzungumza kama tutapata fursa ya kuzungumza na Madaktari na hata jana tuljaribu kuzungumza sana kuona pamoja na haya mengine yote lakini juhudziendelee.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa Serikali ya awamu ya nne ilivyoshika hatamu za uongozi kwa kasi kubwa sana ilipambana na wimbi la ujambazi lillolokuwa limekithiri sana nchini. Kwa kuwa kwa sasa wimbi hilo limeanza tena na limeanza kutoa taswira ya hofu kwa wananchi wetu katika maeneo mbalimbali. Kwa mifano kuvamiwa kwa watalii huko Serengeti na majambazi, lakini vilevile ile biashara ya usafirishaji binadamu iliyosababisha baadhi ya Waethiopia kukutwa wamekufa pale Kongwa. Lakini na hili tukio la

kutekwa kwa Dkt. Ulimboka na majambazi na kuumizwa vibaya.

Je, sasa Serikali inachukua hatua gani ili kuwaondolea wananchi hofu ambayo imeanza kupanda?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba yako matukio yamejitokeza ambayo kidogo yameanza kutupa wasiwasi hata upande wa Serikali. Hili la Serengeti ni mojawapo, lakini hata hilo uliloligusia la kusafirisha Waethiopia kuitia Tanzania nalo vilevile limekuwa ni jambo kubwa.

Lile la Ndugu yangu Ulimboka kama nilivyosema kwa sababu uchunguzi umeanza tutaona litakapoishia. Lakini kwa ujumla tu niseme hali ya uhalifu nchini ni kweli kwamba yako matukio ya hapa na pale makubwa ambayo yanahitaji kutazamwa kwa haraka sana. (*Makofi*)

Kwa hiyo, uamuzi umeshafanywa na Serikali na tulikuwa na Rais lakini ameona arudi Dar es Salaam kwa sababu ya kwenda kuzungumza mambo haya nadhani Baraza lile la Usalama la Taifa litajadili kwa kina jambo hili ili liweze kutoa maelekezo sasa juu ya hatua stahiki ambazo zinaweza zikachukuliwa ndani ya kipindi hiki kifupi. (*Makofi*)

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu suala la utafutaji mafuta katika Visiwa vya Zanzibar ni moja kati ya kero kubwa katika kero za Muungano. Hivi karibuni Serikali

ya Zanzibar kupitia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mheshimiwa Mohamed Aboot, alitoa kauli akisema kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeshatoa taarifa kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu uchimbaji na utafiti wa mafuta katika Visiwa vya Zanzibar akiweka wazi kwamba mafuta ya Zanzibar yatachimbwa na Serikali ya Zanzibar.

Huu ni msimamo mpya ambao umetolewa hivi karibuni. Je, Serikali ya Muungano inatoa msimamo gani mpya juu ya suala hili la mafuta ya Zanzibar?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa mafuta una hatua nyingi, hatua ya msingi kabisa ni ile ya mwanzo ya utafiti au uchunguzi. Ni kweli kwamba kwa upande wa Tanzania Zanzibar hilo bado limekuwa ni eneo moja ambalo hata kwanza lilikuwa halijaanza kufanyiwa utafiti kutokana na sababu mbalimbali. (*Makofi*)

Baada ya pale mkishapata ndio mnaingia katika hatua sasa yenewe ya kuchimba mafuta. Lakini swali lako la msingi ni lile linalohusu hili hili eneo la mafuta na pengine na gesi maana vyote vinakwenda pamoja. Kwamba Serikali ya Zanzibar imeamua jambo hili litasimamiwa na Serikali ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ukiniuliza nasema wala sioni tatizo hata kidogo, sina mgogoro na jambo hili. Nasema hili kwa moyo mkunjufu tu kwamba kwangu Zanzibar ikipata mafuta sidhani kama Tanzania tutakosa kitu chochote. Tutakachofaidi ni kwamba tutayapata mafuta pua na mdomo. Kwa hiyo,

itakuwa rahisi sana, gharama nafuu sana kuliko ikiwa mbali zaidi.

Tatizo tu ni lile la kisheria na Kikatiba, lakini upande wa Tanzania na sisi kama unavyosema jambo hili tumekwishaanza kulifanyia kazi nadhani wakati wowote litapelekwa kwenye *cabinet* kwa maana ya kufanya uamuzi wa msingi ili turuhusu hili jambo liendelee wakati taratibu nyingine hizo za kuja kuondoa au kutokuondoa kwa sababu Katiba liko kwenye *schedule* basi ikifika likute hilo jambo liko mikononi kwa wahusika. Kwa hiyo, binafsi nadhani halina mgogoro mkubwa sana. (*Makofi*)

**MHE. KHATIB SAIDI HAJI:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika na ahsante Mhesimiwa Waziri Mkuu kwa jibu zuri lenye matumaini.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, je, suala hili la utafutaji wa mafuta Zanzibar unadhani kwa mawazo yako litatupeleka mpaka kwenye Katiba mpya au ufumbuzi wake unaweza ukapatikana katika siku za karibuni?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Khatib ninachosema tu hapa ni kwamba nataka hili jambo litazamwe kwa maana ya hatua za sasa. Kwamba kutafuta mafuta inachukua miaka 7 au 8 ni muda mrefu sana na kipindi chote kile inakuwa ni uchunguzi.

Mimi kimitazamo nasema kwa upande wa Serikali ya Muungano ni vizuri tukaliona kwa nia njema kwamba turuhusu ule uchunguzi angalau wa katika hatua za awali uanze tu sababu hatujui kitakachotoka pale ni nini.

Suala la kuliondoa kwenye eneo lile bahati nzuri tuko katika mchakato wa Katiba Mpya linaweza likafika wakati ule na pengine tutakuwa hata mafuta yenewe hatujayaona bado, lakini ni vizuri tukaanza bila kuchelewa ili tuwape nafasi waweze kufanya hiyo kazi.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa muda mrefu tumekuwa tukigharamia Mbio za Mwenge ambazo zimekuwa zikihamasisha na kufungua miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hadi sasa Serikali inaweza kuliambia nini Taifa faida jumla na hasara ambazo zimekuwa zikipatikana katika mbio hizi za Mwenge? (*Makofii*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kila Taifa lina mambo ambayo ingependa yawasaki die wananchi wake kuwakumbusha mambo fulani fulani. Upande wetu sisi tuliona kwamba pengine suala hili la kukimbiza Mwenge linaweza kuwa linatusaidia kuwakumbusha Watanzania mambo fulani fulani ya msingi. Ndiyo maana unakuta hata *Olympic* wanakimbiza Mwenge na unazunguka mpaka huku nchi nyingine, tunakwenda tunaupokea, kuna vitu ambavyo mnakuwa mmedhamiria kuvifanya.

Hasa kwa upande wa Tanzania Mwenge unatukumbusha mambo mengi na hasa ni kauli ya Baba wa Taifa alipokuwa anawasha Mwenge alitoa maneno ambayo yalikuwa ni mazito sana "Kwamba nataka uwekwe juu ya Mlima Kilimanjaro itoe matumaini kwa watu, iendeleze amani tujaribu kujenga." Ile hisia za mshikamano na maendeleo ilikuwa hasa ndio lengo la kutaka tukumbushane. Ndiyo maana tunapoukimbiza tunatumia fursa hiyo mara nyingi kuwa na kauli mbiu fulani fulani.

Sasa Mwenge una nguvu sana kwa sababu unavuta watu wengi, unapita maeneo mengi. Kwa hiyo kaulimbiu zile SENSA, UKIMWI, MAENDELEO na kadhalika, unaufikisha kwa watu kwa namna ambayo ni rahisi na haina tatizo. (*Makofi*)

Lakini pili, tumetumia sana Mwenge hasa kwenye kuwafanya watu watumie muda zaidi kidogo katika Miradi ya Maendeleo. Ndiyo maana katika Mwenge unakuta tunazindua miradi mingi sana, tunaweka mawe ya msingi mengi sana na kadhalika. Kwa kweli kimsingi nasema ni jambo jema na ni vizuri tusiliache bila ya sababu. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Kama hakuna haja ya swali la nyongeza sio lazima uulize.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, je, Serikali inatambua manung'uniko ya wananchi ya

kwamba kunapokuwa na mkesha wa mbio hizo za Mwenge kunafanyika zinaa ambayo ni kicho cheo cha UKIMWI? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Haji zinaa inafanyika popote tu na kila mahali. Ndio!! Kwa hiyo kusema kwamba wakati wa Mwenge ndio zinaa inafanyika, mimi nadhani hatuutendei haki Mwange hata kidogo. Maana binadamu tulivyo tukianza kutafutana hapa kwenye eneo hilo sijui mtasema nini, nadhani ukweli ndio huo.

**SPIKA:** *Night clubs* zipo. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, moja kati ya sababu zilizosababisha mfumko wa bei nchini ni chakula. Serikali katika kukabiliana nalo imekuwa ikijaribu sana kutawanya chakula kwa gharama kubwa kutoka maeneo ya uzalishaji na kupeleka sehemu nyingine.

Kwa kuwa Mkoa wa Rukwa na Katavi ina idadi kubwa sana ya chakula, mwaka huu peke yake Mkoa wa Rukwa unatarajiwa kuwa na akiba ziada ya tani 229,777.

Je, Serikali haioni kuunganisha eneo hili la uzalishaji na reli ili kupunguza gharama hii ambayo imekuwa ikiingia kwa kutumia usafiri wa malori ambayo ni gharama sana.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, sikumpata vizuri. Amesema meli Reli.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Reli Mheshimiwa.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, maana maneno haya meli na reli ukiwa mbali kidogo tabu kutofautisha lakini vyovyote vile ninachowea kusema kwamba kwanza nikiri kwamba Rukwa kwa ujumla pamoja na Mkoa mpya wa Katavi ni kweli una wazalishaji wakubwa sana wa chakula na hasa mahindi na tatizo letu sisi ni namna ya kuondoa mahindi kwenye eneo hilo kuyapeleka maeneo yenyе mahitaji ama kwa kutumia reli ama kwa kutumia barabara vyovyote tunavyofikiri ni njia ambazo zingeweza kusaidia. Sasa kwanza nikubaliane na wewe kwamba hiyo ni changamoto kwa upande wetu.

Lakini niamini kabisa kwa mpango wa maendeleo ulivyowekwa reli hii ya kati itakavyoanza kukarabatiwa pamoja na ile ya Mpanda na kwenda Kigoma tunaamini tunaweza kuboresha sana huduma hiyo kupeleka mahindi kwenye maeneo mengine. Lakini si hiyo tu, iko haja vilevile ya kufungua barabara ya kutoka Mpanda kwenda Tabora, kupitia Sikunge kwa njia ya lami. Tukifanya hivyo hili nalo litakuwa ni njia nyingine rahisi sana ya kupeleka vyakula hasa kwenye maeneo ya Kanda ya Ziwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini niongeze vilevile kwamba hata kama tungepata usafiri wa meli ungeweza

kutusaidia sana kufikisha angalau pale Kigoma, Kigoma mnaingiza kwenye treni nayo ingeweza kuwa njia nyingine. Kwa hiyo, tutajitahidi kuona kila njia ambayo tunafikiri inaweza kutusaidia kuboresha usafirishaji wa mazao haya.

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu mwezi wa pili Madaktari walipogoma hili suala ulilichukua wewe mwenyewe na ukalishughulikia na baadaye taifa likatangaziwa kwamba Madaktari hawatagoma tena. Haijapita miezi mitatu Madaktari wamegoma nchi nzima. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwanini usiwajibike kwa kujiuzulu kwa kushindwa kutatua matatizo ya Madaktari wetu. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, yapo mazingira unayoweza ukawajibika kwa njia hiyo lakini si lazima yakawa yote. Mimi sioni kama hili ni moja kati ya maeneo ambayo unaweza ukasema kistahiki hivi naweza nikafikia hatua hiyo. *Ninacho-appreciate* ni kwamba tatizo hili ni kweli ni la muda mrefu lakini *I have done my best* kujaribu kulitatu kwa kiasi kikubwa sana. Ndiyo maana nasema ukinifikisha pale na mimi nitakuwa na maelezo vilevile kueleza ni nini nimefanya katika jitihada za kujaribu kulimaliza.

Lakini *being what It is* inabidi tukubali kwamba bado linachangamoto nyingi kwa sababu ya mambo mengi tu ambayo yameingiliana na mgogoro wenyewe. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu swali la nyongeza.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu *if you have done your very best and you have failed why don't you resign?* (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Hilo swali linarudia swali lilelile. Naomba usijibu kwa sababu linarudia lilelile.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Tundu Lissu hiyo si lugha nzuri sana. Mimi nakuheshimu sana. Lakini sidhani kama *that is the best approach* ya kuzungumza na wakubwa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Tunaendelea na Mheshimiwa Martha Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa ziko habari zinazosambaa katika jamii kwamba madhara haya makubwa yanayotokana na mgomo wa Madaktari unasababishwa na baadhi ya vikundi vyta watu ambavyo vinawatumia baadhi ya madaktari kwa kuwapa fedha ili waende wakahamasishe mgomo na kulazimisha baadhi ya Madaktari kwa sababu wanataka eti nchi isitawalike. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa mgomo wa madaktari una madhara makubwa sana katika taifa

hili. Je, Serikali sasa iko tayari kuchunguza ukweli huu na uvumi huu ili kuona ukweli uko wapi tuweze kuokoa maisha ya Watanzania wanaokufa bila hatia? Ahsante sana. (*Makof*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mgogoro huu wa madaktari una maneno mengi sana. Hilo unalolisema dada yangu Mlata na mimi vilevile nimelisikia lakini tulishaomba vyombo vyetu vyatilizwa na usalama vijaribu kulifuatilia tuone kama lina ukweli wowote ndani yake. Kama tutapata maelezo yanayotosheleza kuonyesha kwamba kuna ukweli huo basi nadhani hatua zinazostahili zitachukuliwa. (*Makof*)

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, mimi nashukuru kwa majibu ya mazuri. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa pamoja na kwamba Serikali haina dini lakini watu wake wana dini. Je, uko tayari kuomba taasisi zote za dini zikafanya maombi kwa ajili ya kuwaombea watu hawa wabaya wanaotaka kuharibu usalama wa taifa letu. (*Makof/Kicheko*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mimi siyo mcha Mungu, lakini ni Muumini wa dini vilevile. Rai kwa maana ya rai na pengine usi-*confine* tu kwa hawa wabaya. Mimi nadhani tuliombee taifa hili amani kwa ujumla. Mimi nataka niwashukuru sana viongozi wa madhehebu ya dini ambao kila kukicha wanaliombea taifa hili amani. Kwa sababu *the bottom line* vyovyote vile itakavyokuwa bila amani nchi hii hakuna kitakachofanyika. Kwa hiyo, mimi nadhani rai ni nzuri

tutaendelea kuwaomba waendelee kuliombea taifa kwa kadri itakavyowezekana.

**SPIKA:** Wewe mbona hauko kwenye orodha.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Naomba tafadhalii tuendelee. Kwenye kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu hakuna Kanuni inayosema tutafanya mwongozo. Tuendelee Mheshimiwa Hemed.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, sio mwongozo ni kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Wenje tusibishane. Mheshimiwa Salum Hemed Khamis. Pole sana tumefurahi kukuona.

**MHE SALUM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru nilidhani umeshaniruka. Maana kwenye orodha mimi ni mtu wa nne. Mheshimiwa Waziri Mkuu tarehe 28 Agosti, 2008 nilikuuliza swali hapa katika kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu kuhusu ahadi ya Serikali ya Muungano juu ya kifuta machozi cha familia za wahanga wa maandamano ya tarehe 26 na 27 Januari 2001 kule Zanzibar ambapo watu 23 waliuawa kwa kupigwa risasi na Polisi na taarifa hizo ni kwa mujibu wa Serikali yenyewe. Lakini kwa sababu ulikuwa bado ni Waziri Mkuu mpya ulimwomba Naibu Spika ambaye sasa hivi ndiye Spika mwenyewe akupe muda wa kufuatilia sakata lile. Januari mwaka huu tayari

imetimia miaka 12 tangu mauaji yale yafanyike na nadhani karibu miaka minne toka ulipoahidi kulifuatilia. Wakati tunaongea sasa hivi familia za wahanga na Wazanzibar kwa ujumla wanakuona na wanakusikiliza. Je, naomba uwaambie ni kwanini ahadi ile imechelewa hadi leo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu rafiki yangu Salim kama ifuatavyo:-

Ni kweli tukio hilo lilitokea na ni kweli jambo hilo llipewa ahadi ya namna fulani ya kifuta machozi na mimi baada ya kuniuliza siku ile nilijaribu kulifuatilia lakini halijapata ufumbuzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salim swali la nyongeza.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, inasikitisha ikiwa wafugaji wa Loliondo, Monduli na Ngorongoro wamepewa kifuta machozi karibu shilingi bilioni 633 kwa sababu ya kupoteza mifugo yao kutokana na ukame. Leo watu ambao binadamu wamepoteza ama mke ama mume au mtoto na Serikali imeahidi lakini mpaka leo hakuna ufumbuzi. Je, hapa kuna nia thabiti ya kupeleka hiyo ahadi kama ilivyotolewa au ni ubabaishaji?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ahadi ni deni. Mimi naamin tuvute subira jambo hili lina mambo mengi litakapokamilika nina hakika litatoa majibu yake.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu maswali yamekwisha na wewe tunakushukuru sana

kwa majibu na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kuuliza maswali. Kwa kifupi na tumeweza kumaliza wale wote waliomba kuzungumza. Tunaendelea na *Order Papaer*, Katibu.

## **MASWALI NA MAJIBU YA KAWAIDA**

**SPIKA:** Tunaendelea, Mheshimiwa Peter Kafumu atauliza swali la kwanza.

Na. 94

### **Ukubwa wa Jimbo la Igunga**

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU** aliuliza:-

Jimbo la Igunga lina eneo kubwa na wakazi zaidi ya 500,000. Sasa je, ni lini Serikali italigawa Jimbo hilo na kufanya Majimbo mawili ili kurahisisha uwakilishi na kutoa huduma nzuri zaidi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati wa kugawa Majimbo ya Uchaguzi mwaka 2010 kabla ya Uchaguzi Mkuu, Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliweka vigezo na utaratibu wa kupokea maombi ya kugawa majimbo kutoka

Halmashauri mbalimbali. Tume ilipokea maombi 53 yakiwemo maombi kutoka Jimbo la Igunga. Kati ya maombi hayo maombi 42 yalitimiza vigezo likiwemo Jimbo la Igunga.

Hata hivyo Tume ya Taifa ya Uchaguzi haikuweza kuligawa kutokana na ufinyu wa Bajeti ya kuendesha Bunge lakini pia nafasi ya Ukumbi wa Bunge na ongezeko la Wabunge wa Viti Maalum kutoka 75 mpaka 102. Hivyo tume iliweza kugawa Majimbo saba tu kati ya Majimbo 42 yaliyokuwa yamefikia vigezo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Katiba ya Nchi inatoa mamlaka kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuchunguza mipaka ya Majimbo kwa vipindi maalum, Tume wataendelea kutekeleza jukumu lake hilo na pale ambapo zoezi hilo litafanyika tena Jimbo la Igunga litafikiriwa kugawanywa kwa kuzingatia vigezo vitakavyowekwa. (*Makofi*)

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Waziri kwa majibu yake mazuri na nategemea baadaye Igunga nayo itapendelewa iwe kati ya yale yatakayogawanya awamu inayokuja. Naomba sasa nimwulize swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa ni dhahiri kuwa eneo la Jimbo la Igunga ni kubwa na kwa kuwa Jimbo hili linapokea wananchi wenye mifugo kutoka maeneo mengine wanahamia.

Idadi ya watu katika Jimbo hilo inaongeza sana. Je, Serikali itakuwa tayari baada ya Sensa ya mwezi wa nane idadi ya watu itakapo julikana itakuwa tayari kuruhusu mchakato wa maombi yetu tutakayoleta ya

kuligawa Jimbo la Igunga kuwa Wilaya mbili yenye Jimbo moja moja?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, mimi naomba Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote tusubiri zoezi kubwa zaidi linalokuja la mapitio ya Katiba kwa sababu kwanza hata utaratibu wa Tume wa kufikiria huwa unaenda kila baada ya miaka kadhaa.

Haiendi kila mwaka na sio kila kipindi kimoja Tume inafanya jambo hilo. Kwa hiyo kimsingi ningeomba tuvute subira kwa sababu mimi naamini yapo mambo mengi sana ambayo yanahitaji kurekebishwa kutokana na mwenendo wa uchaguzi.

Jana tumeulizwa swalii na Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kupitia Mkoa wa Dodoma juu ya uchaguzi mdogo. Watu wengine wanafikiri hata *by-elections* zisiwepo. Kwa sababu *by-election* moja kama ile ya Igunga au ya Arumeru ina-cost Serikali shilingi bilioni 1.57. (*Makofii*)

Sasa ukiacha fedha za vyama vilivyoshiriki, ukiacha na wapambe wengine, vyombo vyaa habari zinatumika fedha nyingi na hizi zote huwa haziko kwenye Bajeti. Ikitoka *by-election* basi Serikali inakwenda kuchota Hazina ambazo hazikuwa kwenye Bajeti kwa sababu huwezi kubajeti kitu ambacho hakipo na zinatumika 1.57 billion kwa ajili ya jambo kama hilo.

Kwa hiyo, yapo mambo mengi sana ambayo tukitengeneza Katiba yetu vizuri inawezekana hata mfumo wa uchaguzi, idadi ya Majimbo na utaratibu wa uendeshaji wa uchaguzi ukabadilika.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Tume ya Taifa ya Uchaguzi imekuwa inakosea katika ugawaji wa Madiwani wa Viti Maalum katika maeneo mengi sana nchini. Je, Serikali iko tayari kulichunguza jambo hili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mkosamali, unasema ugawaji wa nini? Majimbo ya Madiwani au *what*?

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, Viti Maalum vya Udiwani vinavyogawanywa kwenye Halmashauri zetu nchini wamekuwa wanakosea katika kufanya mchakato huu katika maeneo mengi. Je, Serikali iko tayari kulifuatilia jambo hili ili kubaini ukweli na mimi niko tayari kutoa ushahidi wa makosa ambayo wamekuwa wanayafanya?

**SPIKA:** Tunalikubali tu lakini ilikuwa kugawa Majimbo, sasa kugawa Madiniwani tena. Haya Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, ikiwa kama Mheshimiwa Mkosamali ana tatizo kama hilo na lina vielelezo na anaushauri namshauri mambo mawili. Anaweza kulifikisha jambo hilo kwenye Tume

likachunguzwa au unaweza ukani pa mimi ambaye ndiye mwakilishi wao hapa nikapeleka likachunguzwa. Haina tabu.

Na. 95

### **Kurejesha Magari ya Wagonjwa yaliyohamishwa**

**MHE. MARIA I. HEWA (K.n.y. MHE. DKT. TITUS M. KAMANI)** aliuliza:-

Magari mawili ya wagonjwa yaliyokabidhiwa katika kituo cha afya cha Nasa na Zahanati ya Lukungu mnamo mwezi mei, 2010 yaliondolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Magu na hivyo kutokufanya kazi katika vituo hivyo kama ilivyokusudiwa:-

Je, Serikali itarejesha lini magari hayo ili yatumike kwa malengo yaliyokusudiwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Titus Mlenganya Kamani, Mbunge wa Busege, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Magu mwaka 2010 ilipata magari mawili yenye namba za usajili T 848 BFP na T 854 BFP aina ya *Fiat Ducato Ambulance* kwa ajili ya kusaidia huduma

ya kubeba wagonjwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu.

Magari hayo yalitolewa na Taasisi isiyo ya Kiserikali ijulikanayo kama *Community Development Relief Agency* ya mjini Magu. Magari haya yalipokelewa na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Busega kwa wakati huo, Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni na aliyakabidhi katika kituo cha Afya Nassa na Zahanati ya Lukungu mnamo mwezi Mei, 2010. Magari haya hayakuwa mapya yalikuwa yametumika huo nchi za Ulaya.

Mheshimiwa Spika, magari haya yalifanya kazi kwa takribani miezi mitatu tu baada ya kukabidhiwa na kisha yalianza kusumbua, hivyo ilibidi yahamishiwe kwa mhandisi wa Halmashauri ili mafundi waweze kuyafanya uchunguzi wa kina. Ukaguzi ulibaini kuwa magari haya yalikuwa na matatizo makubwa ambayo yalihitaji matengenezo makubwa pamoja na kubadilishwa vipuri mbalimbali. Baada ya hatua hii, zoezi lililofuatia lilikuwa ni kuandaa vidadisi bei na kupelekwa kwa wazabuni. Wazabuni walishindwa kujaza vidadisi bei kutokana na ugumu wa kupatikana vipuri vyta aina ya magari hayo. Magari hayo hayakuondolewa bali yalirudishwa Halmashauri kwa ajili ya matengenezo ili yaendelee kutoa huduma katika Zahanati ya Lukungu na kituo cha Afya Nassa.

Mheshimiwa Spika, magari hayo yamehifadhiwa katika yadi ya Halmashauri yakisubiri utaratibu tija kama itakavyoamuliwa na uongozi wa Halmashauri. Halmashauri kwa sasa inaendelea kuwahudumia

wananchi wake wote kwa kutumia magari matano yaliyopo katika vituo vya Afya vya Kisesa, Nyanguge, Igalukilo, khabila na gari liliopo katika hospitali ya Wilaya ikiwemo Zahanati ya Lukungu na Kituo cha Afya Nassा. (Makof)

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu yaliyotolewa, ninachotaka kuuliza baada ya wahandisi kushindwa kujaza mambo yanayoitwa vidadisi bei na sasa ni awamu tatu za Bajeti tangu mwaka 2010 mpaka leo tunajadili Bajeti ya 2012/2013. Wizara kama Wizara inawasaidiaje watu hawa ambapo wanasubiri utaratibu ambao utaleta tija ni utaratibu upi ili muwasaidie haya magari. Aidha yauzwe au kitu kingine kifanyike?

Mheshimiwa Spika, la pili wakati *process* hii inafanyika ilikuwa Magu moja sasa Busega imemegeka ninaamini haina hili gari linalozungumzwa la wagonjwa. Mheshimiwa Waziri unaifikiriaje Busega kupata gari la kujitegemea?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) :** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maria Hewa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hili jambo analolisema Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa ni kweli na hivi tunavyozungumza hapa *RAS* yupo ananisikia hapa wa Mkoa huu wa Mwanza ambao kwa kipindi hiki cha mpito bado anakaa pale. Tunayo barua

nimezungumza na Kordeli Ngurudungi ambaye ndiye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu kuhusu jambo hili linalozungumzwa hapa na akaniambia kwenye barua ile ambayo wameandikiwa kutoka kwenye ofisi ya *RAS* ilielekezwa kwamba tuangalie uwezekano wa kuyauza haya magari na hapa nimeitaja hii *Community Development and Relief Agency* ambayo ndiyo iliyotoa msaada huo, wako pale mpaka sasa hivi tunapozungumza hapa. Kwa hiyo, ukitaka kuuza pale lazima urudi kwa yule aliyekupa gari ili kupata ridhaa yake kwamba ufanye hivyo au usifanye hivyo ndicho ambacho kimebaki pale.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna tatizo hili la vipuri kama nilivyoeleza hapo mwanzo ni tatizo kubwa sasa wataangalia na wakishaafikiana na yule mtoaji wa huo msaada wanaweza wakaenda katika hatua hiyo inayozungumzwa.

Pili, anazungumzia kuhusu hii *Development* mpya ni kweli sasa tunazungumza hapa Busega ni Wilaya mpya utaratibu wa nchi wakati unapokuwa umegawanya mamlaka hizi na tawala hizi zinataka sasa Halmashauri ile ikae pamoja na ile nyingine wote kwa pamoja wagawane mali pale. Kwa hiyo, sasa hivi tunapozungumza hapa huduma zote zinatoka kwenye ile Halmashauri Mama kwa maana ya Magu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wakati utakapofika wataketi wale wa Magu na hawa wa Busega watakaa vizuri. Cha kuchunga hapa ni ku - *maintain* uhusiano mzuri kati ya hizi Wilaya mbili mpya kwa sababu Wilaya

ile ilioanzishwa mpya kwakuwa Wilaya mpya ilioanzishwa ndiyo huwa ina- *suffer*. Kwa kawaida tukiangalia utaratibu unavyokuwa na ninatoa maelekezo hapa mpaka tutakapokuwa tumeunda Halmashauri ya Wilaya ya Busega huduma zote muhimu pamoja na *Ambulance* na vile vingine vyote vinavyotolewa kule vitaendelea kutolewa na Halmshauri ya Wilaya mama. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Richard Ndassa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba kuitia kituo chake cha Afya cha Nyambiti hakina gari tufanyeje ili tupate gari?

**SPIKA:** Mheshimiwa Richard Ndassa yaani wewe unauliza tu na mimi nataka gari sasa tutafanyaje? Naomba hilo swali walilette wakati wa Wizara ya Afya. Tunaenda Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Mheshimiwa Haji Khatibu Kai atauliza swali. (*Makofi*)

Na. 96

### **Itifaki ya Viongozi Nchini**

**MHE. HAJI KHATIB KAI** aliuliza:-

Kutokana na mabadiliko ya Katiba ya Tanzania, Zanzibar ya kuwa na Serikali yenyewe Muundo wa Umoja wa Kitaifa kumesababisha ongezeko la viongozi huko

Tanzania, Zanzibar hivyo kuchanganya itifaki ya viongozi wa kitaifa wa Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA)  
alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa napenda kujibu swali la nyongeza la Mbunge wa Micheweni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kutokana na mabadiliko ya Katiba ya Zanzibar mwaka 1984, hasa Sura ya nne inayozungumzia muundo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, imepelekea utaratibu wa Kiitifikasi kwa viongozi wa kitaifa kubadilika, mabadiliko haya ya mwaka 2010, katika Katiba ya Zanzibar yameondoa kiti cha Waziri Kiongozi kama ilivyokuwa awali na kuanzisha utaratibu wa makamu wa kwanza na Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar. Kutokana na hali hii, itifaki ya sasa kwa viongozi wa Kitaifa ni kama ifuatavyo:-

1. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
2. Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
3. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

4. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
5. Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar; na
6. Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini ya Wizara kwamba kwa maelezo haya, naamini kwamba kuanzia sasa hakutakuwa na utata wa Itifaki ya Viongozi wa Kitaifa. (*Makofii*)

**MHE: HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante SANAkwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza yenyе kifungu (a) na (b) kwa kuwa, cheo cha Waziri Mkuu ni cha kuteuliwa na Rais na kwa kuwa, Rais wa Zanzibar amechaguliwa na wananchi. Je, kiitifikasi Waziri Mkuu na Rais wa Zanzibar ni nani mkubwa kiutawala?

**SPIKA:** Hili la ukubwa tena itifaki siyo ukubwa haya. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa napenda kujibu swali la nyongeza la Mbunge wa Micheweni, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa kwenye jibu langu la msingi nimeeleza na iko dhahiri kabisa na masuala ya Itifiki hayaonyeshi nani ni mkubwa. Lakini pia masuala

haya yako kikatiba na nimeeleza dhahiri kabisa kwamba anaanza Rais wa Jamhuri ya Muungano, wa pili anafuata Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, na wa tatu ni Rais wa Zanzibar, wa nne ni Waziri Mkuu. (*Makof*).

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, kwa majibu aliyotoa Naibu Waziri kwamba Serikali inatambua *protocol* iliyopo kwa Makamu wa Rais wawili wa Zanzibar. Ukitiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haitambui Makamu wa Rais wawili wa Zanzibar, bali inatambua Waziri Kiongozi.

Je, hamwoni kwamba kwa *protocol* hiyo mnavunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa napenda kujibu swalil la nyongeza la Mheshimiwa Ezekiel Wenje, Mbunge wa Nyamagana.

Kwanza kabisa wote mnatambua kwamba mabadiliko haya ya Katiba ya Zanzibar yalikuja mwaka 2010 na wote tunatambua kwamba na sisi katika Jamhuri ya Muungano tuko katika wa kuleta maoni ya Katiba mpya hivyo basi tusubiri yoyote mwenye mapendezo yake asubiri wakati huo aweze kutoa maoni na ninaamini suala hili litashughulikiwa ipasavyo. (*Makof*)

**Matumizi ya Sheria ya Ununuzi wa Vifaa vya Serikali Na. 21/2004**

**MHE. DKT. MARTY M. MWANJELWA** aliuliza:-

(a) Je, ni kwa nini licha ya kuwa na Sheria Na. 21 ya Mwaka 2004 ya Ununuzi wa vifaa vya Serikali zoezi la kutangaza zabuni zilizokwisha tangazwa na Wakala wa huduma ya ununuzi wa Serikali bado zinaendelea?

(b) Je, ni hatua gani zitakazochukuliwa dhidi ya Halmashauri na Taasisi za Serikali zinazoendelea kukiuka Sheria hiyo mpya na kuleta mkanganyiko mionganoni mwa Wazabuni?

(c) Je, Serikali haioni kuwa jambo hilo linaweza kuiingizia gharama kubwa na upotevu wa fedha zinazotokana na kodi za wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Mbunge viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kabisa baadhi ya Taasisi za Umma zikiwemo Halmashauri zinaendelea kutangaza zabuni zilizokwisha kutangazwa na Wakala wa Huduma ya ununuzi Serikalini kwasababu zifuatazo:-

(i) Uelewa mdogo juu ya mfumo wa ununuzi wa pamoja wa vifaa na huduma mtambuka.

(ii) Sheria ya ununuzi wa Umma Na. 21 ya 2004, kutotamka wazi kwamba, Taasisi za Umma sharti zitumie utaratibu wa kununua kwa pamoja utakaoandaliwa na Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini.

(b) Hatua zilizochukuliwa na Serikali baada ya kugundua kuwa baadhi ya Taasisi za Umma zinaendelea kutangaza zabuni zilizokwisha tangazwa na Wakala ni pamoja na:-

(i) Serikali ilitoa maelekezo kwa Makatibu Wakuu, Wakuu wa Idara zinazojitegemea, Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma na Wakala za Serikali Tanzania Bara, tarehe 18 Juni, 2010 waraka namba CFA /140/150/01/09 iliyozielekeza Taasisi za Umma kutumia mikataba ilioandaliwa na Wakala kufanya Ununuzi wa Pamoja wa vifaa na huduma mtambuka.

(ii) Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini allendesha mafunzo tarehe 5 Mpaka tarehe 15 Machi, 2011 kwa nchi nzima kwa watumishi 4,016 kwa Taasisi za Umma wanaoshughulika na masuala ya ununuzi pamoja na wafanya biashara. Aidha Serikali imefanya mapitio ya Sheria ya ununuzi wa Umma Namba 21 ya 2004 na kuweka vifungu vinavyoelekeza Taasisi za Umma kutumia mfumo huu.

(c) Ni kweli kwamba Taasisi za Umma kuendelea kutangaza Zabuni kutaiingizia Serikali gharama kupitia eneo la ununuzi wa Umma. Hivyo basi, Serikali imeamua kurekebisha Sheria ya ununuzi wa umma na kuainisha wazi matumizi ya mfumo huu. (*Makof*)

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Waziri ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza yenyé (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mikataba mingi imekuwa kwa upande mmoja tu wa Serikali na adhabu kutolewa kwa mkandarasi akishindwa kutekeleza.

(a) Je, Serikali au Taasisi zinaposhindwa kumlipa mkandarasi kwa uzembe akimaliza kazi kwa muda inakuwaje?

(b) Sheria mpya ya manunuzi pamoja na kanuni zake itaanza lini? Ningombala Mheshimiwa Naibu Waziri atujulishe kuwa itaanza lini kutumika ili kuokoa fedha za walipa kodi zinazopotea kutokana na matumizi mabovu, nashukuru. (*Makof*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala lake la mwanzo lilihusiana na vipi Serikali ikiwa inashindwa kumlipa mkandarasi. Kwa kawaida mikataba inakuwa imeeleza wazi

*perlatus* ambazo zimo katika mkataba ule kwa pande zote mbili. Kwa hiyo, mikataba ile inakuwa inaonyesha wazi vipi kama Serikali itakuwa inakiuka taratibu husani wakati wa malipo mara nyingi tunakuwa tunalipa *interest* kwa kuchelewa kulipa mkandarasi.

Lakini matumizi ya Sheria mpya kama nilivyoeleza katika suala langu la msingi kwamba kulikuwa na marekebisho hususani yanayohusiana manunuzi ya jumla. Kwa hiyo, sheria hiyo inatumika lakini Sheria hii ikiwa itafanyiwa maboresho na tuko katika mchakato wa kuanza kukusanya maoni na Wabunge vilevile mtahusika *once* tukiwa tumemaliza na kusainiwa Sheria hiyo itaanza kutumika rasmi.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa, katika Halmashauri nyingi nchini zimetunga Sheria zinazokiuka Sheria ya ushuru wa mazao uliotangazwa mwaka 2002 na aliyekuwa Waziri wa Serikali za mitaa Brigedia Gen. Hassan Ngwilizi.

Je, Serikali inatueleza nini sasa ushuru huo unaotozwa kwa Sheria zilitungwa katika Halmashauri ambapo inakiuka Sheria mama tangazo la Waziri na haijafutwa mpaka leo na wananchi wanataabika katika Halmashauri mbalimbali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Susan huoni kuwa ilikuwa *Procurement* wewe umeenda kwenye mazao? Haya Mheshimiwa Jitu Soni oh! umeshaondoa swalilako haya tuendelee na sijaona mtu mwingine na

tunaendelea na swali linalofuata Mheshimiwa Clara Mwatuka, swali linalofuata.

Na. 98

### **Riba Kubwa Kwa Mikopo ya SACOSS na VICOBA**

**MHE. CLARA D. MWATUKA** aliuliza:-

Lengo la Serikali katika kuhamasisha wananchi kuunda vikundi vya *SACCOS* na *VIKOBA* ni kuwasaidia kujikwamua kiuchumi:-

(a) Je, Serikali inasemaje kuhusu riba kubwa wanayotozwa wananchi kutokana na fedha zao wanazoziveka benki?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mbunge wa viti maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, viwango vya juu vya riba vinavyotozwa na Taasisi na asasi za fedha vinatokana na sababu mbalimbali ikiwemo sera yenyewe ya Taifa ya Taasisi ndogondogo za fedha (*Microfinance*).

Sera inatamka kwamba, viwango vya riba kwa ajili ya mikopo vitapangwa na asasi husika bila kuingiliwa na Serikali, Benki Kuu wala wafadhili kwasababu asasi zinafahamu fika gharama za

uendeshaji, hatari/ usalama wa mikopo na mbinu za biashara.

Gharama za uendeshaji, taarifa za mkopaji, hatari/usalama wa mikopo na mbinu za biashara, kwa pamoja hujumuishwa katika kufanya maamuzi wakati wa kupanga viwango nya riba.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida, *SACCOs* na *VICOBA* hazitoi riba kubwa kama zinatumia fedha zao kukopesha, bali hukopa kwenye benki za biashara ambapo riba ni za juu na hivyo kufanya riba zao pia kuwa za juu. *SACCOS/VOCOBA* hulazimika kuongeza riba ili waweze kupata faida na kuweza kujendesha.

Hata hivyo, inatarajiwa kwamba kuongezeka kwa idadi kubwa ya asasi hizi na kuwepo kwa aina nyingi za bidhaa (mikopo) kutaleta ushindani ambao hatima yake ni kuteremka kwa viwango nya riba na kuongeza ubora wa huduma.

Mheshimiwa Spika, ni vema pia kugusia mikakati mbalimbali ambayo Serikali na Taasisi zake zimechukua katika kushughulikia tatizo la riba kubwa inayotozwa na benki na Taasisi nyingine za fedha zikiwemo *SACCOS* na *VICOBA*.

Hii ni pamoja na kuweka mfumo wa upatikanaji wa taarifa za wakopaji wa taarifa za wakopaji yaani *credit reference system*. Mfumo huu utarahisisha upatikananji wa taarifa za wakopaji na hivyo kuziwezesha Taasisi zinazokopesha kufanya maamuzi stahiki ikiwemo kiasi cha riba. Mfumo huu utatoa

mzania mzuri wa usalama wa mikopo (*safety credit vs credit risk*).

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo katika hatua nzuri za kuboresha masijala ya Ardhi (*Land Registry*) ili kurahisisha upatikanaji wa Hati za viwanja/Mashamba zitakazoweza kutumiwa na wakopaji kama dhamana na hivyo kupunguza riba inayotozwa.

Mkakati mwingine ni pamoja na kuweka mfumo wa kusimamia Taasisi zinazokopesha kwa kutumia fedha zao wenyewe. Aidha, Serikali kupitia Benki kuu inaandaa mfumo wa kuelimisha jamii ya mambo yanayohusu fedha na mikopo. Elimu ya fedha na mikopo itasaidia kuondoa hali ya wananchi kutozwa riba kubwa kwa kukosa tu uelewa wa masuala ya mikopo, riba ya mikopo. (*Makofi*)

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa fedha.

- (a) Kwa kuwa, *SACCOs* na *VICOBA* hukopa fedha zao benki na wao ndipo hukopesha wana vikundi jambo ambalo linawafanya wananchi hawa kutozwa riba mara mbili. Je, Serikali haioni ya kwamba inawapa mzigo mkubwa na kuwafanya hawa wanyanyasike?

(b) Je, isingekuwa rahisi Serikali ikafanya mpango wa kuwafanya hawa wakopeshwe na benki moja kwa moja?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali inaona mzigo mkubwa ambao unawapata wananchi hususani kutozwa riba mara mbili na ndiyo maana katika swali la msingi nilieleza hatua ambazo Serikali inachukua kwa ajili ya ku-*address issue* hii.

Kwa hiyo, Serikali tayari inaona huu mzigo na kwamba tuko katika mwendelezo wa kufanya *Credit Reference System* kwa ajili ya kuangalia hasa ile hatari ama *reference* ya yule mkopaji hivyo itarudisha chini kiwango wa riba.

Mheshimiwa Spika, lakini swali lake la pili lilisema Serikali inahakikisha vipi kwamba mwananchi wa kawaida kuweza kukopa benki moja kwa moja, nadhani katika hotuba ya Waziri wa Fedha imeeleza wazi hatua ambazo Serikali inachukua katika kuingiza mitaji katika mabenki ambao utasababisha wananchi tu wa kawaida waende wakakope kule. Kwa hivyo naomba tu turejee katika ile hotuba na tujue Serikali inafanya hatua gani katika kuelezea tatizo hili. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, *SACCOS* na *VIKOBA* imekuwa mkombozi wa wananchi wa hali ya chini hasa katika sehemu za vijijini, ningeomba kuuliza ni lini *VIKOBA* itapewa nafasi kama ilivyo *SACCOS* ili iweze kupata mikopo kwa ajili ya kusaidia wananchi kama inavyofanyiwa *SACCOS* hasa katika lile eneo la Misenyi?

**SPIKA:** Ahsante sana, *VIKOBA* kupata hadhi ya *SACCOS* Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali na wadau wote wengine wamegundua kwamba *VIKOBA* ni mfumo ambao umeweza kuwatoa wananchi wengi katika dimbwi la umaskini. Kwa hiyo, nadhani ni ushauri mzuri na sisi tunauchukua tutakwenda kuufanyia kazi ili *VIKOBA* vyenyewe navyo vipate hadhi *SACCOS* ili kuweza kuwasaidia wananchi. Siwezi nikatoa tarehe maalum lakini hili ni suala zuri na Serikali italichukua tutalifanyia kazi. (*Makofî*)

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa, nchi nyingi Duniani zina mfumo wa kuwataka mabenki yanayowekeza ndani ya nchi yao kuchangia katika huduma za maendeleo. Je Serikali yetu ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba mabenki yanayowekeza ndani ya nchi yetu yanachangia kwenye mifuko ya *SACCOS* na *VIKOBA*?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Spika, Serikali si tu kwenye Mabenki, lakini na makampuni mengine ya uwekezaji inayataka lazima watimize wajibu wao kwa jamii yaani (*Cooperate social responsibility*) kwa hiyo huo ni wajibu wao. Lakini Serikali haim-confine benki ama shirika kuweza kusaidia VIKOBA parse lakini inataka iwe inahudumia jamii kama ni *part* yake ya *cooperate social responsibility*. Kwa hiyo hilo itakuwa ni wajibu wa mwekezaji mwenyewe, ni wajibu wa kampuni yenyewe na ni wajibu benki yenyewe lakini nalo si suala baya. (*Makof*)

**SPIKA:** *VIKOBA* na *SACCOS* isije ikaonekana ni mambo ya akina mama tu, Mheshimiwa Mpina swali la mwisho la nyongeza.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa hivi sasa hapa nchini tuna tatizo kubwa sana la riba za mabenki kwamba riba hizi zipo juu sana, *avarege* ya riba sasa hivi katika *Financial Institutions* imefikia asilimia 33, wanatoza riba ya asilimia 33 ambayo ni kumbwa mno na kwamba haiwasaidii kabisa hawa wananchi wanaoenda kukopa badala yake ni kufilisiwa malli zao.

Kwa kuwa tatizo la riba kuwa kubwa linasababishwa na upatikanaji wa mitaji ambako *Financial Institution* pamoja na *Commercial Bank* kule wabakopata mitaji kwa ajili ya kukopesha wateja wao. Je Serikali ina mpango gani wa kuweka utaratibu mahsus wa zile *Unit Cost* ili waweze ku-regulate hizi riba za mabenki kwa sababu hakutakuwa na sababu

tena ya kuwa na mabenki ya kukopesha wananchi kwa sababu yanawafilisi badala ya kuwasaidia?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba kumpongeza Naibu Waziri wangu kwa majibu yake mazuri ambayo ameyatoa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mpina anataka kujua ni namna gani Serikali inaweza kuwa na *strategies* ya kupunguza gharama ya kukopesha (*Cost of Lending*).

Mheshimiwa Spika, naomba kwa manufaa ya Wabunge wote nitoe mambo manne ya msingi ambapo mabenki yanafanya ili riba ile iweze kuwa ipo. Kwanza, ni gharama ya kuwa na pesa ile iliyo mkononi (*cost of borrowing*), wao wameipata kwa gharama gani, kwa hivi tunaanzia hapo.

Pili ni gharama au athari au yule anayekopa wanamtizama anaweza akawa na uwezo wa kurudisha au namna gani (*Borrowers risk*) na katika hilo wanatazama vigezo vitatu. Kigezo cha kwanza je huyu anayekopa biashara yake ina uwezo gani wa kurudisha pesa, kigezo cha pili wanatizama uwezo wake wa huyu anayetaka kukopa yaani (*borrowers capacity*) na *intergrity* yake, na kigezo cha tatu wanatizama je ikiwa hatalipa hela ile itarudi namna gani (*collateral au security*).

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la tatu kinachokuwa katika *component* ya *interest rate ni cost of doing business* yaani ni gharama gani wao wanaikabili katika kuendesha ile shughuli. Kwa hiyo kazi ya benki ni sawa na kazi zingine katika

kugharamia. Kwa hivyo kuna gharama ya umeme, kuna gharama ya mishahara, kuna gharama ya uendeshaji kwa hivi nayo inaingia katika *element* ya *costing* ya *ile interest rate*.

Mheshimiwa Spika, nne wanatizama kitu kinaitwa (*profit margin au mark up*), hiyo inakuwa katika namna gani wao wata-peg ili kiwango gani ili nao waweze kuwa na faida. Kwa hivyo wanapo-*calculate interest rate* wanatizama vyote vinne kwa mpigo. Sasa hali ya Tanzania bado gharama ya kukopesha iko juu kwa sababu ya vitu vya msingi ambavyo bado lazima tuvifanyie kazi katika uchumi kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, kwanza *from the supplies side* yaani upande wa wakopeshaji. Je, wapo wa kutosha ili wao wenyewe washindane ili gharama ya kukopesha iweze ikapungua. Kwa hivi ni kazi ya Serikali tunatizama namna gani ya kuboresha hali ya *financial institutions* katika nchi hii ili kwanza ziweze kuwa nyingi na zikishakuwa nyingi zinaposhindana ile riba yenyewe nayo itaanza kuteremka. Kwa hivi kuna vitu vingi tunatizama kisayansi ili viweze vikaja vikasaidia kwa muda mrefu katika hali halisi ya kuteremsha *interest rate*. Ahsante sana. (*Makof!*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na majibu haya ya mwisho ni semina ya bure, kwa hiyo, tunashukuru kwa elimu hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, wageni tulionao hapa kwetu. Tunao Madiwani 35 kutoka Kata zote za Jimbo la Handeni wakiongozwa na Mwenyekiti wa

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni Ndugu Ramadhani Diliwa, naomba mahali walipo wasimame kama wapo ndani, karibuni sana kumbe ni watatu tu. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge tunao wanafunzi hamsini kutoka shule ya sekondari ya Bihawana pamoja na walimu wao, Walimu na wanafunzi naomba msimame mlipo, ahsante sana wengine wapo huku nyuma, karibuni sana tunaomba msomo kwa bidii. Siku hizi kusoma ni kushindana, karibuni sana. Tuna wanafunzi na walimu 55 kutoka Kanisa la Pentekoste Jimbo la Dodoma wapo wapi ahsanteni sana. Tunashukuru sana na ninyi pia mkaizane kusoma, msome vizuri. Halafu tuna wanafunzi na walimu 85 kutoka shule ya msingi ya Amani ya Dr es Salaam wako wapi? Ahsanteni sana poleni na safari karibuni sana nadhani mtajifunza mambo machache hapa kuhusu mwenendo wa Bunge ahsanteni sana. Kuna wanafunzi na walimu 52 kutoka shule ya msingi Ignusius ya Dodoma wapo *basement* wamekosa nafasi labda baadaye watapanda huku juu.

Waheshimiwa Wabunge kuna wanafunzi 30 kutoka chuo Kikuu cha Dodoma ambao ni wageni wa Waheshimiwa mbalimbali hapa Bungeni, wanafunzi wote wa *UDOM* mahali walipo wasimame, karibuni sana tunawatachia masomo mema. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo yanayohusu shughuli za Kamati. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo hii saa saba

mchana kutakuwa na kikao cha Kamati katika ukumbi wa chumba Namba 231. Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa John Lwanji, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo saa saba mchana kutakuwa na kikao cha Kamati katika ukumbi Na. 227.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mahamoud Mgimwa, anaomba niwatangazie Wajumeb wa Kamati yake hiyo kwamba leo saa saba kutakuwa na kikao katika Ukumbi Na. 219.

Waheshimiwa Wabunge nina tangazo linalotoka kwa Katibu wa Wabunge wa CUF Mheshimiwa Magdalena Sakaya anaomba niwatangazie Wabunge wote wa CUF kuwa wanatakiwa kuhudhuria kikao kitakachofanyika leo saa nane mchana ukumbi wa Msekwa C.

Mheshimiwa Yahya Kassim Issa wale watu wako hawakukutana siku ile? Anaomba niwatangazie Wabunge wote wanaoishi magorofa ya *site* moja, mbili, tatu na nyumba za kisasa wanaombwa wakutane leo saa saba mchana baada ya kumaliza kikao cha Buneg ukumbi wa Pius Msekwa, sijui siku ile hawakukutana basi mnaombwa tena mkutane anasema ni muhimu sana kuhudhuria kwa wale wote wanaohusika, kuhudhuria kwenu ndiyo mafanikio mnayokwenda kuongea.

Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbarak, Mbunge wa Viti Maalum, amefiwa na mama yake mzazi usiku wa kuamkia leo na watakuwa na maziko huko Zanzibar siku ya leo. Tunayo taarifa tena Mheshimiwa Waziri Wassira naye amefiwa na mama yake mzazi ndiyo maana hamumwoni hapa amefariki kuamkia leo. Kwa hiyo tuwaombee wazee wetu hawa Mwenyezi Mungu apumzishe roho zao mahali pema peponi. Ahsanteni sana, tunaendelea.

**WABUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Unajua mimi matumizi ya mwongozo huwa sielewi, kwa sababu toka tumeanza ni maswali ya Waziri Mkuu na maswli ya kawaida na mimi, sasa mwongozo haya hebu tusikilize na kama siyo sahihi nitawaambia siyo, Mheshimiwa Dkt. Mbassa.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kupitia Kanuni ya 68 (7), mapema wakati wa kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu kuna Mbunge mwenzetu ameliarifu Bunge hili kwamba kuna kikundi cha watu ambacho kinachanga fedha kuwapa Madaktari kushinikiza mgomo na suala hili ni suala ambalo linagusa maisha ya watu na ni suala ambalo halipaswi kufanyiwa mzaha.

Naomba mwongozo wako Mbunge huyu kwanini asikitaje hicho kikundi ili kurahisisha kazi ya Serikali kusuluhisha mgomo huo, ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Bahati nzuri wakati anajibu yule aliyeulizwa alisema na wao wamesikia sikia na utafiti unaendelea.

**WABUNGE:** Kelele.

**SPIKA:** Ndivyo alivyosema! Kwa hiyo tunaomba huo utafiti uendelee. Mnapiga kelele kwa sababu gani?

Mheshimiwa Mnyika Mwongozo mwingine.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 116 ambayo naomba niisome, Mbali na majukumu ya msingi ambayo yameorodheshwa kwa kila Kamati ya Kudumu, Kamati yeote inaweza kupendekezwa kwa Spika ipewe majukumu ya nyongeza ambayo yatatajwa katika pendekezo hilo, na vile vile Spika anaweza kukabidhi jambo lingine lolote kwa Kamati yeote kadri atakavyoona inafaa kwa ajili ya kushughulikiwa na Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba niweke mkazo kwenye maneno. Vile vile Spika anaweza kukabidhi jambo lingine lolote kwa Kamati yeote kwa kadri atakavyoona inafaa kwa ajili ya kushughulikiwa na Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba ninukuu Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayosema sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndiyo chombo kikuu cha Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, ambacho kitakuwa na Madaraka kwa niaba ya wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna mambo yametokea mapema leo na jana. Mosi ni taarifa tulizoelezwa jana na Naibu Spika kwamba Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii ambayo ilipewa kazi mwezi Februari mwaka 2012 kuhusu suala la madai ya madaktari ilishakamilisha kazi yake na kwa taarifa tuliyoelezwa jana Bungeni tayari taarifa hiyo imekwishapelekwa Bungeni. Lakini mimi ni mbunge na sijawahi kupewa nakala ya hiyo taarifa na hiyo taarifa haijawahi kuja Bungeni.

Lakini leo vile vile tumeelezwa hapa kwamba Serikali imeacha kutoa kauli leo ambayo ilikuwa kwenye orodha za shughuli za leo kwa maelezo kwamba kuna mambo bado inayafanya kazi, hali ambayo inaoonesha kwamba mpaka katika hatua ya sasa na kwa kuwa mgomo unaendelea upo kwenye hali mbaya, Serikali imeshindwa kushughulikia tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeshindwa kushughulikia tatizo hili, ningeomba mwongozo wako ili uweze kutumia madaraka yako kwa mujibu wa kifungu cha 116 cha Kanuni ili kuweza kuelekeza Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, ifanye mambo mawili muhimu. Moja itupatie sisi Wabunge nakala ya ile taarifa ambayo imetumia siku nyingi sana kufanyiwa

kazi na imesikiliza pande zote mbili tofauti mbali na hizi taarifa za upande mmoja tunazopewa na Serikali.

Lakini la pili, Kamati ya Bunge iweze kuingilia kati kusuluhisha kwa sababu hapa mgogoro ni kati ya Serikali na Madaktari na Serikali imeshindwa kutatua mgogoro ili Bunge tusionekane na sisi Wabunge na Bunge tunazembea kuchukua hatua. Kamati ya Bunge iingilie kati ishughulikie maana yake maisha ya watu yanapotea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. (*Makofi*)

**SPIKA:** Haya, na hiyo Kanuni ukisoma inasema Spika anaweza kutoa majibu baadaye, sasa naomba Katibu endelea na *Order Paper*.

## KAULI ZA MAWAZIRI

### Mgomo wa Madaktari Nchini

**SPIKA:** Nimesema huyu nitamjibu baadaye, kwa sababu majibu yake yanalingana na ninachotaka kusema katika hatua inayofuata ya *agenda* ya siku ya leo. Kauli ya Waziri tulioambiwa kwamba itatolewa leo haitatolewa. Sababu zake ni kwamba, Mhimili mwingine umelalamika kwamba wao wanashughulikia masuala yanayokuwa katika Mhimili wao. Sisi hapa tunaendelea kutoa taarifa. Kwa hiyo, hiki kipengele hakitakuwepo leo cha Kauli ya Mawaziri.

Vivyo hivyo hiyo taarifa anayosema Mheshimiwa Mnyika, ile Kamati niliagiza wakae na Serikali wajadiliane kauli iliyotolewa hapa na Waziri aliyehusika. Walifanya hiyo kazi, walikwenda Dar es Salaam na Kamati yangu ya Uongozi tulikutana na tuliwaleta na ndege usiku kutoka Dar es Salaam ili waweze kuitolea *briefing* Kamati ya Uongozi kuhusu kazi waliyokwenda kufanya kule. Wakatoa taarifa yao, tulikaa mpaka saa saba usiku tukakubaliana kwamba taarifa ile haitaletwa Bungeni hapa kwa sababu ipo katika mikono ya *Executive*. Sisi siyo wa kujibu mambo ya *Executive* hapa tuna kazi yetu. Hivyo ndivyo tulivyokubaliana.

Kuna mengine ambayo walipendekeza usiku ule, tulikubaliana kwamba, mimi nitaenda kuwashauri wanaohusika wachukue hatua zinazostahili. Kwa bahati hatua zile zilichukuliwa, hiyo taarifa imepelekwa *Executive* na wamefanyia mambo mengi yanayoendelea. Kwa hiyo, haitakuja hapa kwa sababu mimi ndiyo niliyewaagiza wafanye hiyo kazi na Kamati ya Uongozi walipitia hiyo taarifa na wakatoa taarifa inavyostahili. Hivi sasa suala hili lipo Mahakamani, naomba lifungwe. Tunaendelea. (*Makofii*)

## HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka  
2012/2013 – Ofisi ya Waziri Mkuu  
na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nina orodha hapa ya wachangiaji, kuna ambao hawajachangia hata mara moja wanafikia 55 na waliochangia mara moja wanafika 46. Kwa hiyo, kwa mujibu wa taratibu zetu, tunaanza na ambao hawajachangia hata mara moja ambapo yupo Mheshimiwa Abdalla Haji Ali na Mheshimiwa Yusuph Haji Khamis.

**MHE. ABDALLA HAJI ALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyenijalia leo na mimi kunipa uwezo wa kusimama hapa katika Bunge lako Tukufu. Pia nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii. Ninakupongeza wewe binafsi na Watendaji wako katika Kiti chako hicho, kwa kuhimili mikiki mizito ya Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilisikiliza Hotuba ya Waziri Mkuu kwa umakini kabisa na mwisho nikagundua kwamba, katika Hotuba yake ya mwaka huu kuna upungufu. Kama kawaida yake, Mheshimiwa Waziri Mkuu ametaja angalau kwa kifupi masuala ya elimu, umeme, kilimo, utalii, afya, uvuvi na mambo mengine. Upungufu niliougundua katika Hotuba yake hii hakutaja hata kipengele kimoja kuhusu suala la nyumba na maendeleo ya makazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii inakwenda kinyume na Hotuba yake ya Bajeti ya mwaka uliopita, ambayo alizungumzia suala hili kwa kina na uthibitisho ukapatikana katika Hotuba yake ya mwaka 2011/2012, ukurasa wa 28, naomba ninukuu: "Nyumba na

maendeleo ya makazi: Mheshimiwa Spika, Serikali imehamasisha mabenki na vyombo vingine vya fedha kutoa mikopo ya ujenzi wa nyumba ya muda mrefu na yenye riba nafuu kupitia Sheria ya Mikopo ya Nyumba Namba 17 ya Mwaka 2018. Sheria hiyo, imewezesha baadhi ya mabenki kutoa mikopo kwa ajili ya kununua na kujenga nyumba kwa masharti ya kurejesha mikopo hiyo ndani ya miaka 15." (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri Mkuu atakapokuja kufanya majumuisho ya Hotuba yake hii, hili ni suala muhimu sana, kifungu hiki nacho akipe nafasi akiyeke katika Hotuba yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na hilo, nimeona angalau kwa maneno machache kabisa nizungumzie suala la nyumba na maendeleo ya makazi. Sote tunafahamu kwamba, mwendelezaji mkuu wa ujenzi wa nyumba katika nchi yetu ni Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*). Shirika hili ni la kupigiwa mfano; ni Shirika lenye kuleta maendeleo makubwa katika nchi hii na ni vizuri mashirika mengine yakaiga mwenendo mzima wa Shirika hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika mafanikio yake Shirika hili, naomba kwa uchache nitaje Shirika la Nyumba, hatua yake ya mwanzo lina hazina ya ardhi eneo la kutosha, eneo lipatalo ekari 562.8 katika maeneo mbalimbali ya nchi, ambapo ekari 202.2 zipo eneo la Kibada, Kingamboni - Dar es Salaam ambalo wamekusudia kujenga nyumba zipatazo 223 za bei nafuu kwa ajili ya wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika mafanikio yake, vile vile Shirika lina Miradi kumi yenye nyumba 827, kati yake Miradi mitatu imeshakamilika ya nyumba 86 kwa ajili ya kuuzwa na nyumba 741 zinaendelea kujengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile Shirika kwa mwaka huu limekusanya makusanyo ya pango yenye kuvuka lengo kabisa. Shirika lilijipangia au lilikadiria kukusanya shilingi bilioni 43.1, lakini mpaka Mei, Shirika kwa ufanisi kabisa limefanikiwa kukusanya shilingi bilioni 47.2, sawa na asilimia 146. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Shirika hili linafanya kazi na wafanyakazi wake hawana miujuza kutoka Mbinguni, siri yao kubwa ni ushirikiano, wanashirikiana vizuri. Wakurugenzi wako huru kuendesha Idara zao bila kubughudhiwa. Shirika hili lina wabunifu mahiri kabisa waliokusudia kwa dhati kuweka historia katika nchi hii kuitia Shirika lao. Nachukua fursa ya makusudi kuwapongeza Wafanyakazi wa Shirika la Nyumba. Pongezi pekee zimwendee Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba, Ndugu Mchechu; kijana huyu ni mahiri, ni makini na ni mchapakazi mkubwa. Naiomba Serikali impe ushirikiano mkubwa na ana nia ya dhati kuipeleka nchi hii mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, penye mafanikio hapakosi changamoto au matatizo; Shirika la Nyumba linakabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo mionganoni mwao moja ni Kodi ya VAT kwa Serikali. Shirika hulazimika kuzipandisha nyumba bei ili kufidia tatizo hilo. Tulielezwa nyumba inaweza kuuzwa pengine

kwa shilingi milioni 25 lakini kulinganisha na gharama nyingine zinazoingizwa pale za VAT, nyumba hufikia shilingi milioni 35 mpaka shilingi milioni 40. Naiomba Serikali iwaondolee Shirika la Nyumba Kodi ya VAT na iwapatie fursa ya kuwauzia bei mwafaka wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine inayowakumba watu wa Shirika la Nyumba ni pale wanapokwenda kuwekeza katika maeneo mapya hulazimika kupeleka miundombinu ya maji, umeme na barabara. Yote hii ni gharama ambayo hujumuishwa kwenye manunuzi ya nyumba na nyumba ikawa ni ghali hainunuliki. Vile vile na nyumba ya Serikali ijewekeze kwenye miundombinu katika maeneo haya mapya ili Shirika lipate nafuu ya kuwapunguzia wananchi bei. (*Makofi*)

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa ruhusa yako. Nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu, kwa kuniwezesha na mimi kushiriki katika Kikao hiki cha Bajeti. Pia nakushukuru wewe Mheshimiwa Spika, kwa kuniruhusu kusimama kuchangia Hotuba iliyopo mbele yetu. Siku kama ya leo tarehe 12 Aprili, 2012 katika Kipindi cha Maswali ya Papo kwa Papo, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, alimwuliza Waziri Mkuu, naomba kunukuu alivyomwuliza: "Ni kiasi gani kimerudi na Mheshimiwa Waziri Mkuu hizo fedha zitapelekwa kwenda kunusuru Sekta ya Elimu na zitagawanywa kwa utaratibu gani ili kuhakikisha kwamba zinatimiza kusudi lillokusudiwa." (*Makofi*)

Hizi zilikuwa fedha za ujisadi wa rada ambao tunazitakasa kwa ajili ya chenji za rada. Halafu katika Kitabu hiki cha Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, katika ukurasa huu unaoning'inia sijui ukurasa namba ngapi huu hapa, umeelezea hivyo hivyo kuhusu fedha za rada. Alivyojibu Waziri Mkuu na majibu yaliyopo katika ukurasa huu yanalingana. Kwa hiyo, hakuna wasiwasi kwamba, Baraza la Mawaziri limekaa na kuzigawanya fedha hizi. Fedha hizi zimegawiwa katika shule za msingi Tanzania Bara peke yake na hizi fedha ni za Jamhuri ya Muungano kwa kupitia Jeshi la Wananchi wa Tanzania. (*Makofi*)

Kinachonishangaza, katika Baraza la Mawaziri, tunao Mawaziri kutoka Zanzibar, ambao walikuwa wana haki ya kuitetea haki hii kwenda Zanzibar, lakini mpaka leo sijasikia kauli yoyote waliyotamka na Zanzibar hakukupelekwa kitu chochote. Nataka kujua kama kilikuwepo Kikao cha Baraza la Mawaziri na wao hawakuchangia chochote na haki ya Zanzibar ikapotea au kama walikaa Watanzania Bara peke yao wao hawakupata nafasi ya kuzungumzia kitu chochote basi pia walitakiwa watoe kauli tuisikie kwamba na wao wametetea Zanzibar kuhusu fedha hizi. Kutokana na kwamba wao hawakuwajibika kuwatetea Zanzibar, nafikiria Zanzibar yapo matatizo chungu nzima ya shule za msingi, madawati hakuna na vyoo hakuna, lakini wameshindwa kutetea basi mimi naomba wawajibike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kuwajibika hawa Mawaziri, nitanukuu Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Ibara ya 54(1) inayosema kwamba: "Kutakuwa na Baraza la Mawaziri ambalo Wajumbe wake watakuwa ni Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Rais wa Zanzibar na Mawaziri wote. Huyu Rais wa Zanzibar ninamvua hatakuwemo lakini Mawaziri wale walioteuliwa na Rais Jakaya Mrisho Kikwete kutoka Zanzibar, naomba wawajibike kwa sababu hawakuitendea haki Zanzibar. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, hawa Mawaziri wanafanya kitu kimoja. Sasa unawatoaje wao katika Baraza lao? Wewe dai hela ya chenji tu.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, mimi nimekuwa nikishangaa sana kuhusu hizi fedha za ujisadi wa rada huu, tumekuwa tunashabikia kama pamepita jambo la kawaida tu. Wabunge wamekuwa kila mmoja anaziomba hizi fedha zikatumike katika Jimbo lake pasipo aibu, sijui pana matatizo chungu nzima kana kwamba tumefanya biashara yenye faida kubwa sasa tunashangilia tumepeata mapato kumbe tunakwenda mahali pabaya sana. Kulikuwa kuna mambo ya msingi ya kushughulikia, kwanza, watafutwe akina nani walihusika wapelekwe katika vyombo vyasheria ili wawajibike. Ujisadi Tanzania unakua mkubwa na unaimeza Tanzania kila siku. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tuna ujisadi chungu nzima, leo Tanzania imekuwa kama jambo la kawaida; mara utasikia kuna ujisadi wa rada, kuna ujisadi wa *EPA*, ujisadi wa *Richmond*. Sasa hivi pia nimesoma gazeti

jana au juzi, kuna matrillioni ya shilingi ambayo yanatajwa yamefanyiwa ujisadi ndani ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sasa Taifa hili halifiki mahali pazuri, tutakuwa tuna kazi kubwa sana za kupeleka mahali pazuri halafu vizazi vinyavyokuja vitatushtaki kwa Mwenyezi Mungu. Neema ya Mungu kaiweka ndani ya Tanzania nyingi juu na chini; chini tuna madini na juu ardhini tuna miti na kila kitu lakini tunakwenda vibaya sana. Tugeuze njia tuelekee mahali ambapo tumekusudia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, juzi wakati nikiwa katika Bunge hili hili wamesimama Waheshimiwa Wabunge hapa wamesema tumegundua gesi nyingi, imetajwa kwa matrillioni, kwa mapipa, tutauza. Kama hatuna mwelekeo mzuri hata tuzalishe kitu gani tutabaki hapa hapa. Watu wengine wanasonga mbele sisi tunabakia nyuma. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini maneno ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere tunakuwa tunayatamka ndani ya mdomo hatuyatendei kazi? Hii ni aibu kwa Taifa hili; kila anayekaa utamsikia ana-quote maneno ya Mwalimu, Mwalimu kasema kupanga ni kuchagua kumbe tunawanyima watu maendeleo, tunachelewesha maendeleo. Hebu tufanye juhudi ya makusudi kumuezi Mwalimu. Mwalimu alikuwa na uchungu wa nchi hii na mambo haya mabaya hayakuwahi kutokea enzi za Mwalimu. Kwa nini hatuwezi kufuata nyayo za Mwalimu kwa vitendo?

Mimi nina-quote usemi wa Mwalimu ambao amesema ili tuendelee tunahitaji mambo manne; Ardhi, Watu, Siasa Safi na Uongozi Bora. Inaonekana Uongozi wa CCM siyo bora na ndiyo unatupeleka hapa. Kwa nini twende hivi? Lazima twende vizuri. (*Makofi*)

Leo sisi tuna madini chungu nzima, nimetembelea Geita kule na Kamati ya Nishati na Madini, kuna mashimo makubwa ambayo hayafukuliki hata siku ya kiama. Watu wanachukua mali, sisi tunabakia. Ukienda kule, watoto shule zao hafifu, hawana madawati, hawana *dispensary*, barabara chafu, maji ya kunywa pia hamna, mali zinatoka katika ardhi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo kubwa kwa nchi yetu, lazima turudi nyuma tuangalie, nchi hii itakuwa kila mwenye mikono mikubwa anakuja kuchota mali, sisi tunabaki kuangalia. Kitakachopatikana kitakuwa kigumu na itabakia historia tu, mashimo yaliyokuwepo yanayochimbwa madini, yanabakia kama yalivyo halafu vizazi vyetu vitakuja kutulaani na tuna wajibu wa kwenda kujibu hoja kwa sababu wengi tunaamini tutakufa, tutakwenda kujibu hoja juu ya urithi, mali Mungu aliyowapa Watanzania halafu vlongozi tukashindwa kusimamia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati umefika...

(*Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

**SPIKA:** Umefika kumaliza. (*Kicheko*)

Ahsante Mheshimiwa. Sasa namwita Mheshimiwa Hussein Amar na Mheshimiwa Dkt. Antony Mbassa ajiandae na Mheshimiwa Jenista Mhagama ajiandae.

**MHE. HUSSEIN NASSOR AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Waziri Mkuu. Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ameniwezesha kunipa afya njema na kuweza kusimama tena kwenye Ukumbi huu kutoa malalamiko ya Wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa kutusogezea huduma ya Kiwilaya, Jimbo la Nyang'hwale, sasa hivi ni Wilaya na Makao Makuu yake ni Karumwa. Kwa hiyo, tunaipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kutusogezea huduma ya Kiwilaya. Baada ya pongezi zangu, napenda pia nitoe taarifa kwamba, Jimbo hili la Nyang'hwale lina upungufu wa chakula kama ilivyotokea mwaka jana, lakini tunaishukuru Serikali iliweza kutuvusha mwaka jana kwa kutupa chakula cha msaada na cha bei nafuu. Tunaiomba Serikali ijipange tena kwa sababu upungufu wa chakula katika Jimbo la Nyang'hwale ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, sasa naanza kuchangia. Kuna ahadi ambazo zilitolewa mwaka jana katika maswali yangu ambayo niliuliza, hakuna hata moja ambayo imetekelvezwa. Niliulizia Serikali ina mpango gani kutekeleza ahadi za Mheshimiwa Rais alipokuja Jimboni, aliahidi mambo mengi; aliahidi

kututengenezea barabara ya kutoka Busisi kwenda Kahama kwa kiwango cha lami, alituahidi maji, utafufuliwa mtambo ambao ulikuwa umesimama tangu mwaka 1975 na Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mwanri alisema kwamba, tayari kuna pesa zimetengwa, shilingi milioni 20 kwa ajili ya upembuzi lakini hakuna ambacho kimefanyika mpaka hivi sasa!

Mheshimiwa Rais aliahidi kupandisha Kituo cha Afya cha Karumwa na kuwa Hospitali ya Wilaya lakini mpaka sasa hakuna kinachoendelea wala dalili ya aina yoyote. Hizo ni ahadi za mwaka jana na pia aliahidi kwamba umeme utawashwa, mpaka leo hii Jimbo la Nyang'hwale tunaesubiri umeme kwa hamu sana, lakini tumeoneshwa kwamba sasa hivi umeme utawashwa kwa sababu nguzo zimetupwatupwa kila eneo. Nguzo hizo hazijasimamishwa leo takriban zaidi ya miezi minane. Naiomba Serikali isije ikawachukulia hatua Wananchi wangu wa Jimbo la Nyang'hwale watakapoanza kuzichanja zile nguzo na kutumia kama kuni.

Mheshimiwa Spika, masuala ya umeme; sasa hivi tayari ni Wilaya. tunategemea umeme utakapowashwa Wilaya hiyo itakwenda kwa kasi. Tunaomba ahadi ambazo ziliahidiwa zitekelezwe na mimi nitaunga mkono hoja hii baada ya kutolewa tamko kwamba ahadi zote nilizoahidiwa mwaka jana angalau zitaanza kutekelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la elimu; tunashukuru kwamba sasa hivi walimu wameongezeka kwa kiasi

fulani, lakini bado kuna changamoto nyingi; madawati hakuna, nyumba za walimu hakuna, hii *change* ya rada ambayo inazungumzwa na sisi Jimbo la Nyang'hwale basi hebu zituangukie kwa kutengenezewa madawati na nyumba za walimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina masikitiko makubwa sana; sisi Wananchi wa Kanda ya Ziwa ukiangalia uchumi tulionao na maisha yetu tuliyonayo inasikitisha sana. Msemaji aliyemaliza kuchangia sasa hivi amesema tuna migodi zaidi ya saba katika Kanda ya Ziwa Victoria ikiwemo na Nyang'hwale, lakini ukiangalia sisi tuliozungukwa na migodi hiyo, kaangalie maisha ya wananchi walioko pale ni ya kusikitisha sana; hali ni mbaya, hakuna maji, hakuna barabara, ahadi nyingi wametuahidi watu wa migodi, tuliahidiwa kuchimbiwa visima saba na Mgodi wa Bulyanhulu, lakini tangu wametuahidi leo miaka minane visima saba hawajachimba hata kimoja. Hayo ni malalamiko na nasema kwamba, yachukuliwe kwa kina ili kujenga mahusiano yaliyo mazuri kati ya wawekezaji na wananchi.

Mheshimiwa Spika, masikitiko mengine kuhusu Zao la Pamba; Kanda ya Ziwa ni wakulima wazuri sana wa pamba, lakini hebu jaribuni kuangalia hali ya wananchi hao ilivyo mpaka hivi sasa. Wananyanyaswa na soko la pamba. Wananchi wangu wa Jimbo la Nyang'hwale msiuze pamba hiyo chini ya shilingi 1,000 na ikiwezekana iwe mara ya mwisho mwaka huu kulima pamba, limeni alizeti ambayo haina vikao. (*Makofi*)

Mwaka jana msimu wa pamba ulipofika vilianza vikao bei ikashuka na mwaka huu msimu umefika bei imeshuka; mbona hatujasikia vikao vyatya msimu wa alizeti? Ninawaomba wananchi msiuze pamba chini ya shilingi 1000, limeni alizeti mwaka ujao nitawatafutieni soko la alizeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, angalieni maisha ya Wananchi wa Kanda ya Ziwa, mmetusahau. Nimezungumzia kuna migodi saba, Tarime, Geita, Kahama, migodi hiyo ipo mpaka Shinyanga kuna almasi. Migodi saba ambayo naifahamu lakini jaribuni kuangalia maisha ya wananchi. Angalia hata kwenye Uchaguzi, CCM imepata kura nydingi sana Kanda ya Ziwa, lakini angalieni maisha ya Wananchi wa Kanda ya Ziwa mmetusahau. Tunaiomba Serikali ijaribu kutuangalia, ardhi yetu imetobolewa na hawa wawekezaji na maisha yetu ni mabovu. Leo Kanda ya Ziwa inaleta uchumi mkubwa sana katika nchi, lakini ndiyo imekuwa ya nyuma. Mmetusahau hata kwenye uongozi, angalia Baraza la Mawaziri, Kanda ya Kaskazini, angalia hata kwenye Vyama vya Upinzani, Viongozi wake wa ngazi ya juu wanatoka Kaskazini. Kwa nini ina maana sisi Wasukuma hatuna elimu? Tumekuwa daraja la kupandiwa. Uchumi Kanda ya Ziwa; leo angalia zao la samaki, Kanda ya Ziwa tulikuwa na uchumi pamba na samaki, lakini vyote vimeporomoka kwa nini? Jaribuni kuiangalia Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, siungi mkono hoja mpaka mambo niliyoyataja ambayo yaliahidiwa mwaka jana yatakapotekelezwa. Siungi mkono hoja mpaka nitakapo jibowiwa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Haya ahsante, mpaka apatikane Mwenyekiti wa CHADEMA huko Musoma. Haya, mtakuwa mbali mno. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Antony Mbassa, atafuatiwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Riziki Omari Juma na Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Mheshimiwa Mbunge, nafasi ipo CHADEMA aje tu atapata Uongozi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye amenijalia afya njema ya kuwepo mahala hapa. Vile vile nawashukuru Wananchi wa Jimbo la Biharamulo Magharibi, ambao tumekuwa pamoja, wameshirikiana nami hususan katika kipindi chote ambacho nilikuwa nashughulikia kesi ya uchaguzi; ninawashukuru; Mwenyezi Mungu azidi kuwajalia na nimeshinda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia kwa kulaani kitendo cha kijambazi ambacho amefanyiwa Daktari Ulimboka, ambaye anatetea maslahi ya Madaktari wanaohudumia Wananchi wa Tanzania hii. Madaktari wanaofanya kazi katika mazingira magumu, ambao hawana vitendea kazi, posho duni, lakini kwa kulifanya hilo, ameonekana amekuwa mbuzi wa kafara; tunamwombea Mungu atamjalia kheri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Kagera tuna tatizo la wahamiaji haramu. Wahamiaji hawa haramu

sasa wamegeuza *Burigi Game Reserve* kama makao, wanasumbua sana wananchi, wamefuga kiholela kiasi kwamba sasa inaonekana Mkao wetu sasa umekuwa ni shamba la bibi ambalo halina mwenyewe. Inasikitisha sana watu hawa wanapokuja na kuwakuta wananchi, wazalendo, wakaonekana wazalendo hawana haki. Katika Jimbo langu la Biharamulo Magharibi imekuwa ni kero, mazingira yote yamevamiwa, watu hawa wanafuga kiholela na wanaharibu mazingira. Mimi nashindwa kuelewa Serikali yetu jamani inatusaidia vipi? Watu hawa wamekuwa na kiburi kweli, kila mahala wanaona ni eneo lao la kufanya mambo yao wanayoyataka. (*Makofi*)

Naomba Serikali tafadhali iliangalie hili kwa makini sana na ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, taarifa zetu nyingi tumezileta kama Wabunge wa Mkao wa Kagera uzifanyie kazi, tumechoshwa na vitendo hivi. Leo hii inaonekana mzawa ndani ya nchi yake hana haki ila mgeni ndiyo mwenye haki na mgeni ndiyo anathaminiwa zaidi kuliko mzawa; hii inatusikitisha sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ufgaji huu wa kiholela umeharibu sana *Burigi Game Reserve* kiasi kwamba hata wanyama wanatoka sasa kule porini kwenda kushambulia wananchi kwa sababu wamefukuzwa na hawa wafugaji haramu na tumesikitika kwa hili, kwa sababu kule kuna askari wa wanyamapori, wanafanya kazi ya kulinda wanyama wetu, lakini ajabu wanaruhusu hao wafugaji. Hivi ni sheria ipi

inayowaruhusu wafugie ndani ya *reserve*? Je, Serikali hailioni hili? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, matokeo yake, mifugo ile inapita mle na mbaya zaidi sasa imefika mahala hata hatua nyingine imebadilika, hata maaskari wetu wanadiriki kuwaangalia au kuchukua mifugo ya wafugaji wanaofugia karibu na *Nora Reserve* na kuifukuzia ndani ya *reserve* na matokeo yake wanaanza kuwatoza wale wenye ile mifugo pesa ambazo haziingii kwenye Mfuko wowote ule wa Serikali; inasikitisha sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ng'ombe wamekufa kule, watu wanatishiwa, ni maisha ya ajabu sana. Sasa huyu mwananchi tutamwendelezaje? Imeonekana mfugaji hana chake katika nchi hii. Ninaomba tafadhali Serikali iangalie kwa makini sana na pindi inapotokea suala la namna hiyo, tunapotoa malalamiko yetu mtusaidie.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana niliuliza swalii katika Bunge lako hili Tukufu na nikajibwa kwa ahadi ya matumaini mazuri. Wafugaji wangu wana tatizo kubwa la kukosa sehemu za kufugia. Nilimwomba Mheshimiwa Waziri afanye mchakato ndani ya Wizara yake, najua ni suala mtambuka lakini wananchi hawa wapewe eneo la kufugia, ahadi ikatolewa vizuri tu na kabla ya suala hilo kuna wafugaji walishakuja mpaka hapa Dodoma wakamwona Mheshimiwa Waziri na akawaahidi kulitatua lakini mpaka leo hii imekuwa ni ahadi ya kiini macho. Ninaomba Mheshimiwa Waziri utekeleze suala hilo.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge hili tumeshuhudia kodi ya vijana wetu wanaoendesha pikipiki imeondolewa na tukaridhika kabisa kwamba, kwa kuondoa kodi hii tumetengeneza nafasi za ajira lakini siyo kweli. Hawa wanaoendesha hizi pikipiki ni asilimia ngapi ya vijana walioko mtaani ambao hawana ajira? Hawa wachache wanaoendesha pikipiki wanasaidiaje kuinua kipato cha wenzao ambao hawana ajira?

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Bunge lako hili liliidhinisha Mpango wa kujengwa Vyuo vya VETA lakini ajabu mpaka leo hii hatuoni hivyo vyuo vimejengwa wapi. Ukisoma taarifa wanasema wamejenga kimoja. Suluhisho la ajira kwa vijana wetu ingekuwa ni kujenga vyuo ambavyo vitawasaidia wapate ufundi, leo hii tumewahalalishia waendeshe pikipiki lakini nani atakayetengeneza hizo pikipiki kama hatuanzishi Vyuo vya VETA na vya Ufundi?

Mheshimiwa Spika, tukubaliane kabisa kwamba, hapa sasa kuna haja ya msingi ya kuangalia hili kundi la vijana, tuwatafutie shughuli maalum itakayowawezesha kujajiri wao wenyewe na si vingine bali ni kuwa na vyuo vya VETA. Leo hii ukihesabu Vyuo vya VETA vilivyokuwepo ni vichache mno, vinachukua idadi ndogo sana ya wanafunzi. Vyuo vilivyokuwepo vya FDC leo hii vingine hata vimetelekezwa, vinachukua vijana kidogo sana. Tunaomba tafadhali Serikali iwaangalie vijana kwa upana na ukubwa ili waweze kupata ujuzi utakaowasaidia katika kujenga maisha yao ya baadaye. Kila siku tunaambiwa vijana Taifa la kesho, hapana, kujenga Taifa la kesho unaanza

leo hii, tuseme nguvu ya vijana sasa hivi ndiyo inayohitajika si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kuhusu Mabaraza ya Kata. Mabaraza haya ya Kata yamekuwepo lakini sina uhakika wala sina imani kama yamejengewa uwezo. Leo hii Mabaraza haya yanafanya kazi kadiri yanavyojua. Ukiangalia mapato yake yanapatikanaje au wanalipwaje hawa Wajumbe wa Baraza hili ni tabu tupu. Leo hii inafika mahala unajichukulia maamuzi ya kutoza faini au vifungu vingine vyaa sheria ambavyo havipo.

Mtu ameshtakiwa kwenye Baraza la Kata anaambiwa hana haki ya kujieleza. Sasa kama hana haki ya kujieleza kwa nini anapelekwa pale asipelekwe kwenye vyombo vinavyohusika? Baraza la Kata linamwambia wewe hupaswi kujieleza hapa; inasikitisha sana. Inafika mahala wanatoza adhabu, bado wanampangia yule kwamba uende kwa Mtendaji akakupangie kazi inayolingana na thamani ya shilingi fulani kama adhabu yako. Mimi nafikiri hatuwatendei haki wananchi. Ninaomba tafadhali Mabaraza ya Kata yajengewe uwezo, wafahamu misingi inayowafanya wao kuwepo pale, wajue wanatumia taratibu zippi katika kutoa suluhu mbalimbali na wao watambuliwe wapewe posho, vinginevyo ndiyo tunakokuta ukiritimba wa rushwa zisizokuwa na mwelekeo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bei ya mazao ya wakulima; inasikitisha sana wakati wakulima hawa wanapoanza kilimo, wanapewa maneno mazuri sana

ya ushawishi; walime, bei nzuri, lakini wakati wa kuuza ni tabu. Nimeshuhudia wakulima wa Zao la Tumbaku katika Kata zote zinazolima tumbaku Jimbo la Biharamulo Magharibi, kuna mgogoro na Afisa Ushirika, wameletewa pembejeo, bei hawaambiwi, mwisho wa siku wanaenda kudai pesa yao wanaambiwa wametumbukia, ndiyo neno wanadolitumia. Wao wanasomesha watoto, wana familia, wana mahitaji yao, unakuwa mgogoro. Hesabu zinakokotolewa siku nne, lakini jibu halitoki. Tafadhalii waambieni wakulima ukweli kwamba zao hili zamu hii bei haipo waelewe.

Mheshimiwa Spika, hakuna elfu, hakuna kilo ya pamba. Ahsante.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili leo ili na mimi niweze kuwawakilisha Wananchi wa Jimbo la Peramiho katika kuzungumza machache kwenye Hotuba hii ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwaomba Wabunge wote waunge mkono hoja ya Bajeti hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninasema hivyo kwa sababu nikianza hata na mse maji mwenzangu aliyekaa hivi punde, Mheshimiwa Dkt. Mbassa, ameeleza kero za wananchi katika Jimbo lake. Sisi Wabunge wote ni Madiwani katika Mabaraza ya Halmashauri kwenye maeneo yetu. Kwa hiyo, hakuna Bajeti ambayo ni msaada mkubwa kwetu kutatua kero za wananchi

kama hii, inayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, ambapo TAMISEMI pia ipo humo ndani. Kwa hiyo, ninawaomba Wabunge wenzangu, kutokuunga mkono Bajeti hii ni kushindwa kutekeleza Sera na Mipango ya Serikali kwenye Halmashauri zetu kupitia TAMISEMI na sisi tukiwa kama Madiwani ndani ya Halmashauri hizo na tunaona matatizo ya wananchi katika Halmashauri tunazoziongoza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Halmashauri yangu, ambayo ndiyo inayosimamia maendeleo ya Wananchi wa Jimbo la Peramiho, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote walioko katika Wizara yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea, ninampongeza kwa dhati kabisa Mkuu wetu wa Mkoa tuliyeteletewa, ameanza kazi kwa *speed* ya ajabu. Ametambua ni nini mahitaji ya Wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na amekuja na *spirit* ya kuturudisha kwenye Agizo la Mlale ambalo lilisimamia Siasa ya Kilimo na Ujenzi wa Nyumba Bora. Mheshimiwa Mwambungu, nakupongeza. Wabunge Wote wa Mkoa wa Ruvuma, tunakupa ahadi ya kushirikiana na wewe bega kwa bega na tutafanya kazi kwa maslahi ya wananchi wetu na kwa kuwa wewe ni Kiongozi Bora, tunaamini utatuendeleza zaidi katika Mkoa wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza *DCs* wetu. Karibu Mkoa mzima tumepatiwa *DCs* wapya, tutakuwa nao bega kwa bega. Nimwombe Mkuu wangu wa Wilaya, aamini kabisa kwamba, mimi na Dokta

Nchimbi, Wabunge wake katika Wilaya yake ya Songea, tutafanya nae kazi kwa maslahi ya Wananchi wa Wilaya ya Songea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi niingie kwenye kupongeza zaidi na hasa ari yangu ya kuunga mkono Bajeti hii. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninakushukuru sana kwa kupokea kilio cha Madiwani na kuwaongezea posho. Ninaomba Ofisi yako iende mbele zaidi kuhakikisha Madiwani hawapati shida ya mikopo ya vyombo vya usafiri na mambo mengine wanayoyahitaji ili waweze kutusimamia shughuli zetu vizuri. Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, hilo ulilolifanya ni jema na ninaamini Mawaziri katika Ofisi yako, watatusaidia sana kuyasimamia hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali yangu kwa kukubali Hospitali ya Peramiho kuingia kwenye Mpango wa *DDH*. Tumeungana na Serikali, Hospitali ya Peramiho sasa ni Hospitali ya Rufaa kwenye Mkoa wetu. Ninamwomba sana Waziri wa Afya, toka Hopsitali hiyo imepanda hadhi hatujapata Madaktari. Kwa hiyo, ninaomba sana katika Bajeti ya Wizara ya Afya, nipate majibu ni Madaktari wangapi wataletwa kwenye Hospitali ya Peramiho. Ninashukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Ofisi yako imepokea ombi la Mji Mdogo wa Madaba; Kijiji cha Madaba, kupanda hadhi sasa kuwa Mji Mdogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaamini kabla mwaka huu haujaisha, Gazeti la Serikali litatangaza Madaba kuwa Mji Mdogo. Namshukuru sana Waziri aliyepita, Mheshimiwa George Mkuchika, alitoa ushirikiano wa

kutosha sana kwenye Halmashauri yetu. Ninaamini kabisa, dada yangu Mheshimiwa Hawa Ghasia na yeye ataongeza nguvu kuhakikisha Madaba sasa inakuwa Mji Mdogo. Dada Hawa Ghasia, Waziri wetu, ninakutakia kila la heri ufanikishe hili, hitaji kubwa sana la Wananchi wa Madaba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pale Madaba bado tuna hoja ya ujenzi wa chumba cha upasuaji kwenye Kituo cha Afya. Dada Hawa Ghasia, utakuta faili letu kwenye Ofisi yako, ninaomba pia tushirikiane katika hilo.

Mheshimiwa Spika, haya ninayoyasema, yananipa moyo kuunga mkono Bajeti hii kwa sababu ni hivi juzi tu Mheshimiwa Magufuli ametuletea Halmashauri yetu shilingi milioni 500 na kitu kutekeleza Mradi Mkubwa wa Barabara mbili. Barabara moja ikitoka Kijiji cha Matimila kwenda Mkongotema, nikiungana na ndugu yangu Mheshimiwa Vita Kawawa. Barabara nyingine tuliyopata *favour* ni kutoka Ndongosi kwenda Nambendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, barabara hizo hazijawahi kupitiwa na greda toka zimeanza, toka Uhuru umepatikana. Hivi leo nikisimama hapa nikasema siungi mkono hoja hii, hata wale wananchi watanishangaa. Kwa hiyo, naomba niseme naunga mkono hoja hii. Namshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Magufuli na naishukuru Serikali yangu. Bado tunasubiri ujenzi wa barabara kutoka Likuyufusi kwenda Mkenda, Serikali imeshatoa fedha barabara ile imeshafanyiwa upembuzi yakinifu, inatuunganisha na mpaka wa

Tanzania na Msumbiji. Ninadhani tupo kwenye mazungumzo mazuri, Serikali itapanga bajeti kuendeleza Daraja la Mwekulu na kuendeleza kiporo cha barabara kinachounganisha Jimbo lako na Jimbo langu na wewe unaufahamu Mradi wetu huo. Basi nimwombe Mheshimiwa Hawa Ghasia, afungue mafaili aone ule Mradi wetu atusaidie uweze kukamilika na unazidi kuendelea kwa faida ya wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nikiingia kwenye killimo, suala la mbolea; ninaomba niiambie Serikali, tafadhalii sana tusirudie makosa tuliyoyafanya mwaka jana. Mbolea ilichelewa, mbegu zilichelewa, uzalishaji wa chakula unategemea Mikoa ya Kusini kwa nchi nzima ya Tanzania, sasa lile lisijitokeze, lakini tulipata tatizo kubwa sana la soko. Ninamwomba sana Waziri wa Kilimo na Wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na hasa Jimbo la Peramiho, safari hii utaratibu wa soko la mahindi usiwe na matatizo tena. Ajenda hii ni muhimu. Mhimili mkubwa wa uchumi wa Wananchi wa Jimbo la Peramiho na Mkoa wa Ruvuma, upo kwenye mazao ya chakula na hasa mahindi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba niungane na Mheshimiwa Devotha Likokola, jana aliomba tujengewe soko. Mheshimiwa Mary Nagu anakumbuka, mama wa uwekezaji, Mheshimiwa Waziri wangu; nimekuomba sana soko mpakani mwa Tanzania na Msumbiji, hebu wekeza pale uwasaidie Wananchi wa Jimbo la Peramiho na Mkoa wa Ruvuma, kuongeza uchumi wao kupitia soko la mahindi, ndiyo zao tunalolitegemea. Mheshimiwa Mary Nagu, ninaamini kabisa Waziri wangu, sasa twende

kwenye ule mkakati ambao toka ukiwa enzi za Wizara ile mpaka sasa bado haujafanyiwa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Serikali kwa kutenga fedha kwa umeme wa gridi kutoka Makambako mpaka Songea. Nina haja ya kuishukuru Serikali, umeme utapita Igawisenga, Wino, Lilondo, Madaba, Gumbilo na Mchangimbole. Sasa ni kwa nini nisiunge mkono Bajeti hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia pale Lilondo, mimi na wananchi wangu, tumeshaanza kutengeneza umeme kwenye maporomoko. Tuna uwezo wa kuuza umeme huo kwenye Gridi ya Taifa, lakini naiomba Serikali ipeleke umeme kwenye taasisi zilizoko pale Peramiho, Mlale JKT na katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kuzungumzia suala la ajira kwa vijana. Tatizo la ajira kwa vijana ni kubwa sana. Mimi nilikuwa ninafikiri mambo haya nitakayosema yafanyike, Serikali ianze kuangalia jinsi ya kuwekeza katika miundombinu. Kuna nchi zimefanikiwa kwenye ajira kwa sababu ya kuwekeza kwenye miundombinu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja hii kwa maslahi ya Wananchi wa Jimbo la Peramiho. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Umesahau kwamba na kwangu unapita Kifanya pia. Unapita Kifanya kule kwangu.

Sasa namwita Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir, Mheshimiwa Zaynab Vullu ajiandae, Mheshimiwa Mbaruk Salim ajiandae na Mheshimiwa Pindi Hazara Chana ajiandae.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa, napenda kutoa pongozi zangu kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Waziri Mkuu Mizengo Kayanza Peter Pinda na wewe pia Mheshimiwa Spika, kwa kujali masuala ya watu wenye ulemavu, mnajali na mnafuatilia. Nawapongezeni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia masuala ya watu wenye ulemavu kuondoka kwenye Wizara ya Afya na wahamishiwe kwenye Wizara ya Waziri Mkuu. Ombi hilo tumeliomba sana, siyo peke yangu ninazungumza leo, lakini limeshazungumzwa sana. Kwa hiyo, leo naomba kutilia msisitizo na kuiomba Serikali iangalie masuala ya watu wenye ulemavu kwenye Wizara ya Afya, yahamishiwe Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa sababu pale kwa Waziri Mkuu kuna Kitengo Maalum kinashughulikia masuala hayo. Kwa hiyo, tunaomba tuwepo pale, ombi hili nalileta tena na nimeshawahi kuomba, lakini naomba kurudia tena leo kwamba, tunaomba masuala ya watu wenye ulemavu yaje kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, naomba kuzungumzia masuala ya viziwi. Kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Ibara ya 18, inazungumzia haki ya kupata habari za jamii. Viziwi haki hiyo hawaipati

wananyanyasika. Kunatoka taarifa kwenye vyombo vya habari, wao habari hawapati, hawajui chochote kinachozungumzwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ombi langu, kwenye Vyombo vya *Television*, kuwepo na watu wa lugha ya alama ili na wao wapate taarifa kinachoendelea. Sasa hivi Bunge linaendelea, hakuna wanachokijua, hawaelewi kinafanyika nini humu ndani. Hawajui kitu gani kinazungumzwa humu ndani kwa sababu ile haki hawaipati. Wananyanyasika kwenye nchi yao wenyewe kama wageni, kumbe wao ni raia wa nchi hii. Wapewe haki hiyo na wao wapate kusikia na kuelewa kitu gani kinaendelea ndani ya Bunge, kitu gani kinachoendelea kwenye masuala yote mengi. Kunakuja sasa hivi Tume ya Katiba, itapita kuzunguka na wao wapate haki ya kutoa maoni yao. Hilo naomba lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu kumekuwa hakuna chuo cha kujifunzia lugha ya alama. Natoa ombi kwa Serikali, kuna Chuo cha Patandi kinaweza kikageuzwa yakapelekwa mafunzo ya lugha ya alama yakaenda kwenye Chuo hicho. Naiomba ombi langu hilo lisikillizwe na wao watendewe haki, wapate haki ya kupata habari katika jamii wajue kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, naomba kuingia kwenye suala la Baraza la Ushauri kwa watu wenyewe ulemavu. Sheria ilipopitishwa ya watu wenyewe ulemavu kuna Baraza tumeambiwa litaundwa; swali langu je, Baraza hili litaundwa lini?

Mheshimiwa Spika, naomba kupata jibu kwenye swalii hilo kwamba, hili Baraza litaundwa maana naona siku zinazidi kwenda. Sheria imeshapita; je, ni lini Baraza hilo litaundwa kwa ajili ya kushughulikia masuala ya watu wenye ulemavu?

Mheshimiwa Spika, lingine ninalopenda kuongelea ni kuhusu miundombinu. Miundombinu kwa watu wenye ulemavu ni tatizo kubwa sana. Wanapofika kwenye majengo, watu wenye ulemavu wa viungo wanapata matatizo, haki hawana. Unakuta jengo, haliko rafiki kwa mtu mwenye ulemavu wa viungo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina mfano mzuri kwenye majengo yanayojengwa sasa hivi na *National Housing*. Majengo mengi yanayojengwa sasa hivi siyo rafiki kwa watu wenye ulemavu wa viungo. Nina mfano mzuri; juzi nimepata mgeni nyumbani ana ulemavu; ilibidi kumbeba kumuweka kwenye *lift*, angalau pana *lift*, pia ilibidi kumbeba hakuweza kumudu mwenyewe. Hakukuwa na lile eneo la kupita kwa ile *Wheel Chair* yake, kwa hiyo, hiyo siyo haki.

Mheshimiwa Spika, ninaomba suala hili, ninarudia tena kulisema na nimeshasema sana na nitaendelea kusema sitachoka. Narudia kuzungumza na Wizara husika wanansikia; majengo yanayojengwa yawekewe miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu. Kwa sababu watu wenye ulemavu wanapigia kelele matatizo yao kila siku, lakini

hayafanyiwi kazi; kuna tatizo gani? Wamekosa nini watu wenyewe ulemavu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hali ya uchumi ni ngumu, maisha ni magumu, lakini watu wenyewe ulemavu ugumu huu unakuwa mara mbili zaidi au mara tatu zaidi kwao. Basi tuangalie hata yanayowezekana yafanyike. Ninarudia kusema haya yanayowezekana yafanyike.

Mheshimiwa Spika, hapo hapo kwenye miundombinu, ninaingia kwenye alama za barabarani; suala la alama za barabarani nimeshazungumza 2010, wakati ule Waziri wa Miundombinu akiwa Mheshimiwa Kawambwa. Nilimkabidhi Mheshimiwa Spika, kitabu kama hiki.

Mheshimiwa Spika, nilimpa Mheshimiwa Kawambwa, kitabu hiki chenye alama za barabarani kwa ajili ya watu wenyewe ulemavu. Suala hili limeshindikana, kuna taasisi inaitwa Kamati ya Usalama Barabarani kwa Watu Wenyewe Ulemavu, kuna Mwenyekiti pale anaitwa Bwana Kabatele, hodari sana huyo bwana; ameshughulika amepata mabango, mabango yanaota vumbi yako karibu sabini na kitu, yamewekwa ndani uwezekano wa kuwekwa umeshindikana mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam analijua hili. Walikwenda kwake kumwomba yale mabango yawekwe, kibali kimetoka Manispaa ya Kinondoni na Manispaa ya Temeke yale mabango yawekwe kusaidia mlemavu wa viungo akipita kuwe na tahadhari kwamba, hapa jamani anapita mlemavu

wa viungo, hapa anapita mwenye ulemavu wa ngozi, ana uoni hafifu haoni, kwa hiyo, aonekane anapovuka barabara. Kuna viziwi hawasikii sauti yoyote, anapovuka barabara aonekane.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Waziri Mkuu, hili suala lifanyiwe kazi. Barua ilikuja kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuomba suala hili litiliwe maanani. Kiki kitabu ninacho, naweza nikamkabidhi Mheshimiwa Waziri Mkuu akione na alama hizo zipo azione.

Mheshimiwa Spika, naomba kuingia sasa kwenye suala la mauaji ya walemovu wa ngozi (*albino*). Mauaji yanaendelea, juzi ameuwawa *albino* Arumeru, Arusha. Amekatwa mikono, amenyofolewa sehemu za siri, ametolewa koromeo, haya mauwaji yataisha lini katika nchi hii?

Mheshimiwa Spika, viungo vinachukuliwa vinaenda kuuzwa, hawa wanaochukua viungo hawajulikani? Ina maana imeshindikana kuwajua watu wanaotumia viungo? Mbona faru ameuwawa juzi, sijui anaitwa George, wauwaji wameshakamatwa tayari? Kumetokea mauwaji juzi kwenye utalii huko, wauwaji wameshakamatwa. Inashindikana nini kwenye mauwaji ya walemovu wa ngozi? Idadi imekuwa kubwa, wanakimbilia themanini na kitu, wanazidi kufa, kutishika na kukatwa mikono. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tatizo hili limekuwa kubwa. Katika watetezi Mheshimiwa Spika na wewe umo, tutetee. Ulikuja Lindi tukashereheke pamoja sherehe. Natamani hata kulia, najisikia kulia kwa sababu

wanauwawa, wanakatwa mikono, wananyofolewa sehemu za siri; tumekosa nini katika nchi hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumekosa nini? Naumia rohoni mwangu. Siungi mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika hoja iliyopo mbele yetu. Nianze na kulizungumzia Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Bunge lina shughuli maalum na mahususi na ni Mhimili ambao unajitegemea, lakini Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Chombo cha Serikali. Kimekuwa kikitumika muda wote kwa ajili ya kuihudumia Serikali na kufanya kazi za Serikali. Wabunge hawapati fursa ya kuwasilisha maoni na hoja mbalimbali za wananchi.

Mheshimiwa Spika, natolea mfano, nina hoja ambayo nimeiwasilisha katika Ofisi ya Spika toka mwezi Novemba, ambayo inagusa maslahi na matatizo ya wananchi, lakini kila siku Huduma za Serikali, Shughuli za Serikali na Hoja za Serikali, zimepewa kipaumbele kuliko matatizo ya wananchi. Vivyo hivyo, hata inapofikia masuala ya kujadili Taarifa za Kamati za Bunge nazo zinanyimwa muda, zinapewa muda mdogo; Kamati tatu kwa siku moja, jambo ambalo linatunyima uhuru wa kujadili masuala yanayowahusu wananchi. Jambo hili linasikitisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ilikuwa ni suala la ardhi. Mmesikia wenyewe, kila Mbunge aliyesimama

hana amezungumzia matatizo yanayogusa ardhi. Ninayo CD hapa ya matokeo yaliyotokana na kuzembea kutokuisikiliza hoja yangu, nitaiwasilisha kwenye Meza yako.

Mheshimiwa Spika, natoka kwenye Bunge, nakuja kwenye Bajeti. Tutengeneze sasa Bajeti ambazo zinatекеlezeka. Tusiwape wananchi matumaini ya tarakimu wakati bajeti hazitekelezeki. Nitatoa mfano, Halmashauri yangu ya Mji wa Mpanda katika Bajeti iliyopita ya Maendeleo, tulikuwa tumetengewa na kudhinishiwa na Bunge lako Tukufu shilingi bilioni 4.42, lakini mpaka mwisho wa mwaka tumepokea shilingi bilioni 1.78, sawa na asilimia 43 tu. Wananchi walikuwa na matarajio makubwa sana kutokana na bajeti iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge lakini Serikali haitezemshi fedha kwenye Halmashauri zetu ili Miradi iweze kutekelezeka. Maeneo mengine hatukupata fedha kabisa. (*Makofii*)

Nyumba za watumishi hatukupata fedha, Mpango wa Maendeleo ya Elimu za Sekondari ambao tulikuwa tumeidhinishwa shilingi 6,014 milioni hatukupata lakini kwenye taarifa ya majedwali yaliyoambatanishwa kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu, inasema kwamba, kuna madawati 1200 yametengenezwa yenye thamani ya shilingi milioni 97, kitu ambacho nina mashaka nacho na sina uhakika nacho kwa sababu nafahamu hakuna fedha iliyolekwa katika Halmashauri yetu lakini kwenye taarifa inaonekana kwamba kuna madawati yametengenezwa. Kwa hiyo, nitahitaji kupata maelezo katika hilo.

Mheshimiwa Spika, juu ya Bajeti, tulikuwa tumetengewa bilioni moja na milioni mia tatu kwa ajili ya Miradi ya Maji. Mpaka mwisho wa mwaka tumepata milioni 422 ambayo ni sawasawa na asilimia kama 33 hivi. Tatizo la maji katika Mji wa Mpanda litaendelea kuwepo, tumeshindwa kukamilisha tenki la maji, niombe sasa Serikali, fedha ambazo zimeidhinishwa na Bunge zipelekwe ili wananchi waweze kupata maendeleo yaliyokuwa yamekusudiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mpanda tunalima tumbaku, wakulima wa tumbaku wanalipwa wanauzwa tumbaku yao kwa dola, wanalipwa kwa Shilingi za Kitanzania, kama waliuza kwa dola walipe kwa dola. Nilipata malalamiko, siku ambayo mkulima amekuja kulalamika kwangu dola ilikuwa shilingi 733 na yeye analipwa shilingi 1,400 na Chama cha Msingi; huu wizi muuangalie, wakulima wa tumbaku walipwe fedha kutokana na bei ambayo wameuza kwenye masoko. Zaidi ya hapo, nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, mwaka 2010 wakati anafungua Soko la Tumbaku pale Majalila na mimi nikiwepo, aliwaahidi wakulima kuwatafutia soko Nchini China, wakulima wameongeza kilimo cha Zao la Tumbaku lisituleteee tena mgogoro kama msimu uliopita.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo ni kwamba, Ushirika ni hiari, kwa hiyo, wananchi wanapokuwa wameungana wakaamua kuanzisha Ushirika wao waruhusiwe wasiweke urasimu na vikwazo. (*Makofii*)

Chama cha Msingi cha Wakulima wa Tumbaku cha Mpanda Kati ni kikubwa na ni lazima kigawanywe na jitihada za kutaka kukigawa Chama hiki kila zinapofanyika wananchi ambao wanataka kujenga Ushirika wanazuiliwa.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la Mkurugenzi wa Mji wa Mpanda, ambaye aliwahi kuwa Afisa Utumishi pale, akawa Kaimu Mkurugenzi wa Mji, sasa amethibitishwa kuwa Mkurugenzi, namtakia kila la heri na baraka na mafanikio katika kazi yake mpya. Alipewa uhamisho kwenda lleje kama Afisa Utumishi akazuiliwa na TAMISEMI asiondoke, amethibitishwa kuwa Mkurugenzi amepelekwa Ngala amezuiliwa tena asiondoke Mpanda tatizo ni nini? Je, analinda maslahi ya nani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo kubwa juu ya pensheni za walimu, wengi hawapati pensheni zao kwa wakati, aidha wapo ambao wamefariki pensheni zinakuja na wapo ambao wako hai na hawapati pensheni zao. Jambo hili naomba liangaliwe ni namna gani wanaweza kulisimamia hilo. Nilipata bahati ya kutembelea shule za msingi zilizopo katika Jimbo langu, kuna tatizo kubwa la uhaba wa vyumba vyatatu na madarasa na madawati, watoto wengi wanakaa chini na si Mpanda tu pake yake limekuwa ni tatizo la nchi nzima, watoto wengi wanakaa chini kutokana na uhaba wa madawati. Kibaya zaidi, hakuna mkakati wa makusudi ambao umewekwa na Serikali kwa ajili ya kuliondoa hili tatizo na kuhakikisha kwamba watoto wetu wanapata elimu katika mazingira mazuri, salama na safi. Niombe nijue mkakati wa Serikali katika

kukabiliana na tatizo la uhaba wa vyumba vyatayi na madarasa na madawati hususan katika shule za msingi.

Mheshimiwa Spika, nirejee Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa 37, inayohusu umeme kwamba, Wakala wa Umeme Vijiji ni umetekeleza Programu Kabambe katika mikoa kadhaa ikiwemo Mkoa wa Rukwa. Rukwa tuna tatizo kubwa sana la umeme achilia mbali vijiji, ambapo mimi sikubaliani na taarifa hii, kwa sababu siamini kama kuna mpango wowote wa kufikisha umeme katika kijiji chochote katika Mkoa wa Rukwa na Katavi. Iwapo katika Makao Makuu yenye ya Wilaya za Mikoa ya Rukwa na Katavi umeme ni tatizo, Mpanda umeme ni tatizo, Sumbawanga ni tatizo, Nkasi hawana kabisa, kwa hiyo, ninaposoma kwamba kuna mpango wa kupeleka umeme vijiji, taarifa hii inanitia mashaka na sina uhakika kama Mheshimiwa Waziri aliisoma na kwa sababu na yeye anatoka Rukwa, ana uhakika ni kijiji gani ambacho kimepelekewa umeme. Nadhani atakapohitimisha ataniambia ndugu yangu Arfi, tulishapeleka umeme katika vijiji kadhaa.

Pia nizungumzie suala la barabara za kuunganisha Mpanda, wamesema wenzangu waliotangulia kwamba, Mkoa wa Rukwa na Katavi tunazalisha mazao ya kutosha hasa mahindi na tunapeleka katika mikoa ambayo inakuwa na upungufu wa chakula. Barabara za Mpanda - Tabora na Mpanda - Kigoma, zipewe kipaumbele kuhakikisha zinapitika wakati wote na zijengwe kwa kiwango cha lami kama itawezekana.

Mwisho kabisa, kama sitazungumzia reli nitakuwa sijakamilisha mchango wangu. Reli nayo tuitazame hususan Reli ya Mpanda. Hivi sasa tukienda Mpanda, tuondokane na zile fikra za zamani kwamba, Reli ya Mpanda ilikuwa ni kwa ajili ya kutoa huduma tu, Reli ya Mpanda ipo kwa ajili ya biashara. Kuna biashara kubwa ambayo ipo Mpanda, Shirika la Reli limeshindwa kui-tape hiyo biashara ya kuhamisha na kusafirisha mizigo. Kuna shehena kubwa ya mahindi na tumbaku inangojea kusafirishwa kutoka Mpanda. Nakushukuru. (*Makofi*)

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kusema naunga mkono hoja hii na ninazo sababu za msingi.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa Hotuba nzuri, lakini pia namshukuru kwa uteuzi wa Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Kanali Mstaafu Fabian Massawe, ambaye sisi kule kwetu Kagera tumemwongezea jina anaitwa Kanali Mstaafu Fabian Massawe Mlokozi. (*Makofi*)

Mlokozi kule kwetu maana yake ni mkombozi. Kanali Massawe alitokea Wilaya ya Karagwe kabla hajapandishwa kuwa Mkuu wa Mkoa, kwa hiyo, namfahamu vizuri sana. Kusema kweli Mkoa wa Kagera tumebahatika, kama ni karata tunasema tumelamba dume. Tunamhakikishia ukishirikano wa hali ya juu sana na sisi wote Wabunge wa Kagera tumejipanga kuhakikisha kwamba tunamsahidia kadiri ya uwezo wetu kuendeleza mkoa wetu.

Mheshimiwa Spika, nianze na riba za mabenki; ili wananchi wetu waweze kuendelea ni lazima wachangie katika uchumi wa nchi hii kwa kukopa lakini riba za mabenki ziko juu sana. Naomba Serikali iwaangalie wananchi, wanaogopa benki kama kituo cha polisi.

Mheshimiwa Spika, ningetamani sana nione Tawi la Benki ya Kilimo Kayanga katika Makao Makuu ya Wilaya ya Karagwe kwa sababu hakuna Mwananchi wa Karagwe ambaye anaweza kwenda Dar es Salaam akapata mkopo katika benki hii. Vilevile Benki hii iende kwenye wilaya zote ili wananchi wetu waweze kufaidika kwa maana wakulima wako vijijini hawako Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine, Serikali imekuwa na utaratibu wa kutumia fedha za Serikali kupitia Benki moja hapa nchini, ambayo ni Benki ya *NMB*, fedha zote za Serikali zinapitia Akaunti ya *NMB*. Fedha hizi zinakaa kwenye benki bila kutoa riba hata senti tano na kawaida ya fedha ni kwamba, fedha zinachakaa. Sasa juzi hapa Serikali ilitoa zabuni ikatangaza mabenki yashindane kwa ajili ya kutoa huduma katika Akaunti za Serikali. Jambo zuri sana, nilibahatika kuiona zabuni hii, kigezo kimojawapo ni kwamba kila benki ambayo inashindana katika hili ni lazima iwe na tawi katika wilaya zote.

Ukiangalia Benki ambayo ina Matawi katika Wilaya karibu zote ni Benki ya *NMB*. Sasa kigezo hiki kimeondolea ushindani Benki kama *Barclays*, *CRDB*,

*Akiba Commercial Bank* na Mabenki mengine. Kwa maana hiyo basi ni kwamba, tangazo ni kama lililenga kuipatia nafasi Benki moja tu.

Kwa hiyo, naishauri Serikali zabuni hii isiwe ya kibaguzi. Naiomba Serikali iangalie na Mheshimiwa Waziri Mkuu naamini kabisa utaliangalia kwa makini hili; tufute zabuni hii ili kigezo hiki kiondoke na Benki zetu zishindane. Pia nilikuwa napendekeza fedha za Serikali ziwekwe katika Mabenki, kwa mfano, *TANROADS*, wao fedha zao wanaweka katika Benki na wanatengeneza *interest* wanapata faida kwa maana kwamba, fedha ya Serikali isikae kabla hajatumika, unaweza ukatengeneza faida ndani ya siku tatu, saba, ni masuala ya makubaliano.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi hasa za Halmashauri za Wilaya zikiwekwa katika akaunti fulani ambazo zinatoa *interest* kabla hazijatumika na kabla kandarasi hazifanyika, zitasaidia ku-generate *profit*, yaani faida ambayo itasaidia sana matatizo mengi ambayo tunapata katika Halmashauri zetu za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kuunga mkono hoja kwa sababu nimefarijika na kazi ya inayofanywa na Serikali hasa kupeleka umeme vijijini. Kule kwangu Jimbo la Karagwe, Serikali imesikia kilio changu cha muda mrefu wanaanza kupeleka umeme katika Tarafa ya Nyaishozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, angalizo langu katika Mradi huu na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ningeomba anisikilize kwa sababu nipo kwenye eneo

lake ni kwamba, Mradi huu wa Umeme umeruka baadhi ya vijiji. Kuna Kijiji kinaitwa Lukale, wamekiruka hawakupeleka hata nguvu. Pia wameruka Kijiji cha Misha, Kijiji cha Ruhita, Kijiji cha Rubare, Kijiji cha Kibogoizi na Kijiji cha Omorusimbi. Sasa Mradi huu ndiyo ni mzuri lakini usiwe wa kibaguzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitao wakati wa kampeni mwaka 2010 katika Mji Mdogo wa Nyakaiga, Tarafa ya Nyabionza. Wananchi walimwomba Mradi wa Umeme na aliahidi na Mradi huu nilitegemea uwe umeanza katika kipindi cha mwaka uliopita. Kwa maana ya kupeleka Mradi wa Umeme katika Vijiji vya Kamagambo, Kiruruma, Nyakaiga, Chamchuzi, Chabuora, Bukangara, Akishaka na tarafa nzima ya Nyabionza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mradi huu ukianza Serikali iache ile tabia ya kuruka kijiji fulani na kwenda kingine. Mimi ningeomba waanzie Chamchuzi, kuna Kijiji kinaitwa Chamchuzi Serikali ianzie hapo, ianzie Kijiji kinachoitwa Kaiko na Kijiji cha Kanyomagana waende mpaka Kamagambo, Mkangala, yaani kwa maana kwamba unapojenga Mradi wa Umeme basi eneo lote ille liwake siyo wengine wabaki wanunu.

Kwa hiyo, naomba sana Tarafa ya Nyabionza. Katika bajeti hii sitaki kumtisha Mheshimiwa Waziri wa Nishati kwa sababu ni mgeni na ni mtani wangu, lakini nilikuwa namwomba ajikite vizuri katika eneo hili ahakikishe kwamba bajeti ijayo ili nimuunge mkono, vijiji vyangu vyote hivi vya Tarafa vya Nyabionza

viwepo kama ambavyo Serikali imekuwa ikiahidi tangu mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, tuna Mradi wa Umeme ambaoulianiza tangu mwaka 2006, lakini nguzo zimelala Ukanda wa Kituntu mpaka Rwambezi. Mwaka 2006 niliiomba Serikali ije iondoe nguzo hizo ipeleke sehemu nyingine ambapo zitaonekana zina umuhimu. Kwa Mkoa wetu wa Kagera, amezungumza Mheshimiwa Mbassa, tuna tatizo la wahamiaji wasio rasmi, mimi siwezi kuwaita haramu; tunaiomba sana Serikali ituhakikishie kwamba ifikapo tarehe 1 Mei, watakuwa wameondoka wao na mifugo yao. Naombba Serikali jambo hilo itueleze wakati Waziri Mkuu ana-*wind up* kwamba amefikia wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo la vitalu vyawafugaji, nimezungumza humu nadhani inaweza kuwakama mara ya 20 kwa maana ya Kata ya Kihanga, Vitalu vyawafugaji vya Ranchi ya NARCO viligawiwa kwa wafugaji; sina tatizo nao, lakini kuna Kampuni moja ya Kagera Sugar ilipewa hekta karibu 45,000 lakini na vijiji vyangu sita vya Kishoju, Kihanga, Katanda, Kibwera, Mlamba na Bishabaigulu, ninaambiwa kwamba navyo vimepewa hekta 2000 wakati mtummoja wa Kagera Sugar amepewa hekta 45,000.

Naiomba Serikali iangalie uwezekano wa harakasana kutenga hekta zisizopungua 20,000 kwa ajili ya vijiji hivi sita ili wananchi wangu waweze kufaidika.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera tunahitaji Chuo cha VETA, hakuna Chuo cha VETA, tunakiomba kwa ajili ya vijana wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi Kagera ni wakulima wa kahawa, tunategemea kahawa, bei ya kahawa inasuasua, ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe bei elekezi isimamie kuanzia shilingi 1000 na kuendelea isiwe inashuka. Hatuwezi kukubali leo wanunuzi wanakuja na bei ya kwanza shilingi 1500 mwisho wanashuka mpaka shilingi 700. Kwa hiyo, nitafurahi sana wananchi wangu wakijua kwamba bei hasa ambayo ni ya kununulia kahawa ni shilingi 1500 na kuendelea siyo wale walangazi wanakuja kutuibia.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa sana, naunga mkono hoja kama nilivyosema. (*Makofi*)

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema na kusimama katika Bunge letu Tukufu kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nianze na Mabaraza ya Watoto; Mabaraza ya Watoto ni sehemu moja ambayo ina changamoto kubwa na ina watoto wenye vipaji sana na upeo mzuri wa kutoa hoja na hata ukiwauliza maswali wanavyojibu utafikiria labda huyu mtoto ameshakuwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, watoto wanavyotetea haki zao hutodhani kwamba hawa ni watoto wa umri midogo; wanajenga hoja vizuri, wanatoa ushahidi mzuri

mahakamani na inafika wakati hata wazazi wengine wenye roho za kikatilii wanaowakatili watoto wao wa kuwazaa wanafungwa kwa ushahidi wa watoto na usimamizi mzuri wa watoto. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kupitia Wizara hii ya TAMISEMI, itenye fedha hizi kwa ajili ya Mabaraza ya Watoto. Mimi ni shahidi niliyepita kuwaangalia watoto na hata Waziri wa Fedha wa hivi sasa alikuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo, naye namwomba asimamie hili kwa sababu ni Waziri wa Fedha. Kuzisimamia Halmashauri kutenga fedha kwa ajili ya kuwawezesha watoto, watoto wana vipaji vizuri, tutapata viongozi wazuri sana wa baadaye.

Hata Wabunge wakija kugombea watakuwa wazuri, nadhani tukianza kule ni sawasawa timu za mpira tukianza kuwaanzisha watoto wadogo tutapata timu nzuri. Basi Serikali ikiwekeza kule kwa watoto nadhani tutakuwa na Viongozi wazuri. Naiomba sana Serikali iangalie Mabaraza ya Watoto ni mazuri kwa kweli. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lingine nije katika Hotuba ya Waziri wa Nchi, TAMISEMI, ukurasa wa 12 kuhusu Muungano; Muungano ni Chombo muhimu sana na kwa kweli watu wengine wanatafsiri labda Wazanzibari hatuupendi.

Mheshimiwa Spika, lakini kinachopelekea tuonekane hatuupendi Muungano ni kero za Muungano kwamba hazitatuliwi. Haya siyasemi mimi tu, nimesoma gazeti la Zanzibar Leo, wapo baadhi ya

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, hotuba zao zimesema kwamba sisi tunaupenda Muungano, lakini kinachotupelekea liwe ni jambo ambalo linaonekana hatuupendi, ni kero za Muungano kwamba, zinachukua muda hazitatuliwi.

Leo ukiangalia Mheshimiwa Waziri ameorodhesha kero 13 halafu anaeeleza kwamba zilizopatiwa ufumbuzi ni kero mbili, kKatika hizo mbili ikiwemo mfuko wa Jimbo. Mfuko wa Jimbo kweli ni kero ya Muungano? Mimi naona hii bado hatujawa *serious* katika kutatua kero za Muungano, na hili ndilo linalopelekea matatizo yanayotukuta Zanzibar. Lakini kama kweli Serikali zetu mbili zitakaa kwa dhati kabisa na kujadili mambo ya kero za Muungano na kuonyesha umahiri wa kutatua kero za Muungano, nadhani wananchi wengi tutaupenda Muungano.

Kwa hiyo, naziomba Serikali zote mbili zikae ziharakishe kutatua kero za Muungano na pia ningemwomba Waziri kwa sababu leo kaeleza kero mbili tu, hebu hizo kero 11 zilizobaki akija hapa akifanya majumuisho atuainishie ni kero gani zilizokuwa hazijatatuliwa? Mimi nadhani hizo ndiyo zitakuwa kero hasa za Wazanzibar kuliko hizo zilizotatuliwa.

Mheshimiwa Spika, nije kidogo katika suala la mgomo wa Madaktari, lakini siingilii hili lililopo Mahakamani. Naomba nieleze kabisa, nataka kutoa rai tu, lakini kwanza ni-*declare interest* kwamba ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii. Nadhani tulipoleta maelezo yetu au taarifa yetu, wewe ulikuwa ni shahidi na mimi niliichangia hii kwamba Serikali

imefika wakati sasa ijenje hospitali kubwa ya kijeshi kwa sababu tumeshaona kwamba majeshi ni chombo kimoja ambacho kinafanya kazi kwa nidhamu kubwa sana na ninadhani hata tulipowahoji hawa Wanajeshi tukawaambia kwa ninyi hamfanyi mgomo kwenye hospitali? Wakasema hili jambo kwetu ni mwiko na wao hawafanyi kazi kwa kulipwa kulingana na mishahara ya vyeo vya kidaktari, bali wao wanakwenda kwa mishahara ya vyeo vya Kijeshi. Kwa hiyo, ni taabu sana kufanya mgomo katika chombo hiki cha majeshi.

Kwa hiyo, naiomba Serikali, umefika wakati sasa ione ipo haja kujengewa hospitali kubwa majeshi yetu na wanajeshi wasomeshwe vizuri ili tupate hospitali kubwa mbadala. Kama Muhimbili watagoma leo, tayari Serikali inasema watu wakatibiwe Lugalo, lakini Lugalo haiwezi kukidhi haya ya wananchi wote kama vile Muhimbili. Lakini itakapojengwa hospitali kubwa kama ya Muhimbili au zaidi ya Muhimbili, mimi nadhani itakidhi haja na matatizo ya migomo yataondoka.

Mheshimiwa Spika, nije katika ujenzi wa reli. Lazima tukubali kwamba sasa hivi Serikali ipo haja ya kuhimiza ujenzi wa reli. Wenzetu hapa Mawaziri wahimize suala hili kwa sababu barabara zetu kwa kweli zinakufa sana na ajali zinaongezeka kutokana na kufa kwa barabara kwa magari makubwa ya mizigo. Tayari Serikali inatuambia imetenga fedha za kutosha, hebu sasa tuwaombe Mawaziri walismamie hili. Mheshimiwa Mwakyembe tunakuamini, tunaomba ulisimamie hili.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wanapokuwa benchi, wenzetu kwa kweli ndiyo wachangiaji wazuri, wasemaji

wazuri, lakini tunaomba mnapokuwa huko sasa na ninyi muwe kwa kweli watekelezaji wazuri. Uzalendo tunataka utumike sana. Wenzetu muujali uzalendo ili mambo haya yatekelezwe. Hebu safari hii tuenze, wananchi watapiga kelele wapi? Nadhani kutakuwa hakuna kelele kubwa, reli hii inapigiwa kelele na kweli wanyonge watafaidika na uchumi utakua. Kwa kweli ipo haja reli yetu ijengwe.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, nizungumzie jambo moja ambalo kwa kweli nchi yetu hii inasikitishwa sana na inatuambia sana hapa kwamba iwapo itapewa masharti ya misaada kwamba labda tuingie katika ndoa ya jinsia moja; juzi Mheshimiwa Membe alisema hapa kwamba tutafunga mkanda kwa dhati kabisa, lakini misaada hiyo hatutaipokea. Sisi tunaipongeza Serikali kwa hilo. Lakini Serikali yetu kwa nini haipigi vita kwa vitendo ambavyo vinaashiria ushoga? Kwa mfano, *the Comedy*, wale madume mazima yanaji-*act* kama wanawake, wanarembua macho kwenye vyombo vyta televisheni kuliko mwanamke mwenyewe, kweli watu wale hawaashirii ushoga? Hawaitangazi nchi yetu kama kweli? Kwa sababu dume na dume lina-*act* mtu na mkewe. Hetu tuangalle kwani kitendo kama hiki naomba Serikali ipige vita na penye wanawake waweke wanawake, wapo wasanii wanawake.

Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.  
(*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Bahati Ali Abeid na Mheshimiwa Namelok Sokoine ajiandae.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii mchana huu wa leo na mimi kuwa mchangiaji wa hotuba hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia, naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

Mimi mchango wangu wa kwanza naanza ukurasa huu wa 28 kwenye kitabu hiki cha maelezo ya kiutendaji ambacho kimewasilishwa na Mheshimiwa Hawa Ghasia.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi Wazanzibar wamechangia fedha hizi za chenji ya Rada, lakini mimi nataka nizigusie kidogo fedha za chenji ya Rada kwamba, kama Rada yenyewe imenunuliwa kwa fedha ambazo zimetoka kwenye mfuko wa Muungano, basi namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuja kutoa majumuisho atuambie hii ni haki ya kuleta mchanganuo huu wa fedha hizi za chenji ya Rada kupelekwa katika sehemu moja ya Muungano na sehemu nyingine fedha hizi zisiende? Kama fedha hizi za ununuzi wa Rada hazikutoka kwenye mfuko huu wa fedha za Muungano, basi atueleze ili tuweze kuelewa. Ninavyomjua Mheshimiwa Waziri Mkuu, hana shida na hili atatueleza tu ili tuweze kufahamu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nichangie kwenye fedha ambazo ziliitwa mabilioni ya Kikwete, kwa Zanzibar fedha hizi zilitolewa na Mheshimiwa Rais wetu Jakaya M. Kikwete na Mheshimiwa Aman Karume kwa wakati ule na zilikuwa na madhumuni ya kukuza mitaji ya wafanyabiashara wadogo wadodo, wajasiriamali, na fedha hizi zilikuwa zinatolewa kwa njia ya mkopo, siwezi kusema kwamba fedha hizi hazikutolewa. Fedha hizi zilitolewa na zilitolewa kwa njia hiyo hiyo ya mkopo kwamba waliokopa warejeshe ili na wengine waweze kukopa.

Mheshimiwa Spika, lakini cha kusikitisha, fedha hizi uendelevu wake hauonekani. Kwa kuwa, Wabunge tuliokuwepo wakati ule tulimwomba sana Mheshimiwa Rais wetu Jakaya Kikwete fedha hizi ziende mpaka Zanzibar na ombi letu likakubaliwa hapa Bungeni, kwa hiyo, mimi leo namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu afanye mawasiliano na Zanzibar kwa kuwa fedha hizi tuliziomba ndani ya Bunge lako Tukufu afanye mawasiliano na Zanzibar ili tuweze kujua fedha hizi ziko wapi na zinafanya nini. Kama zipo kwenye utaratibu mwingine, basi pia tuweze kuelezwa ili wananchi hawa wafanyabiashara ndogo ndogo ambao wanaitwa Wajasiriamali wakituuliza tuweze kuwajibu; tunakuwa hatuna majibu ya uhakika juu ya fedha hizi. Marais wetu wetu hawa walizitoa kwa nia ya dhati ya kuwaendeleza Watanzani wajasiriamali, naomba sana Serikali izisimamie fedha hizi ili ziweze kuwanufaisha wafanyabiashara walio wengi.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ambalo nataka kulizungumza kidogo ni kuhusu Muungano.

Mimi binafsi yangu naupenda sana na Wanzibar wengi tunaupenda Muungano. Kama alivyosema Mheshimiwa aliyeppita kuzungumza hapa, lakini mimi napata mshangao kidogo, tunapoweza kuongeza hizi kero za Muungano. Mheshimiwa Waziri Mkuu mimi naomba uwe mwisho sasa wa kuongezeka kwa kero hizi.

Mheshimiwa Spika, ni wakati muafaka sasa kabla hatujakwenda kwenye mchakato wa Katiba mpya, basi kero hizi ziwe zimetatuliwa ili tukifanya mchakato huu wa kupata Katiba mpya tusiweze kuwa tena na kero zile za nyuma zikawa ndiyo vikwazo sasa vyakusababisha Katiba yetu hii mpya nzuri ikaingia dosari za hapa na pale juu ya kutatuliwa kwa kero hizi.

Mimi nimepata mshangao mwingine kuona suala hili la ushauri ambalo wamelitoa Waheshimiwa Wabunge wa Zanzibar wa Majimbo, kusema Mfuko wa Jimbo baada ya kumalizia kwenye Halmashauri na zile Halmashauri hazihusiani na masuala ya Muungano kule Zanzibar, masuala haya ya fedha hizi za Mfuko wa Jimbo ziishie kwenye Ofisi ndogo ya Bunge ya Zanzibar nalo limejumuishwa hapa. Nisingependa kumkosoa Waziri Mkuu, lakini suala hili halikutendewa haki, tuseme sasa kero zilikuwa 12 na iliyotatuliwa ni moja na zimebakia kero 11.

Mheshimiwa Spika, sasa kila ninapopata nafasi ya kusimama hapa au nikichangia katika mchango wangu wa maandishi, huwa napenda sana kuwasemea wastaafuli, hawa walikuwa ni

wafanyakazi wazalendo ndani ya nchi hii ambayo inaongozwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Kuna baadhi ya wastaa fu walio wengi sana, wakistaafu wanapata mafao yao mapema, lakini wapo wachache bado wanaendelea kudhalilika. Nasema kudhalilika kwa sababu kama mstaafu anayetoka Wizara ya Muungano akiwa Zanzibar, wapo wengine mpaka wavuke Bahari waje Tanzania Bara kufuatilia mafao yao, hili siyo jambo zuri. Naomba watu hawa wapatiwe mafao yao haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, lakini siyo hilo tu. Katika kitabu hiki cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, amewasifu sana Askari wa Jeshi la Polisi wanavyofanya kazi kwa umahiri mkubwa na uzalendo mkubwa wa kupenda nchi yao. Lakini anapotokea Askari huyu kufa, mjane na familia yake wanateseka. Naomba wapate mafao haya haraka. Watanzania tumezoea kufarijiana katika misiba mbalimbali inapotokea, ni vema, sasa kwa makusudi mazima Serikali ihakikishe mfanyakazi yejote anapofariki, basi familia yake inayobakia ifarijiwe kwa kupewa mafao yake haraka iwezekanavyo kuliko kuachwa kuhangaika kuteseka na kudhalilika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sisi wengine tumekuwa wachangiaji wa mwisho mwisho, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na ninaendelea kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante. Mwisho wapi? Wewe siyo wa mwisho, kwani bado kuna wengine. Mheshimiwa Namelok Sokoine!

**MHE. NAMELOK E. M. SOKOINE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kusimamia Serikali kwa umakini katika kutekeleza dhana ya Chama cha Mapinduzi. Vilevile nachukua nafasi hii kuwapongeza Mawaziri na Watendaji wote waliosimamia utekelezaji huo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na misukosuko ambayo bado inaendelea kuzikabili nchi mbalimbali duniani kwa viwango tofauti na Tanzania tukiwa wamojawapo, lakini bado tumeweza kupata mafaniko kama tulivyooona katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kama muda utanitosha, nitazungumzla mambo manne. Nitazungumzia tatizo la ardhi, adha wanazokutana nazo wakazi wa jamii ya Ngorongoro; nitazungumzia pia tatizo la maji na tatizo wanalokumbana nalo wakazi wa Jiji la Arusha.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya ardhi ni mengi mno, lakini mimi nitazungumzia mambo matatu tu. Nitazungumzia tatizo la ardhi wanalokumbana nalo jamii ya wafugaji. Kuna tatizo kubwa sana kati ya

wafugaji na wakulima, kuna tatizo kubwa sana kati ya wafugaji na maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori, lakini pia kuna tatizo la ardhi la mipaka kwenye Wilaya zetu.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Kamati yetu ya Kilimo, Maji na Mifugo tulikwenda kutembelea eneo la Ikwiriri. Kulikuwa na ugomvi mkubwa sana kati ya wakulima na wafugaji katika eneo hilo ambao hata imapelekea mauaji. Lakini kitu cha kushangaza, Serikali hadi hivi sasa wameshindwa kutatua migogoro hiyo. Wafugaji waliokwenda katika eneo lile walikuwa wamejitayarisha kwa ajili ya ng'ombe 50,000 lakini kitu cha ajabu kuna ng'ombe zaidi ya 300,000 na hata Serikali hadi hivi sasa hajatoa tamko lolote. Tulipokwenda kukutana na jamii ile, walisema itakapofika tarehe 30 mwezi huu wataamua kuchukua sheria mkononi, kwani hawataki tena kuwaona wafugaji wale katika eneo lile.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hilo, pia lipo tatizo katika hifadhi za wanyamapori. Kuna hifadhi ambazo zimepakana na jamii ya wafugaji. Hivi karibuni tukiwa katika Bunge hili, tarehe 12 Juni, kwenye Hifadhi ya Mikumi Wilaya Kilosa wapo ng'ombe walipigwa risasi, walikwenda kunywa maji katika eneo lile na hii imekuwa kawaida kabisa kwa Hifadhi za Wanyamapori (*TANAPA*) kupiga ng'ombe risasi au kuwachukua ng'ombe wale na kuwadai watu fidia ya Sh. 10,000/= kwa ng'ombe mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika katika Wilaya ya Monduli kuna mgogoro wa mpaka kati ya Wilaya ya Monduli na Arumeru, hali kadhalika Wilaya Longodo na

Arumeru. Najua Serikali ina suluhisho ya matatizo yote hayo, lakini kitu cha kushangaza ni hadi sasa migogoro hiyo inaendelea na Serikali haitoi tamko lolote.

Mheshimiwa Spika, nafahamu nchi yetu ina wataalamu wengi wa mifugo ambao wanaweza kutuambia ng'ombe mmoja kwa mwaka mzima anakula kilomita ngapi na baada ya kufanya hivyo wakafanya sensa ya wanyama na kujua tuna mifugo wangapi, kila watu wakabaki na mifugo yao katika Mikoa yao, wakapewa maeneo ambayo itakuwa kwa vitalu na mifugo ile ikala kwa *rotation*, badala ya hivi sasa ambapo wafugaji wanazunguka tu hawaelewi *wana-belong in which society. (Makof)*

Mheshimiwa Spika, hata ukiangalia dhana ya Kilimo Kwanza, haielezi mfugaji anafaidikaje. Wakulima wanapewa pembejeo, lakini mfugaji haelezewi anafaidikaje na kuwa na dhana ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili nitakalozungumza ni kuhusu Hifadhi ya Ngorongoro. Kuna jamii ya wafugaji inaishi ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro. Mwaka 2008 Serikali iliwasimamisha jamii ile kulima bustani, sote tunafahamu ni jamii ya wafugaji ambao hawafanyi biashara na hawana shughuli nyingine yoyote zaidi ya mifugo. Lakini wakati Serikali inawasimamisha, haikuwaambia pia watapata wapi chakula na wataishije.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa jamii ile wanateseka sana. Unapofika Karatu, Arusha na kila mahali unakutana na akina mama wanakwenda kuuza ugoro,

akina baba dawa za kienyeji, vijana wamekwenda kuwa walinzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vijana wale wengine wanaweza kufanya kazi za ulinzi ndani ya hifadhi ile na pia wanaweza kuajiriwa wakawa madereva na kufanya *petty jobs*, lakini kitu cha ajabu wameachwa tu. Hakuna kipaumbele chochote kinachotolewa kwa jamii ile. Nitafurahi sana wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anahitimisha hotuba yake atueleze hili la Ngorongoro. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nafahamu kuna Baraza la Wafugaji ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro, lakini limekaa kisiasa zaidi. Nilikuwa nashauri kama Serikali inaweza, kungeundwa Mabaraza mengine mawili; Baraza la Wanawake na Baraza la Vijana; na Mabaraza hayo yakawezeshwa na wakapata elimu ya ujasiriamali.

Bahati nzuri hili liko chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambapo kuna Uwezeshaji na Uwekezaji. Mabaraza haya wakatafutiwa wawekezaji ambao watawafundisha wakapata mbegu bora ya mifugo, lakini pia kutokana na mbegu hiyo ya mifugo wakaweza ku-*pack* maziwa, *cheese* na kadhalika ambayo itauzwa katika hifadhi hiyo, wakaweza kupata pato lao kuliko hivi sasa wanavyoteseka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo linalowakumba wakazi wa Jiji la Arusha kwamba hatuna soko, na hatuna stendi. Soko la Arusha Mjini lilijengwa mnamo miaka ya 1970 wakati ule *population* ya watu wa

Arusha ilikuwa kama laki moja hivi, tofauti na hivi sasa ambapo *population* ya Mji wa Arusha ni 590,000. Soko lile linatumwiwa na watu wa Wilaya tatu za Arumeru Mashariki, Magharibi na Arusha Mjini. Hata watu kutoka Wilaya nyingine wanapokuja pale kuleta mazao wanaauza kwa jumla na kuondoka. Kuna msongamano mkubwa sana katika Soko la Arusha Mjini kiasi kwamba, inafikia saa 10.00 jioni kuna barabara imefungwa, watu wame-*pack* bidhaa kila mahali.

Mheshimiwa Spika, nilijaribu kuzungumza na wengine, wananiambia kwamba wana marejesho kila wiki, hawana namna ya kufanya marejesho wasipofanya biashara ya kuuza chakula, kwani hiyo ndiyo biashara ya uhakika ambayo wanaiamini. Lakini sasa nadhani ni wajibu wa Serikali kuwatafutia sehemu nzuri ya kufanyia biashara kwa kuwajengea soko kubwa la kisasa. (*Makof*)

Syo hilo tu, pia tuna tatizo la stendi. Arusha Mjini hakuna stendi. Tunaomba Serikali ifikirie ni kwa namna gani tunaweza tukajengewa stendi na soko la kisasa. Pale Arusha Mjini kuna eneo la wazi la *NMC* ambalo ni mashuhuri kwa kufanyia mikutano ya dini na kisiasa na hata hivi sasa limepata umashuhuri mkubwa, linaitwa *Arusha Tariri Square* kwa ajili ya mikutano ya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nashauri, badala ya barabara hizo kuendelea kufungwa na watu kuweka vyakula njiani ambayo ni hatari, kwani kuna milipuko ya magonjwa inayotokea kwa wingi sana wakati wa mvua. Nilikuwa nashauri Serikali itukubalie eneo lile watu waweze kuweka vitu kwa muda wakati tuko

kwenye kipindi cha mpito tukisubiri kujengewa soko kubwa la kisasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiacha hilo, lipo tatizo la maji ambalo linatukabili wakazi wa Arusha Mjini na Wilaya zote sita ndani ya Mkoa wa Arusha. Tatizo la maji ni kubwa sana ndani ya Mkoa wa wetu wa Arusha. Wilaya zote sita hazina maji ya kudumu. Mheshimiwa Rais alipokuja Arusha mwaka 2010 alisema apelekewe *Arusha Water Plan*. Lakini mpaka sasa *master plan* ya maji hajapelekewa, haijaandikwa na hatufahamu ni kwanini. Tulikuwa tunaomba Serikali isimamie ili Wilaya zote sita ndani ya Arusha Mjini ziweze kupata maji ya kudumu.

Mheshimiwa Spika, vilevile tarehe 24 Juni, 2011 wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mbunge wa Monduli Mheshimiwa Edward Lowassa aliomba Monduli tuingizwe kwenye *list* kama ilivyo Makondeko, *Chalinze Water Basin*. Nami leo kwa mara ya pili nasimama kuendelea kuiomba Serikali ili tuweze kuingizwa katika *list* hiyo. (*Makofi*)

(*Hapa kengele illilia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha*)

**MHE. NAMELOK E. M. SOKOINE:** Kengele ya pili hiyo?

**SPIKA:** Ya pili mama, ahsante.

**MHE. NAMELOK E. M. SOKOINE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu Sub-hanah-wataala kwa kunijalia afya na uzima na salama, na kuniwezesha kushiriki katika hotuba hii muhimu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia na pia nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Kikwete na Serikali yake kwa kututengea maeneo mapya ya utawala.

Mheshimiwa Spika, tumepeata Wilaya mbili mpya jambo ambalo tumelilia kwa muda mrefu na hatimaye limefanikiwa. Hivyo, tuna kila sababu ya kutoa shukrani. Tumepeata ma-*DC* wazuri, nawapongeza na hasa *DC* wangu wa Wilaya mpya ya Ikungi. *Comrade Manju Msambya* ambaye ni mwenzetu tunamfahamu vizuri sana. (*Makofi*)

Nimpongeze sana Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Singida Dkt. Paseko Kone kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kuifanya na kutupa ushirikiano sisi Wabunge na wananchi kwa ujumla. Nimitakie kila la kheri na kuahidi kwamba tutaendelea kushirikiana naye vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 26 Agosti, kutakuwa na sensa kama tulivyoarifiwa. Naikubali na tumeshafanya kazi ya kuwahamasisha wananchi kama tulivyotakiwa, na wako tayari kushiriki katika Sensa. Ombi langu ni kwamba kwa muda mrefu Mheshimiwa Waziri Mkuu anajua kulikuwa na *concern* kwamba, sisi watu wa

Mkoa wa Singida tunaitwa Mkoa wa mwisho, jambo ambalo siyo haki na kwa kweli hatustahili kuitwa kuwa Mkoa wa mwisho kutokana na maendeleo ambayo yamefikiwa katika Mkoa wa Singida. Haiwezekani kabisa! Ni takwimu mbovu za miaka mingi zilizotumika ambazo mimi nachelea, ni kwanini hazitaki kurekebishwa? Ukiangalia Mkoa wa Singida na Mikoa mingine ambayo sitaki kuitaja hapa nitawa-*offend* watu. Haiwezekani Mkoa wa Singida kuambiwa kuwa ni wa mwisho. Haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kupitia sensa hii kwa sababu katika madokezo, najua vigezo vyakimaendeleo ambavyo viko mle ndani vitatumika. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba suala hili sasa angalau limepata fursa hii ya sensa, sasa itumiwe ili kupata takwimu sahihi za kuweza kuuweka Mkoa wa Singida katika mahali pake. Hatuko tayari kuendelea kuambiwa kwamba sisi ni Mkoa wa mwisho wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu umekuja mara nyingi na hata wewe huridhiki. Lakini sijui ni watu gani hawa ambao wanaendelea kutunyanyasa kwa kutuweka Mkoa wa mwisho wakati sisi hatustahili kuwa wa mwisho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, moja ya kero ambazo wapigakura wangu wamenitura na wamekuwa wakinililia, ni suala la soko la zao la biashara la alizeti. Tulihangaika sana, muda mrefu hatukuwa na zao la biashara. Sasa tumepata zao la biashara la alizeti. Tatizo ni kwamba wako walangazi ambao wanakwenda vijiji na mashambani kuwalangua wananchi kwa kuwapa bei duni kabla hata alizeti

yenewe bado ni mbichi na iko shambani. Sasa ukienda kuwahamasisha, wanasesma tunalima alizeti, lakini soko hatupati, mnawaachia walanguzi wanakuja.

Tunatoa majibu kwamba sisi hatuwaachii isipokuwa nyie wenyewe mnaridhika. Lakini ukweli ni kwamba walanguzi wale wanawanyanya sana na kuwadhulumu wananchi wetu. Sasa hivi karibu Mkuu wa Mkoa wa Singida ametoa maelekezo kwamba alizeti inunuliwe na Vyama vya Ushirika na katika magilio. Jambo hili linapingwa na baadhi ya watu ambao wana maslahi binafsi. Mimi kama Mbunge wa Jimbo ambaye wananchi wangu wakulima wanalamika kila siku, alizeti yao inapotea, wanadhulumiwa na walanguzi, hao watu wa katikati. Nitakuwa mtu wa ajabu sana kama nikipingana na azimio la Mkuu wa Mkoa ambaye nia yake ni kumsaidia na kumkomboa mkulima apate bei sahihi na nzuri ya zao lake la biashara. Kwa maana hiyo, naliunga mkono azimio la Mkuu wa Mkoa kwamba, watu waende kwenye Vyama vya Ushirika au magilio kwenye ushindani. Wewe usiende kuwalangua watu kule Kijiji wakati alizeti yenewe bado, halafu unaanza kumdanganya gunia Sh. 15,000/= wakati sasa hivi bei ya soko kwa gunia ni Sh. 40,000/= tayari Serikali imeshatoa bei elekezi ya Sh. 600/= kwa kilo, jambo ambalo hawa walanguzi hawawezi wakatoa kitu kama hicho hata siku moja.

Mheshimiwa Spika, naomba sana tutoe ushirikiano kwa Mkuu wa Mkoa na Serikali yake kwa sababu nia yake ni kumsaidia mkulima ili asiendelee kunyonywa, kwani amenyonywa kwa muda mrefu sana, na sisi

viongozi wengine tushiriki kutoa elimu inayostahili. Uamuzi wowote unaweza ukawa na pande mbili; una faida na hasara zake. Hakuna maamuzi ambayo utafanya ambayo hayatakuwa na pande mbili. Kazi yako ni kuangalia uzuri uko wapi na yale machache ambayo unaona kwamba yana mapungufu unayafanyia kazi. Namwomba Mkuu wa Mkoa kama kuna matatizo yataonekana dhahiri kabisa, labda kuna hiyo *contract farming* na nini, lakini wameshaahidi Serikali ya Mkoa iwe tayari kukaa na wale wafanyabiashara wenye viwanda, watatue yale matatizo. Tusi-*generalise* tukazuia mpango mzuri eti kwa sababu ya watu ambao pengine wana maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana hilo lifanyike. Lakini kazi kubwa zaidi, sisi ni viongozi wa siasa, viongozi wa kuteuliwa, tuendelee kuwaelimisha wananchi wetu umuhimu wa kuuza mazao yao katika Vyama vyta Ushirika na kwenye magilio na waachane kabisa na hao walanguzi ambao wanakwenda kuwadanganya katika maeneo yao mbalimbali. Hilo ndilo lingine ambalo nilitaka nilisemee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilitaka nilisemee ni suala zima la ndege waharibifu. Hakuna hata siku moja hapa nimezungumza bila kugusia ndege waharibifu na Serikali yote inajua, Waziri Mkuu anajua, Mawaziri wa TAMISEMI wote wanajua, kila mtu anajua pale mpaka Rais wa nchi nimewambia alipotembelea kule Singida, lakini hakuna utatuza. Ndege waharibifu wanaharibu sana mazao ya wananchi, mazao ya biashara na chakula. Watu

wanafanya jitihada sana kulima, lakini maskini ya Mungu *at the end of the day* ndege wanakula kile chakula. Sasa wananchi hawaelewi hivi ni mpaka lini Serikali itasikiliza kilio chao cha kutafuta njia nzuri ambazo zinaweza zikawasaidia wananchi wetu wakaondokana na adha hii.

Mheshimiwa Spika, hii ni kadhia kubwa. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu aliangalie hili. Naambiwa hii ndege ambayo tunaitumia ya kuangamiza ndege inamilikiwa na nchi sita au saba. Ndege yenewe ni ya miaka karibu thelathini, kuu kuu. Kwanza ni kuu kuu, halafu moja, na pia ni ya nchi sita au saba. Tunazungumzia Kilimo Kwanza, huwezi kufanikiwa Kilimo Kwanza kama ndege waharibifu wataendelea kumaliza chakula cha wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nishauri, *it is high time* sasa Serikali iangalie uwezekano wa kupata ndege zake kama siyo mbili, basi angalau moja ya kuanzia. Tuachane na hii ambayo wakati wewe unaitaka iko Malawi, unaambiwa sijui iko Botswana, mara unaambiwa sijui iko Angola. Hivi kweli tunadhania Kilimo Kwanza wakati tunategemea ndege moja tu ambayo inatutesa kiasi hiki? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana tununue ndege zetu, na zije kwa wakati. Mazao yanaanza Januari, Februari na Machi, muda unajulikana, kwanini Wizara ya Kilimo hailijui hili mpaka tuanze kuombaomba ndege? Sasa Wizara ya Kilimo iweke utaratibu, Serikali inunue ndege moja au mbili na kadhalika. Lakini juzi

Jumatatu saa 3.00 usiku *TBC1* walirusha kipindi wakaonesha mgunduzi mmoja amegundua mashine ambayo inafukuza ndege waharibifu na hawa wanyama waharibifu. Hebu msaidieni yule mgunduzi mwananchi, Mtanzania ili kusudi tupate suluhu juu ya jambo hili ambalo linafanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji wa Benki ya Dunia umefeli. Jina lake ni kubwa *World Bank* lakini hauna kitu. Mimi nadhani tusidanganyane hapa. Tutafute njia mbadala ya kuwapatia watu wa Singida maji. Tusiendelee kusema kwamba, mna mradi wa Benki ya Dunia, hakuna kitu ni bomu tupu hapa. Mradi una miaka 10, una vijiji kumi. Wewe angalia, yaani mwaka mmoja kijiji kimoja, mwaka mmoja kijiji kimoja, ni mradi gani huo?

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu atutafutie mradi mwingine ambao utakidhi mahitaji ya maji hasa kwa maeneo ya vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atupe *progress report* ya suala la Mahakama ya Kadhi. Yeye amekuwa anasimamia mazungumzo kati ya Serikali na jopo la Mashehe kwa ajili ya kupata ufumbuzi wa suala la Mahakama ya Kadhi. Sasa mimi namwamini Mheshimiwa Pinda, nina hakika ameifanya kazi hiyo na anaendelea kuifanya. Ningependa sana wakati atakapokuwa anajumuisha, tupate *progress report* ya suala la Mahakama ya Kadhi. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria muda wa  
Mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Ahsante, tunashukuru sana kengele ya pili.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Eeh. Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kunipa fursa hii adhimu ya kuweza kuchangia hoja yetu ya chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nami niungane na wenzangu kwanza kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kwanini naunga mkono hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mia kwa mia kama kiongozi wetu wa shughuli za Kiserikali hapa Bungeni, kwa maana ndiye kinara wa usimamizi, utekelezaji wa kero za wananchi katika nchi yetu. Naomba niseme kwamba, tunasemwa sana wakati mwingine kwa kuwa sio wachangiaji sana, hatusemi sana, lakini naomba tu siku ya siku tuhukumiwe kwa kazi zetu tulizozifanya. Naamini wananchi wa Mafia walionichagua hawataniuliza siku moja kwanini hujatoa miongozo mingi hapa Bungeni, sijatoa taarifa nyingi wala kuomba nafasi za kuweza kusimama kila wakati. Lakini akili ni nywele, kila mtu ana zake na tumekutana hapa Dodoma kwa niaba ya wananchi wetu. Kwa hiyo, wakati mwingine kila mtu anakufa na lake.

Mheshimiwa Spika, binafsi nasema naomba niipongeze sana na kutoa shukrani nyingi kwa Serikali

yetu hasa kwa kazi nzuri ambayo ilikuwa kero sugu ya ujenzi wa Gati la Mafia. Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba upokee shukrani hizi za wananchi wa Mafia, Gati letu linaendelea na wakati wowote litakamilika. Mheshimiwa Rais pamoja na wewe na Wizara yote na ikiwezekana kwa sababu ni kitu ambacho ni cha kihistoria, basi Wizara ya Uchukuzi chini ya Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, hebu alika siku hiyo ya kuja kuzindua Baraza lote la Mawaziri lije kule maana ni jambo la kihistoria kwa Wilaya yetu ya Mafia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naishukuru tena Serikali kwamba *Airport* inajengwa na vifaa viliishafika na kazi inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Mwakyembe nakuomba upokee shukrani zetu za Wizara yake na Idara zake zote kupitia Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara katika ujenzi wa uwanja wa ndege, kuna barabara na iliishafanyiwa tathmini. Ninachokuomba kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe anatusikia hapa kwamba tutakuja kuelezewa mengine, maana yake hatuwezi kupata muda, muda wenyewe ni mchache, lakini tathmini tayari imefanyika zaidi ya miaka minne iliyopita. Naomba sana, ujenzi wakati wowote unategemewa kufanyika, na ninaamini katika bajeti hii, inaelewa fedha ya kulipa fidia (*compensation*) wale watakaohamishwa itatolewa, lakini muangalie na hali ya maisha ilivyo.

Mheshimiwa Spika, lugha yetu ya kuongea ni nyepesi, hatutoi ukali, tunataka kwa maana ya kuiomba Serikali iangalie tathmini iliyofanya miaka minne iliyopita na hali ilivyo sasa hivi. Wakati ule mfuko wa sementi kule Mafia ulikuwa Sh. 13,000/= lakini leo ni Sh. 20,000/= mpaka Sh. 22,000/=, na wakati mwingine kama pepo za bahari zinakuwa kali, usafiri unakuwa mgumu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine nililokuwa nataka kulizungumzia baada ya shukrani hizo, katika jambo lolote la heri na changamoto zinakuwepo. Kwa hiyo, naomba sana kutoa changamoto zangu kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu pengine sitaweza kupata bahati ya kuchangia Wizara zote. Naomba sana tuangalie, Mafia tumeanzisha Benki ya Watu wa Mafia. Tumejitahidi sana, leo tunakaribia mwaka mmoja na nusu. Hali yetu tumechemsha katika kukusanya mtaji wa Shilingi milioni 250 kwa ajili ya kupata *licence* ya kuanzisha benki ile. Lakini tumejitahidi, tuna fedha chache Shilingi milioni kama 40 tulizoweza kufikia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na bahati nzuri Mheshimiwa Mama Nagu anatusikia kupitla Baraza lake la Uwezeshaji, atusaidie katika kuihuisha hii benki iweze kufanya kazi. Benki ya Watu wa Mafia itatusaidia sana kwa sababu wote tunalalamika na tunafahamu kwamba Mabenki haya ya kibiashara shughuli zake zinakuwa nzito sana katika ukopaji. Tukianzisha Benki yetu na mkituwezesha kama hamwezi kutupa *grant*, kama mlivyoweza kuisaidia Benki ile ya Wanawake, basi tusaidieni na Benki ya Watu wa Mafia tuweze kuihuisha ifanye kazi.

Naona Mheshimiwa Nagu anatikisa kichwa, nafikiri ameelewa na atatusaidia. Nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, linge ni kero ya watumishi wa kawaida. Hili ni jambo la nchi nzima, watumishi hasa wa kada ya afya. Tunajua tupo katika mtikisiko sasa hivi wa huduma hii kupitia Madaktari wetu. Lakini jambo lolote lile linakuwa na mwisho, hakuna jambo lisilokuwa na mwisho, yatakwisha, yatatalia na nafikiri Serikali kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba wako mbioni katika kumaliza kero zao, basi litakapomalizwa tuangalieni sana watumishi wa Idara ya Afya katika Wilaya ya Mafia.

Mheshimiwa Spika, tuna kazi nzito. Ninapata mzigo mzito, kila inapotokea dharura, basi huwa inabidi nichangie katika kumsafirisha yule mgonjwa kutoka Mafia kumleta Dar es Salaam. Gharama ni kubwa na mimi niko mmoja, watu wanaougu ni wengi, wakati mwingine tunachemsha, inabidi tukusanye wagonjwa wawili, watatu kuwasafirisha kwa njia ya bahari, uwezo wa ndege hatuna. Lakini tukipata wataalamu hawa na bahati nzuri vifaa viro sasa hivi Mafia *X-Ray* inafanya kazi, mtaalamu yupo na baadhi ya vifaa kama *ultrasound* na vingine viro vitawezza kusaidia katika kuwatibu pale pale hawa wagonjwa wanaotokea kule Mafia. Naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na bahati nzuri kaka yangu Dkt. Hussein na Dkt. Seif wanatusikia, mpo pale mtuangalie sana mtuonee huruma watu wa Mafia tunapata kazi nzito, aliyekuwa Bara tofauti na sisi Visiwani. Hali ya Visiwa mnaifahamu, kwa hiyo, sina mengi ya kusema.

Mheshimiwa Spika, lakini suala la Walimu pia ni kero katika Wilaya yetu hasa Walimu wa Shule za Sekondari na Msingi kwa sababu tatizo tunalopata Mafia kwa uchache wa wanafunzi waliokuwa katika shule zetu na vigezo vilivyowekwa na Wizara ya Elimu kwamba Mwalimu mmoja kwa wanafunzi 40, matokeo yake Walimu wachache tunapata na Shule, inakuwa na Walimu wawili hadi watatu. Kwa hiyo, naomba sana suala hili na bahati mbaya miaka mitatu iliyopita Mafia hatukupata Walimu waliopangiwa kuja Mafia. Kwa hiyo, naomba mwaka huu tupangiwe Walimu na tutajitahidi kuongea nao na bahati nzuri tunaboresha mazingira yao ya kuishi vijijini. Tunawawekea katika nyumba za Walimu umeme juu sasa hivi, kwa hiyo, hata akiwa pale ataweza kuwasiliana na wenzake kwa maana ya kuweza kupata huduma zile ambazo yeye atazihitaji kama za kimawasiliano. Kwa hiyo, hili lipo na bahati nzuri kuna mengine tutakuja kuchangia tutakapokuwa katika Wizara ya Nishati na Madini, tutayasema mengi mazuri ambayo sasa hivi Mafia yanaelekezwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine na hili ndilo jambo sugu ambalo nataka nilizungumzie, Mheshimiwa Rais alipokuja Mafia alitoa ahadi, tulimwomba na akasema itatekelezwa. Ahadi kubwa ambayo inatusumbua sasa hivi ni maji katika visiwa vidogo vidogo vya Mafia. Tumejitahidi sana, lakini kama Wilaya kutokana na kigezo tunachopata cha fedha, fedha ndogo tunazozipata za ruzuku, basi tunaomba sasa Wizara ya Maji na Umwagiliaji ilibebe hili, waje kutusaidia katika kuhakikisha kwamba ahadi ya Mheshimiwa Rais inatekelezwa na yale maji yaliyokuwa

na bahati nzuri, visima tumeshachimba, sasa tunatafuta nguvu ya kuweza kununua *pipe* na kuzivusha na siyo mbali sana kama kilomita sita tu. Kwa hiyo, tusaidieni Serikali na naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu alibebi hili suala awaambie Wizara itafute fungu tuweze kuondoa kero hii ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Ni aibu tutakapomaliza kipindi chetu cha safari hii kwa maana awamu hii, basi ahadi ile isipotekeliezwa itaonekana sijui hatusemi ukweli au kitu gani. Kwa hiyo, naomba sana hii ahadi sasa hivi Serikali Kuu muibebe na iweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumza ni suala la uvuvi. Mafia asilimia kati ya 70 au 80 sisi ni wavuvi tunategemea bahari. Lakini kitu ambacho kinatusibu sasa hivi kupitia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu atusaidie kuwaambia watu wa Wizara hiyo waunde Kamati Maalum ya kuweza kuchambua na kufahamu kwamba ni jinsi gani bahari yetu inaweza ikachangia pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, ni aibu kuambiwa kwamba nchi hii ya Tanzania uvuvi au bahari inachangia asilimia moja. Hebu basi wavezesheni hawa wazunguke katika nchi jirani tu zilizokuwa katika nchi hii hii ya bahari ya Hindi waone jinsi bahari wenzetu wanavyoitumia vizuri katika kuondoa umaskini au kuwezesha nchi yao kupata fedha, na hizi kero nyingine kwa mfano za Madaktari fedha zao hata mishahara itapanda.

Mheshimiwa Spika, leo naunga mkono, lakini naomba suala la uvuvi lizungumzwe sana kwa sababu

wananchi wa Mafia na ukanda wa Pwani wanawategemea. (*Makofii*)

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ama kweli mama ni mwenye huruma. Nianze kutoa mchango wangu kwenye maafa. Katika ukurasa wa 58 Na. 95 inasema: "Katika mwaka wa 2011/2012 Serikali imeshughulikia matukio ya maafa katika maeneo mbalimbali nchini." Pia katika ukurasa wa 96 imetaja waathirika wa Mabomu ya Gongolamboto. Hapa nitamtaka Mheshimiwa Waziri Mkuu, atakapokuja kufunga mjadala atuambie ni kwa nini hajaonyesha kwamba Zanzibar kulitokea maafa makubwa ambayo yaliwashtua Watanzania na dunia kwa jumla?

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia katika Muungano. Kwa kawaida Muungano wowote duniani hutegemewa kuongeza nguvu kwa walioungana. Siyo kupunguza nguvu zote za upande huo na kuelekeza upande mmoja ukabaki bufurutupu. Zanzibar ina uwezo wa kupanga mipango yake ya kiuchumi, huduma za jamii na miundombinu. Lakini huwezi kupanga haya bila kujua takwimu ya watu wako na kujua maksio ya wageni wako. Zanzibar haina uwezo wa kudhibiti lolote.

Tuangalie mfano wa *Hong Kong* na *Mak Hou* hivi ni visiwa vya China. China kwa kuvienzi na kuviendeleza visiwa vyake, basi pamoja na kwamba China ni moja, lakini Mchina kutoka Bara hawezi kuingia Hong Kong na *Mak Hou* kiholela bila udhibiti wa aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, uingiaji wa Zanzibar ulikuwepo utaratibu kabla ya Muungano na hata baada ya Muungano, lakini ikafanywa nongwa vikaondolewa. Leo Zanzibar ni nchi pekee duniani ambayo haina uwezo wa kudhibiti uingiaji wa watu. Unaweza kutoka Congo ukapitia taratibu zote za kuingia Dar es Salaam, kwani kwa hilo mko makini, lakini ukishaingia Dar es Salaam, basi utaingia Zanzibar na utateremka kama shamba la bibi.

Mheshimiwa Spika, hakuna ubishi kwamba Mataifa mengi duniani yameungana, lakini tusiishie hapo twende mbali zaidi tuone huu Muungano wao ni Muungano wa namna gani? Ni Muungano wa kumezana au ni Muungano wa kudhoofishana kama vile ambavyo Muungano huu unaidhoofisha Zanzibar na kuifuta katika ramani ya dunia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda niseme jambo moja, mpaka unapomwona mtu mzima analia, basi ana jambo kubwa, mwulize unalilia nini? Leo Zanzibar kusema hawataki Muungano huu, basi waulizwe kulikoni? Wanautaka ama hawautaki? Villevile tujiulize kama huu Muungano wetu ni mzuri au ni tunu ya kuenziwa? Mbona umedumu miaka 50 hadi leo hakuna hata mmoja aliyetamani kujeunga na Muungano huu?

Mheshimiwa Spika, nitarudia. Nasema tujiulize ikiwa Muungano wetu ni mzuri ama ni tunu ya kuenziwa, umedumu miaka 50, mbona hakuna hata mmoja au hata nchi moja iliyotamani kujeunga na

Muungano huu na hata wakati lilipokuja wazo la kuunda Afrika Mashariki hakuna aliyetamani kuuendeleza huu?

Mheshimiwa Spika, hata Umoja wa Ulaya ulipoundwa, walianza na wanachama sita, leo takribani ni 30. Huu ndiyo Muungano. Nimalizie kwa kusema kama aliyosema Waziri Membe. Mheshimiwa Membe alisema: "Watanzania tutakuwa tayari kujifunga mikanda tufe kwa njaa kuliko tusaidiwe tuingie katika ndoa za jinsia moja." Wazanzibar nao wanasema tuko tayari tufe kwa njaa kuliko kubakia katika Muungano huu dhalimu ambao haututendei mema, ambao ni Muungano wa kutudhoofisha na wa kutudhalilisha na kutufuta katika ramani ya dunia.

Mheshimiwa Spika,...

## TAARIFA

**SPIKA:** Taarifa, lakini kengele itagongwa sasa hivi.

**MHE. MOHAMED AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa ndugu yangu kutoka Zanzibar, Wazanzibar wanaojua kwao ni Zanzibar, wenzangu kama mimi siwezi nikakataa Muungano hata siku moja. Kwa hiyo, hiyo ni yake yeye mwenyewe. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante. Bahati nzuri wakati unamtolea taarifa kengele ilimekwishagongwa. Kwa hiyo, unathibitisha kwamba hawa Wazanzibar, hamkuwa wote, basi.

Tunaendelea, Mheshimiwa Magdalena Sakaya halafu Mheshimiwa John Lwanji atafuatiwa na Mheshimiwa Susan Kiwanga kama kutakuwa na muda.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuweza kunipa nafasi hii muhimu niweze kuchangia kwa ufupi kwenye bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuchangia, naomba nitoe rai kwa Serikali iliyoko madarakani, nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nitoe rai kwa Watanzania wote tuweze kuilinda amani tuliyonayo Tanzania. Tunu hii tulioachiwa na Marehemu Mwalimu Nyerere muasisi wa Taifa hili, tumeshaanza kuona kuna dalili za maneno ya viongozi, maneno ya Waheshimiwa Wabunge, maneno ya wanasiasa ya kugusia suala la udini na suala la ukabila.

Mheshimiwa Spika, Serikali isikae kimya tukiacha maneno haya yakiendelea kutamkwatamkwa leo, kesho tutakuwa kama Burundi au kama nchi nyingine za Syria na maeneo mengine. Kwa hiyo, tunu tulioachiwa tuishike, ni almasi, ni keki, hatuwezi kuipata pengine popote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pili, niende kwenye pongezi. Nachukua nafasi hii kwa moyo wa dhati kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Tabora tuliyepewa, Mama Fatuma Mwassa. Kwa kweli tumepewa Mkuu wa Mkoa mwenye dhamira ya dhati, mama mchapakazi, mama mwenye nia ya kusaidia maendeleo ya Mkoa wa

Tabora. Naiomba Serikali im-*support*, wananchi wote wa Mkoa wa Tabora na viongozi tum-*support* kwa moyo wa dhati aweze kubadili maisha ya wananchi wa Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye mchango wangu, nianze na suala la afya. Mkoa wa Tabora umekuwa na huduma duni za afya kwa miaka yote. Mwaka 2011 wakati nachangia bajeti kwa miaka yangu yote saba sasa, kila mwaka nachangia suala la afya, na Serikali ilikuwa inatoa matumaini, lakini hakuna kinachofanyika. Mwaka 2011 wakati nachangia Bunge la Bajeti, Serikali ilisema kwamba kuna mpango kabambe kwa sababu walitoa taarifa hapa Bungeni kwamba Mkoa wa Tabora ni wa pili kwa huduma duni Tanzania za kiafya. Wakasema kuna mpango kabambe kwa kushirikiana na Benki ya Afrika kusaidia kuboresha huduma za afya Mkoa wa Tabora, wakianzia na hospitali kuu ya Kitete kuboresha miundombinu, kuweka mazingira vizuri, hospitali za kinamama za kujifungulia na mambo mengine na kwenda kwenye hospitali zote. Kwa mwaka mzima sasa hakuna juhudhi ambazo tumeziona kuweza kusaidia huduma za afya Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mkoa wa Tabora, Wilaya karibu zote wamejenga *dispensary* kwa nguvu zao miaka mingi. *Dispensary* zile zimekuwa zinadondoka, zimeliwa na mchwa, hazi pelekewi huduma, hawapeleki Watendaji, hakuna Waganga, mpaka leo bado hospitali kuanzia akiwa Mheshimiwa Profesa Mwakyusa amekuja Dkt. Mponda, aliyetoka

sasa hivi, tunaomba suala la afya Mkoa wa Tabora liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunashukuru kwamba Serikali imetupatia Wilaya mpya ya Kaliua. Niseme kwamba wananchi wa Wilaya ya Kaliua wamefurahi na wanaishukuru sana Serikali na wanaomba Wilaya mpya ya Kaliua ibaki ndani ya Mkoa wa Tabora kwa lengo la kusaidia huduma ziweze kuwa jirani na Mkoa wa Tabora. Pia Wilaya hii mpya tayari tumeshapata hospitali iliyokuwa imeshajengwa, hospitali ndogo, lakini hospitali hii ina nyumba mbili za Madaktari na mpaka sasa hivi haijafunguliwa, na hatuna mhudumu yejote. Kwa hiyo, tunaomba Serikali itusaidie kwa sababu sasa hivi ni Wilaya, tuletewe Madaktari hospitali ile ifunguliwe ili tuenze na *speed* mpya ya kuendeleza Wilaya yetu mpya ya Kaliua.

Mheshimiwa Spika, zipo hospitali ambazo Serikali inasema kila siku hapa kwamba huduma za akina mama wajawazito ni bure kwa maeneo yote. Lakini kwa Wilaya ya Urambo bado zipo *dispensary* ambazo zinawatoza akina mama fedha wanapoifungua. Mfano halisi *dispensary* ya Igagala, Tarafa ya Kaliua, mama akishajifungua kama hajatoa Sh. 6,000/= hatoki pale hata siku mbili tatu haondoki. Lakini Serikali kila siku Bungeni inatangaza kwamba huduma ni bure. Kwa hiyo, tunaomba Serikali isimamie maamuzi yake na matamko yake. Kama huduma kwa akina mama ni bure zitolewe bure kwa watoto ni bure na wazee ni bure zitolewe bure. Maagizo ambayo hayafuliwi na Watendaji hayaleti tija kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala la maji kwenye mkoa wangu wa Tabora. Naishukuru Serikali kwamba ina mpango kabambe wa kuleta maji kutoka Kahama. Lakini maji yale kama mradi ule utatekelezwa utazinufaisha Wilaya tatu tu ambayo ni Nzega, Igunga na Manispaa, bado Wilaya nyingine *particularly* Urambo kuna tatizo kubwa la maji.

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji wa *World Bank* umefeli, hakuna hata Kijiji kimoja ambacho kimefanikiwa kuwa na mradi wa *World Bank*. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ije na mpango mwingine, Wilaya nyingine kama Urambo, Uyui na nyingine utaratibu gani umeandaliwa kusaidia wananchi wale?

Mheshimiwa Spika, kwa Wilaya ya Urambo ambapo walipata maji kwa vijiji vitatu, wananchi wanayaangalia mpaka leo tangu mwaka jana mwanzoni. Maji yamepatikana, wameziba kile kisima, hayajasambazwa, wananchi wanayaangalia, tunaambiwa kesi iko Mahakmani. Naiuliza Serikali, inakuwaje wananchi wanateseka kupata maji ambayo yameletwa mpaka wanayaona kwa macho yao kwa kesi ambayo iko Mahakmani? Sasa imekuwa kama ni tabia, inapotokea tatizo mtu anakimbilia Mahakmani, lakini wanaopata shida ni wananchi wa Urambo. Kwa hiyo, naiomba Serikali iliingilie kati, visima ambavyo maji yamepatikana, yasambazwe wananchi wapate maji na yale maeneo mengine ambayo hawajachimba waende. Kwa sababu pesa ilishatolewa, lakini tatizo ni ufuatiliaji, wananchi wa Urambo wanapata shida sana, akina mama wanateseka kwa shida ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala la ardhi. Mkoa wetu wa Tabora ulikuwa unasifika kuwa na misitu mingi, lakini kwa bahati mbaya misitu yote *almost* imeshavamiwa, yote imekwisha. Kila mahali kumeshakuwa nyang'anyang'a. Kwa sasa hivi kwa maeneo mengi kila wananchi wanapokaa wanaambiwa wako hifadhini. Lakini ukifuatilia wananchi wamekaa kule kuanzia mwaka 1972 kabla ya operesheni vijiji leo wanaambiwa wako hifadhini. Unataka kusema Serikali ilikuwa wapi? Mpaka sasa hivi tunapiga kelele, hakuna hatua zinazochukuliwa na hivi ninavyoongea jana nimepigiwa simu kuna maeneo ya vijiji vitatu kilometa 60, Kangeme na Uyumbu wameambiwa wako hifadhini na wamekaa pale tangu mwaka 1972 mpaka leo, wamejenga kila kitu, *dispensary* zipo, nyumba zipo, wanaambiwa ziko hifadhini. Sasa tatizo la Serikali kuona misitu inaingiliwa wakanyamaza kimya halafu baada ya miaka 30 wanasema wananchi wako hifadhini, hatupigi hatua, na haya siyo maendeleo. Naomba juhudzi za dhati.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Tabora ziko tume nyingi zimetumwa na zimefanya utafiti wa maeneo ya hifadhi na wamegundua tatizo liko wapi. Maeneo hayajaainishwa, matatizo yapo, mgongano upo mkubwa, Serikali haifanyii kazi taarifa zile. Kwa hiyo, matatizo yanaendelea kuwepo, matokeo yake wananchi wapo mguu ndani, mguu nje, hawawezi kufanya shughuli za maendeleo kwa sababu hawajui wanastahili kuwepo pale au hawastahili.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye vyama vyamini. Vyama vyetu vyamini vimeundwa kwa nia

ya kuwasaidia wakulima na kusaidia kuinua kilimo. Kwa bahati mbaya sana kwa Mkoa wa Tabora na *particularly* Wilaya ya Urambo, vyama vingi vya msingi vinaingiliwa na Madiwani. Madiwani wengine wamekuwa ni Makatibu na Meneja wa Vyama vya msingi. Matokeo yake wanaingilia hata utendaji kazi wa Maafisa Ushirika, wanakosa nguvu. Kwa hiyo, vingi vimeduwa dhaifu kwa sababu Madiwani wanaingilia utendaji kazi wa vyama vya msingi. Imefikia mahali Diwani akiona kwamba aliyeko pale kwenye Chama cha msingi hamnufaishi yeye binafsi, anamtoa, anamweka mtu ambaye ni *weak* ili aweze kunufaika na kile Chama cha msingi. Kwa hiyo, matokeo yake vyama vimeduwa dhaifu vimeduwa na migogoro na hasa vile vinavyoendeshwa na Madiwani kama ni Makatibu Meneja. Naomba sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe agizo na mwongozo kwenye vyama vya msingi, Madiwani wote wasiwe Makatibu Meneja. Wawaachie wakulima wachague mtu wao ambaye wanajua ataweza kuendesha Chama chao kwa nia ya kunusuru vyama hivi na viweze kuwa na tija kwa sababu ndiyo nia ya msingi ya kuvianzisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye elimu. Suala la elimu imeduwa inashuka siku baada ya siku nchini kwetu na bado juhudhi ambazo zinachukuliwa sioni kama zinaleta tija kwa sababu kitendo cha kuwa na wanafunzi 5000 wasiojua kusoma na kuandika ndani ya mwaka mmoja kwenye Taifa, ni aibu. Lakini pia lipo tatizo la Walimu wapya kutokupewa mishahara yao kwa wakati, inakatisha tamaa. Kwa hiyo, nadhani tatizo la msingi ni maslahi na mahitaji ya Walimu. Hebu tuwasaidie Walimu tuone wafanye kazi yao kwa moyo

na dhati na tuone kama elimu haitainuka ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa haraka haraka lipo suala la Wakurugenzi. Sasa umefika wakati tuwe na Wakurugenzi wa Halmashauri ambao wanapatikana kwa njia ya usaili, wafanyiwe mitihani, tupate watu makini wanaofanya kazi vizuri na wanaoweza kuleta maendeleo kwa ajili ya Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Paul Lwanji, nafikiri Mheshimiwa Susan atapata nafasi jioni.

**MHE. PAUL J. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na pia ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, mimi niliunga mkono hoja hii toka kwenye Kamati, kwa hiyo, sina ugomvi kwa sababu wenzetu itabidi tuwape muda. Tukumbuke hivi karibuni Mheshimiwa Rais alilisuka Baraza lake la Mawaziri akateua Wakuu wa Mkoa, basi tuwape muda tuone hiki kipyaa walichokileta kama kinaweza kutukwamua.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa William Mgimwa, Waziri wetu mpya wa Fedha kwa juhudini alizozionyesha na umahiri mkubwa aliouonyesha katika ku-present. Kwa

hiyo, sina shaka kwamba tukiwapa muda huenda wakatuletea matunda.

Mheshimiwa Spika, siyo kwamba Serikali haijafanya kitu kwa siku zote hizi, imefanya. Jimboni kwangu mengi yamefanywa, barabara zinajengwa, umeme unapelekwa na mambo mengi mengine kadha wa kadha. Lakini tunachogomba hapa ni kwamba tumechelewa katika kupiga hatua kwenye masuala ya maendeleo, tumechelewa. Wakati tunapata uhuru, tulikuwa na matumaini makubwa kwamba tungesonga mbele haraka zaidi pamoja na matatizo yaliyokwisha kutokea. Lakini wenzetu Botswana walipopata uhuru mwaka 1968 miaka saba baada ya sisi kupata uhuru, *GDP per capita income* yao ilikuwa Dola 70. Lakini leo hii 2012 *per capita income* yao ni Dola 14,000 ambazo ni sawa na Shilingi milioni 21. Sasa leo hii *per capita income* yetu ni Dola 1,400. Sasa unaweza kuona.

**SPIKA:** Wapo wangapi Botswana?

**MHE. PAUL J. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, watu ni wachache kuliko sisi.

**SPIKA:** Milioni moja na laki nane.

**MHE. PAUL J. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, tunaelewa hilo, lakini ninachozungumzia hapa ni jinsi tunavyoweza kuzitumia vizuri rasilimali zetu. Ziko nchi ndogo, zina rasilimali za kutosha, lakini zimeshindwa kutumia vizuri rasilimali zao. Kwa hiyo, mimi ndipo hapo ninapogomba kwamba hatujatumia vizuri rasilimali

zetu. Pamoja na kwamba tunazo rasilimali za kutosha, lakini tungezitumia vizuri tungeweza kupiga hatua kama wenzetu wa Botswana, ambayo sasa hivi ni nchi ya uchumi wa kati kama ilivyo Uturuki, Mexico na nchi nyingine. Sasa hilo ndiyo wasiwasi wangu mkubwa ambao unanipa tatizo kwenye eneo hili la kupiga hatua za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Itigi tumegundua *uranium* na tumeambiwa hapa mara mbili, tatu na wataalam, kwamba maeneo hayo ya Wilaya ya Manyoni *uranium* imepatikana. Sasa naomba sana tuandae vizuri watu. Wilaya ya Manyoni ni kubwa, tumekuwa tukiomba sana kwamba tupewa kipaumbele kuigawa Wilaya hii ili Serikali iwe karibu zaidi ku-*honest resources* zake kwa ajili ya maendeleo ya wananchi, lakini imekuwa ngumu na sababu zimetolewa nyingi.

Mheshimiwa Spika, Mwenyezi Mungu ametujalia, ameshusha *uranium* na unaifahamu, ni madini muhimu katika kurutubisha silaha za nyuklia, na inasemekena kwamba sasa hivi kama itabainika kwamba wataweza wakayachimba, tutasafirisha nje *uranium* ghafi. Sasa katika utaratibu ni kwamba ni *yellow cake*. Sasa hii nadhani itatusaidia sana katika kukuza uchumi wa nchi hii. Lakini naomba Serikali, maeneo kama hayo ambayo yana *resources* kama hizo, basi yapewe kipaumbele katika kugawa keki ya Taifa hili vizuri.

Mheshimiwa Spika, mpango wa *D by D*, sisi bado tuna wasiwasi kwa sababu nchi hii imefanya majaribio mengi katika utaratibu huu wa *D by D*. Hii nadhani itakuwa kwenye utaratibu wa *D by D*, itakuwa ni

mpango wa nne kama sikosei ama wa tatu tangu tumepata uhuru. Tulivunja hizi Halmashauri baada ya kuzivunja, tukaja na utaratibu wa *decentralization*, madaraka Mikoani. Lakini utaratibu huu ukashindikana. Huu utaratibu wa *D by D* una maana kwamba, tunachukua pesa nyngi tunazipeleka kwenye Halmashauri zetu. Lakini namna ya kuzisimamia hizi fedha limekuwa tatizo kubwa. Wizi mkubwa ndiyo umekithiri na dada yangu mmoja hapa juzi, Mheshimiwa Lulida alitoa orodha ndefu ya watu wanaohujumu kwa makusudi na Serikali imekaa pale inawaangalia badala ya kuwachukulia hatua madhubuti, wamekuwa wakihamishwa.

Mheshimiwa Spika, hili lilinifanya mpaka niombe mwongozo hapa kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, nilidhani kwamba ametoa kauli yule ambaye ilimuudhi yule ambaye alitoa hiyo hoja, lakini hiyo ilikuwa ni jazba iliyonipata mimi, kwamba, kama wametajwa na wanafahamika, basi waanikwe badala ya kuhamishwa mara kituo hiki, au kituo hiki. Haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, niliona kuna umuhimu wa hao watu, tatizo letu siyo mipango, hata katika Jumuiya ya Afrika Mashariki sasa hivi wanassema sisi Tanzania ni mabingwa wa *ku-drop ideas*, halafu watu wa Kenya wana-*plan*, halafu watu wa Uganda wao wanatengeneza *action plan* halafu wanawaachia Wanyarwanda wana-*implement*. Hapo ndipo tatizo, lakini tatizo letu tuna mipango mizuri na mikakati mizuri, lakini wizi na uhujumu umezidi. Sasa naomba, kama mhalifu anafungwa, atajwe na jina na eneo analotoka na kabilal, basi. Kwanini iwe aibu kutaja mtu

anayehusika na kabilia lake na eneo analotoka ili tuweze kujua hawa watu wanaotuhujumu kiasi hiki tufanye nini? Tuwaweke kwenye hizi nafasi au tujue kwamba sasa hii nchi maana yake tatizo linazungumzwa, umoja wa kitaifa; umoja wa kitaifa ambao unaleta *imbalance*, katika hali hii, hatuwezi kuuvumilia.

Mheshimiwa Spika, naomba eneo hili lizingatiwe, vinginevyo tutaibiwa na mipango yetu haiwezi kwenda. Nasema kwamba ikiwezekana kama kuna eneo lenye miradi mingi kwa mfano eneo fulani, hizi ni *rumours* lakini huenda ikawa ni kweli, kwamba mtu anahamishwa kwa makusudi kwenda kusubiri pesa za huo mradi, akishaiba basi anahamishwa anakwenda sehemu nyingine. Hii hali ni ya kusikitisha.

Mheshimiwa Spika, alikuwepo adui ujinga, umaskini na maradhi, tumeshindwa kuwatokomeza, wote na wameungana hawa watu na wana Kamati Maalum na wame-*incorporate*, wamezaa maadui wengine, wizi, ubadhirifu na ufisadi. Sasa hatuwezi katika hali hii, hawa watu wamekuwa sugu! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi niungana na kaka yangu Mheshimiwa Missanga kwenye suala la maafa. Singida safari hii tumelima sana mtama, lakini mtama huu mwingi umeliwa na ndege. Tuliahidiwa kwamba kutakuwa na ndege maalum ya kuweza kunyunyizia kuwaua hawa ndege, lakini imeshindakana. Safari hii mtama mwingi na mazao haya ya ukame yamepunguzwa kwa kiasi kikubwa na ndege hawa wa kweleakwelias. Sasa tunaiomba Serikali pia kwamba

ingalie uwezekano wa kuwa na ndege yake badala ya kutegemea ndege kutoka sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, suala la njaa linafahamika sana na tumelizungumza sana kwenye Kamati. Hili suala siyo la mchezo na Serikali inaonekana katika eneo hili haijajipanga vizuri. Mimi sijaridhika na utaratibu wa kupeleka chakula katika maeneo ambayo yanakumbwa na janga hili la njaa. Watu wanaingia kwenye utaratibu wa *tender*, hizi ofisi za Halmashauri wakishaingia hizo *tender* inachukua hizo *tender* na hakuna kitu kingine, maana ni ya kupata watu wa kuja kuchukua chakula kama ni Dodoma ili kuweza kupeleka maeneo husika.

*(Hapa kengele ililia kushiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Basi, ahsante. Kengele ya pili.

**MHE. PAUL J. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo machache. Asubuhi niliwataja Madiwani 35 kutoka Kata zote za Jimbo la Handeni wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Handani, Mheshimiwa Ramadhani Diriwa. Waheshimiwa Madiwani karibuni sana. (*Makofi*)

Wakati mwingine tunakuwa na wageni wengi katika ukumbi wetu, basi nafasi yetu inakuwa haitoshi, lakini karibuni sana nadhani mtajifunza mengi.

Halafu nina tangazo lingine. Katibu wa Kamati wa Wabunge wote wa CCM, Mheshimiwa Jenista Mhagama anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM kuwa leo saa 7.00 mchana huu kutakuwa na kikao kitakachofanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Wote mnaombwa kuhudhuria. Asubuhi nilisema ukumbi ule ulikuwa unatumika na watu wengine, nadhani wataelewana wenyewe huko huko.

Tangazo lingine, Wabunge ambao hawajajaza Fomu za Vitambulisho vya Taifa wazijaze fomu hizo kwa Maafisa wa *NIDA* waliopo pale mapokezi kwenye jengo letu la Utawala. Tarehe ya mwisho kwa Maafisa hao ni kesho tarehe 29 Juni, 2012. Hivyo ili kuepeka usumbufu wa kuwafuata Maafisa hao *NIDA*, ni vyema Wabunge mkatumia nafasi mliyonayo. Kama kuna watu ambao wamejisahau, maana kuna wengine wanaweza kusema labda kesho, labda kesho. Kesho ndiyo *deadline*.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya wingi wa wachangiaji kwa kweli asiyekuwepo na lake halipo. Ni wale tu ambao wametoa taarifa, basi wale wataingia. Kwa sababu wachangiaji ni wengi, asiyekuwepo na lake halipo. Mimi nitaendelea na orodha nyingine.

Waheshimiwa Wabunge, sina tangazo lingine. Naomba nisitishe shughuli hizi mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.58 mchana Bunge liliisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipokuwa tunaondoka nilikuwa nimemwita Mheshimiwa Susan Kiwanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Joyce Mukya, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. David Malolle na atafuatia Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed.

**MHE. SUSAN L.A.KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, naenda moja kwa moja katika kuchangia hoja iliyoko mbele yetu ambayo ni Hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, mimi natokea Mkoa wa Morogoro na ni vizuri nikachangia kwa kujikita ndani ya Mkoa ambao ninaufahamu, niliozaliwa, niliokulia na ninaendelea kuishi. Mkoa wa Morogoro ni Mkoa ulio mkubwa kuliko Mikoa yote hapa Tanzania ambapo una eneo la kilometra za mraba sabini na tatu elfu na thelathini na tisa lakini vilevile ni asilimia 8.2 ya nchi yetu. Kwa hiyo, ukiangalia Mkoa wa Morogoro, ni Mkoa ambao ni mkubwa sana na unategemea kwamba bajeti zake zitalingana na Mkoa wenyewe jinsi ulivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini Mkoa wa Morogoro ni Mkoa wa wakulima na wafugaji, vilevile kuna wafanyabiashara na Mkoa wa Morogoro ni Mkoa wa viwanda hapo zamani lakini sasa hivi ni marehemu. Mkoa wa Morogoro Rais wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete mwaka 2006 alitangaza kule Bagamoyo kwamba ni Mkoa ambao ameuita kwamba ni Ghala la Chakula na Mkoa huohuo kwa tamko la Kunduchi kuhusu Kilimo Kwanza umepewa

kwa maneno kipaumbele ambapo tutaendesha Kilimo Kwanza, ukiangalia Mkoa wenyewe barabara zake ni matatizo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ukiangalia Mkoa wenyewe na inasemekana kwamba ni Kilimo Kwanza, hela zinazopangwa katika hicho Kilimo Kwanza ni vichekesho. Mwaka jana katika bajeti ya mwaka 2010/2011 tuliahidiwa kwamba kwa mfano Bonde la Kilombero litaanza uzalishaji mkubwa wa chakula katika kilimo cha mpunga na kilimo cha miwa pamoja na Wami lakini cha kushangaza hela iliyotengwa eti ni ya kufyeka tu. Kwa hiyo, mpaka sasa hata hiyo miradi katika mpango mzima wa kuzalisha chakula bado Wilaya ya Kilombero au Mkoa wa Morogoro kwa ujumla haujaonyesha picha halisi, haujaonyesha faida na haujaonyesha matokeo kwamba hili kweli ni Ghala la Chakula.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika majedwali tuliyopewa, Mkoa wa Morogoro, Wilaya ya Kilombero eti umepewa matrekta mawili makubwa (*power tiller*), hata moja hakuna jamani hicho ndicho Kilimo Kwanza? Hilo ndilo Ghala la Chakula? Hatuoni kama tunasema kwa maneno tu lakini kwa vitendo hatutekelezi? Ndiyo maana mfumuko wa bei umekuwa mkubwa ndani ya nchi yetu lakini Wilaya hiyohiyo ya Kilombero ndani ya Mkoa wa Morogoro kuna kilimo kikubwa sana cha mpunga. Katika Kata ya Mgeta ambapo wanasema *KPTL* (*Kilombero Planting Tanzania Limited*) ambapo inafanya kazi kubwa sana ya kulima, lakini katika Hotuba ya Waziri Mkuu inaonyesha katika ukurasa wa kumi na tisa, inasema kwamba hilo eneo

wakulima wadogo wanafaidika, uzalishaji unaongezeka, wanapewa pembejeo lakini hali halisi katika Tarafa ya Mgeta yenyе Kata tatu Chita, Mgeta na Mchombe hali halisi iliyoko pale kweli mwekezaji yupo na anazalisha kiasi cha kutosha, ametoa elimu kweli kwa vikundi mbalimbali katika hizo Kata lakini hali halisi mpaka sasa wakulima wanaambiwa mfuko mmoja wa mbolea ni shilingi laki moja na wakulima hawana uwezo wa kununua mbolea hiyo, matrekta hamna. Kwa hiyo, wakulima wadogo wanaozunguka ule mradi hawafaidiki, hali ni mbaya, vikundi vimepewa elimu kwani elimu ndiyo kulima? Zinatakiwa zana lakini ukiangalia hali halisi ya mgao wa mbolea katika nchi yetu, mwaka jana Mikoa mingi imelalamika mbolea hazifiki kwa wakati, ile yenyе ruzuku ya Serikali, kwa hiyo, wakulima wanashindwa kulima. Kweli ardhi ni nzuri lakini hakuna faida yoyote kwa wananchi wa kawaida katika kukaa Mgeta, katika zile Kata elimu wamepewa lakini uzalishaji haupo.

Mheshimiwa Spika, hiyo haitoshi, angalia barabara ya kutoka Ifakara mpaka Mgeta, ni mashimo matupu, barabara ya vumbi siyo ya changarawe. Cha kusikitisha katika Bunge hili, tarehe 11/7/2011, mimi nilimuuliza Waziri wa Ujenzi wa wakati huo kwamba barabara ya Kidatu- Ifakara na Ifakara - Mrimba mpaka Madeke mpakani mwa Njombe itatengenezwa lini kwa kiwango cha lami? Nikajibiwa vizuri kuwa kilometra kumi na saba zimeshajengwa kiwango lami na hizo zilizobaki zitawekwa kwa kiwango kwa changarawe lakini mpaka leo ninavyozungumza hamna changarawe wala mawemawe, kuna vumbi tupu wakati wa mvua zile barabara hazipitiki.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Tarafa ya Mgeta yenye Kata tatu wanalima, umeme hakuna, yule mwekezaji pale ana umeme anashindwa kuwasaidia wale wanaomzunguka kupata umeme. Kwa hiyo, hakuna mashine za kukobolea mpunga matokeo yake wakulima wanalima ila wakitaka kupeleka mpunga wao sokoni inabidi wakodi fuso kutoka Mgeta mpaka Ifakara kwa shilingi laki tano wakati ni kilometa themanini tu lakini mfanyabiashata akitoka Ifakara mpaka Dar es Salaam kwa fuso ambapo ni kilometa mia tano ni shilingi laki tano hiyohiyo. Kwa hiyo, hatuoni kuwa wananchi wa Wilaya ya Kilombero wanateseka sana, hawana faida na mpango mzima wa Kilimo Kwanza. Wananchi hawa hawawezi kuondoka katika umaskini kama barabara hakuna. Ni muhimu tunaposema kwa maneno tutekeleze kwa vitendo. Mwaka huu ningependa bajeti ionyeshe kwamba kweli Serikali ina nia ya kuboresha kilimo katika Bonde la Kilombero la sivyo tutakuwa tunaandika maneno vitabuni lakini hali halisi hakuna.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwenye huu ukurasa, sasa matokeo yake ni nini wanaposafirisha ule mpunga kwenda kukoboa mashine za Ifakara, ushuru wa Kijiji wanalipa shilingi elfu moja na mia tano, gunia moja wanagharamia shilingi elfu kumi na Halmashauri wanawa-*charge* shilingi elfu tatu. Mkulima anakuwa-*charged* kwenye geti la Idete, ndiyo maana geti la Idete ni maumivu sana kwa wakulima wa Wilaya ya Kilombero hususani katika Tarafa ya Mgeta, jamani ni kilio. Kuna Sheria ya mwaka 2002, Sheria Na.230, tamko lililotolewa na Brigedia Ngwilizi aliyekuwa Waziri wa

Serikali za Mitaa kwamba ushuru wa mazao umefutwa lakini leo mkulima anateseka kwa kulipia ushuru na siyo mfanyabiashara, anazalisha mpunga mwingi, mashine hakuna, umeme hakuna, anapeleka Ifakara, anakuwa *charged* kwenye geti la Idete, hiki ni kilio kikubwa. Naomba Waziri aje na majibu atawasaidia vipi wananchi wa Kilombero katika ushuru ambao unawatesa kila kukicha, atoe ufanuzi ni kwa nini Sheria zinakiukwa?

Mheshimiwa Spika, ukurasa huohuo wa kumi na tisa kuhusu wananchi wa Kilombero sukari wanafaidika, ametuambia wanafaidika. Mheshimiwa Waziri Mkuu hawafaidiki hata leo na jana wakulima wadogowadogo mashamba yao yameungua kwa bahati mbaya kwa uchomaji wa moto na yule wa kiwandani hataki kuvuna miwa yao na miwa hiyo ikikaa wiki moja inaharibika, wanapata hasara na hizi hasara miaka yote wanazipata. Kibaya zaidi, kule kiwandani wanakoenda kupima miwa hakuna mwakilishi ye yote yule, mwenye kiwanda ni jeuri hataki nini wala nini na haruhusu wakulima wawe na mwakilishi kupima miwa yao kwamba miwa inapatikana sukari kilo ngapi kwa hiyo, hiyo ni taabu.

Mheshimiwa Spika, lakini Halmashauri inakosa mapato, sukari ikizalishwa Kilombero inapelekwa Dar es Salaam halafu inarudi Kilombero, mtu wa Dar es Salaam ananunua bei ya chini na mtu wa Kilombero ananunua bei juu. Kwa hiyo, huyu mwananchi wa Kilombero anafaidika vipi na hicho killimo cha sukari? Kama tunataka kumnufaisha Mtanzania wa kawaida, ni bora tukaboresha miundombinu, tukaruhusu yule

mwekezaji wa *KPTL* awaruhusu *REA* na *REA* wako tayari kupeleka umeme kwa wananchi lakini yeye ni mjeuri, umeme wenyewe ni wa maji na maji ni yetu, hivi kiburi hiki anapata wapi? Hapa wananchi wa kawaida wataonaje kama uwekezaji una faida? Serikali lazima ichukue hatua. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa la wafugaji katika Wilaya ya Kilosa, mpaka leo ng'ombe wameuawa Parakuyo...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

**SPIKA:** Pole, muda umeisha. Sasa nitamwita Mheshimiwa Joyce Mukya, Mheshimiwa David Malolle, Mheshimiwa Profesa Kapuya na Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya wajiandae.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi hii na pia nashukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa pumzi na uhai mpaka sasa hivi. Katika bajeti hii ya Waziri Mkuu, mimi nitajikita katika sehemu tatu; huduma za jamii ambapo nitaongelea huduma ya afya katika Wilaya ya Ngorongoro, Mkoani Arusha, watumishi Wilaya ya Longido, Mkoani Arusha na msongamano wa magari katika Mkoa wa Arusha, Wilaya ya Arusha Mjini.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na msongamano wa magari katika Mkoa wa Arusha, Wilaya ya Arusha Mjini. Kwa wale ambao mmeshafika Arusha Mjini siku za hivi karibuni, mtakubaliana na mimi

kabisa kuwa msongamano wa magari umekuwa ni mkubwa sana na ni kero kubwa kwa wafanyakazi. Mikutano mingi ya Kitaifa inafanyika katika Mkoa ule, Arusha Mjini inajulikana kama kitovu cha utalii katika nchi hii ya Tanzania, watalii wamekuwa wakipata shida sana lakini sasa ninaiomba Serikali ichukue uamuzi wa busara kuweza kusimamia biashara nzima ya utalii kwa sababu tusipofanya hivyo, tunapoteza fedha za kigeni katika biashara hii.

**SPIKA:** Wanaomba uongee taratibu, wanashindwa kukuelewa, punguza *speed*.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Naomba kuingia katika huduma za jamii kuhusiana na suala zima la afya katika Wilaya ya Ngorongoro, sehemu ya Loliondo. Kumekuwa na shida kubwa ya huduma ya afya katika Wilaya ya Loliondo, wananchi wanapata shida sana, kuna Kituo cha Afya katika eneo la Loliondo ambacho ni cha zamani sana lakini kuna Hospitali ya Wilaya ambayo inamilikiwa na Kanisa Katoliki, Parokia ya Arusha Mjini ambayo inapata ruzuku kutoka Serikalini kama wahudumu, vifaa vya matibabu, dawa kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, wananchi wengi hutumia hospitali hiyo. Lakini kutoka katika hospitali hiyo, kuna Kituo kingine cha Afya katika sehemu inayoitwa Sakala. Kituo hicho kimejengwa katika miaka ya 2000, ni kikubwa sana lakini kutoka hapo kuelekea katika kijiji kinachoitwa Nani, katika Kata ya Unguselusambu hakuna Kituo cha Afya kabisa, wananchi wanapata shida sana kutokea katika Kituo cha Nani ambacho ni kijiji kuelekea katika Hospitali ya Wilaya ya Loliondo

hasa wanawake wajawazito kama unavyoelewa wanawake wajawazito wanatakiwa kwenda kliniki kila mwezi. Wanawake hawa hawaendi kliniki wanajifungua kwa kutumia Wakunga wa Jadi. Wajawazito hawa wanapata shida sana kwa sababu Kituo cha Afya kiko mbali. Katika kijiji cha Nani mwaka jana walikufa watoto kumi kutokana na ugonjwa wa Surua. Watoto hawa wamekufa kwa kuwa hawapati chanjo wakati wamezaliwa kwa kuwa mama zao wanajifungua kupitia Wakunga wa Jadi. Hili ni tatizo kubwa katika Wilaya ya Ngorongoro na wakazi wa pale wamelalamika sana kwa sababu ni tatizo lipo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejenga Kituo cha Afya katika eneo la Sakala wakati ni kilomita tano tu kutokea katika Hospitali ya Wilaya ya Loliondo ambayo inamilikiwa na Kanisa Katoliki. Kwa nini Serikali haikujenga Hospitali hiyo katika kijiji cha Nani, katika Kata ya Unguselusambu ambayo ingesaidia wananchi kutoka umbali wa kilomita sabini kuelekea katika hospitali hii ya Wilaya ya Loliondo, tatizo hili ni kubwa sana kwa wananchi wa Loliondo.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni uhaba wa Watumishi katika Wilaya za pembezoni, naongelea Wilaya ya Longido. Wilaya ya Longido imepata Wahasibu mwaka jana mwezi Septemba na mwezi Oktoba, watumishi hao wamekaa chini ya miezi sita katika kituo kile cha kazi na wameondoka katika mazingira ya kutatanisha. Mtumishi mmoja ambaye anaitwa somebody Mkonyi alitoroka na mpaka leo hakuna taarifa kuwa ameelekea sehemu gani na

mtumishi mwingine sikumbuki jina lake vizuri naweza nikaleta taarifa kwenye Meza yako, aliomba kuhamia Mkoa wa Tanga kupitia Katibu Tawala Mkoa wa Arusha lakini baada ya Mkuu wa Mkoa kuelekea katika Halmashauri ya Longido alipewa malalamiko haya na wakazi wa Halmashauri ya Longido na akamwomba RAS ambaye ni Mama Itanisa ampe maelezo kamili. Mama Itanisa akamwambia kuwa maelezo kamili ni kuwa ye ye hajatoa uhamisho wowote kwa mtumishi huyo lakini mtumishi huyu alimwomba ruhusa kuelekea Mkoa wa Tanga na ye ye akakataa lakini mtumishi huyu akapitia wafanyakazi wake wengine kwa njia ya mlango wa nyuma na akapata ruhusa hii na mtu ambaye amempa ruhusa hii anaitwa *somebody* Nkya ambaye ndiye ali- *sign* barua hii.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu hoja hizi atuambie Mheshimiwa huyu Nkya amechukuliwa hatua gani mpaka sasa hivi kwa sababu tukio hili ni la muda mrefu kidogo. Atuambie watumishi hawa kama bado wanapokea mishahara yao mpaka sasa na atuambie watumishi hawa wako wapi. Kwa sababu walipangia kazi katika Halmashauri ya Longido na Halmashauri ya Longido haina watumishi wa kutosha, Wahasibu, kwa sababu watumishi hawa wanakwepa kukaa vijijini na wakati watu wengine wanakaa vijijini kwani wao ni akina nani na kwa nini wasikae vijijini. Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amekuwa akitoa taarifa kila mwaka kuwa mabilioni ya pesa yanatumika kuwalipa watumishi hewa, watumishi ambao hawakai katika maeneo yao ya kazi, watumishi waliofariki, watumishi hawa wamekuwa wakichukua mishahara hii aidha

wanachukua au hawachukui lakini mishahara hii inaenda wapi? Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuwa anajibu hoja hizi aweze kusema suala hili limefikia wapi mpaka sasa hivi, ninashukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Hata mimi nilipokuwa ninaanza, nilikuwa nina *speed* ya kuongea. Sasa nimwite Mheshimiwa Dkt. David Mallole atafuatiwa na Mheshimiwa *Professor* Kapuya na pia atafuatiwa na Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya.

**MHE. DKT. DAVID M. MALOLE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza kabisa, naomba nizungumzie kuhusu kilimo cha zabibu. Tunashukuru sana kwamba mazao mengi yametiliwa umuhimu kama vile pamba, kahawa, chai na mengine mengi lakini kwa bahati mbaya, zao la zabibu halikuweza kuzungumziwa vya kutosha katika hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mimi napenda nitumie nafasi hii kumwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ajaribu kuliangalia suala hilo kwa karibu kwamba wananchi wetu siku za nyuma walijitahidi sana kulima zabibu na walipata moyo wa kuendelea kulima zabibu baada ya kuwa na kiwanda cha *DOWICO* ambacho bahati mbaya baada ya muda kilifungwa. Kipindi kile wakati kiwanda cha *DOWICO* kipo, maisha ya wananchi wa Dodoma yalibadilika sana. Kwanza watu walipata ajira lakini katika kuuza zile zabibu, watu walijikwamua na umaskini kwa kiwango kikubwa sana. Baada ya kile

kiwanda kufungwa, kilimo cha zabibu kikashuka. Tunashukuru kwa sasa hivi kwa kuwa kuna kiwanda cha *CETAWICO* kule Hombolo. Tunamshukuru Bwana Kato pia na ye ye ameanzisha kiwanda cha kununua zabibu lakini pia tunashukuru hata viwanda vilivyoko kule Bihawana pamoja na Miyuji.

Mheshimiwa Spika, viwanda hivi ni vidogovidogo, watu wamehamasika kulima sana zabibu lakini mwisho wa yote zabibu yao yote inakuwa haiwezi kununuliwa. Watu wanayumba hapa Mjini Dodoma kuuza zabibu zao kidogokidogo lakini hatimaye hawawezi kunufaika hata kidogo na sielewi zile ambazo wanashindwa kuuza wanazipeleka wapi. Tunaomba sana katika bajeti yako ujaribu kuliangalia hili kwa karibu, suala la kilimo cha zabibu na aidha kufufua kiwanda cha *DOWICO* na pengine labda kuanzisha viwanda vingine vidogovidogo hasa kwenye maeneo ambako zabibu zinalimwa sana kama vile Mbabala, Mpunguzi, Makutopora na maeneo mengine mengi katika mji wa Dodoma. Hali hii itasaidia kupunguza tatizo la ajira lakini pia watu wetu watauzza zabibu zao na wanaweza kupata nafasi kubwa sana ya kuweza kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, la pili, naomba nizungumzie habari ya matrekta. Tunashukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kupunguza bei ya matrekta kutoka shilingi milioni ishirini na tano mpaka shilingi milioni kumi na sita kwa yale yenye *horsepower* hamsini na kutoka kwenye shilingi milioni arobaini na tano kwenda kwenye shilingi milioni thelathini na nane *point* nane kwa yale yenye *horsepower* sabini. Hata hivyo, bei ya matrekta haya

bado ni kubwa sana. Ni vigumu sana kuweza kupata wananchi ambao wanaweza kununua matrekta haya kwa bei hiyo.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi ninazo Kata 37 na vijiji visivyopungua pia 39, katika Vijiji vile 39 hata kama tungesema tufanye uchambuzi sijui tutapata watu wangapi watakaokuwa na uwezo wa kununua hata lile trekta lenye *horsepower* hamsini, labda katika vijiji vyote 39 wanaweza wakapatikana watu wawili au watatu. Matrekta yatabaki, halafu hata mapinduzi ya kilimo tunayoyazungumzia itakuwa ni vigumu sana kuyafikia. Naiomba sana Ofisi ya Waziri Mkuu na Waziri Mkuu yupo hapa anatusikiliza, ajaribu kuangalia jinsi matrekta haya yatakavyoweza kupelekwa kwa wananchi ili waweze kuyatumia na kuleta mapinduzi ya kilimo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Dodoma tunalima sana uwele, kampuni ya *Tanzania Breweries* inahitaji sana mtama. Nashauri kwa upande wa Dodoma, matrekta hayo yangepelekwa kila kijiji yalime halafu baada ya kutoka hapo wananchi watakapokuwa wamevuna chakula chao, kila ekari moja mtu achangie debe moja, kama ana ekari mbili, madebe mawili na kama ni ekari tano madebe matano kutegemeana na ukubwa wa shamba lake. Ninaimani kabisa kwamba mtama huo Serikali itawauzia kampuni ya *Tanzania Breweries*, mtapata pesa na baada ya misimu miwili, mitatu, ninaimani kabisa kwamba deni lenu lote la shilingi milioni kumi na sita litakuwa limekwishalipwa. Hiyo itasaidia sana kuleta mapinduzi ya kilimo katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu nakwenda kwenye mabwawa. Dodoma ni eneo kame, hii hatuna haja ya kuijadili sana. Mwaka jana kwa mfano Dodoma imepata mvua kwa muda wa siku 14 tu. Tunaomba sana na kwa sababu mji unakua, Vyuo Vikuu vingi, *UDOM*, Chuo Kikuu cha St. Johns hata Chuo cha Madini, Chuo cha Mipango tayari wameshaanza kutoa Digrii na Chuo cha *CBE* na zipo shule nyingi sana za Sekondari za mabweni ambazo zinahitaji mbogamboga. Tunayo mabwawa 20 kwenye Jimbo la Dodoma Mjini, kama yote yale yangechimbiliwa vizuri, baadaye mvua zinapokuja zikajaza maji, itaimarisha kilimo cha mbogamboga kama nyanya, mchicha, kabichi na mbogamboga zingine ambazo hatimaye zinaweza zikauzwa katika vyuo vyetu mbalimbali na Mji wa Dodoma ambao unaendelea kukua kwa kasi. Nashukuru kwamba mlishatenga pesa kipindi kilichopita katika mabwawa fulani kama vile Vikonje, ambako mlipeleka kama shilingi milioni 400 lakini bado kuna milioni 200, mpaka dakika hii bwawa lile halijaanza kutengenezwa. Mabwawa ya Makutupora, tumeambiwa kwamba tayari yataanza kutengenezwa, Mbalawala na maeneo mengine lakini mpaka dakika hii kazi hiyo haijaanza. Naomba mabwawa haya 21, hebu myafanyie kazi kutokana na hali ya ukame wa mji wetu wa Dodoma na moja kwa moja hata maeneo yale ambayo mliyokuwa mmeahidi kwamba mtapeleka pesa muanze kupeleka. Baada ya hapa, mimi nilikuwa natarajia nianze ziara nyingine mpya, nitakapokuwa nimefika kwenye mabwawa hayo sijui nitajibu nini wakati niliwaambia kwamba hayo mabwawa

yanapanuliwa lakini mpaka leo hakuna kazi yoyote ambayo tayari imeshaanza.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie kwa kifupi pia kuhusu suala la maji vijiji. Naishukuru sana Serikali inajitahidi sana kupeleka miradi ya maji lakini labda tuweke utaratibu wa kufuatilia kama miradi hiyo ya maji inafanya kazi. Mimi ninazo Kata 37 kwenye Kata 37 miradi ya maji ilishapelekwa kwenye Kata zipatazo 35 lakini mpaka dakika hii maji yanapatikana kama kwenye Kata 18, zilizobaki mitambo ilishakufa na haifanyi kazi. Ni sawasawa na kusema kwamba robo tatu ya Jimbo la Dodoma halina maji safi na salama ya kunywa. Naomba utaratibu huo ufuatiliwe ama pia fedha za bajeti ya maji ziongezwe ili kusudi mitambo yote iliyoharibika iweze kukarabitiwa na watu waweze kuendelea kupata maji ya kunywa safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine liko kwenye Benki ya Dunia, tunawashukuru kwamba wao wanatupatia msaada sana wa maji, lakini masharti yaliyopo ya kwamba wanatakiwa wananchi kuchangia asilimia 2.5, inaonekana kiasi hiki ni kidogo kusema asilimia 2.5, lakini pesa wanazotoa ni mamillioni na mabillioni ya pesa, wananchi wanashindwa kutoa hiyo asilimia 2.5. Hivi kwa nini maji yasingeweza kupelekwa kule, watu wakapewa na baada ya hapo maji yatakapokuwa yamefika, kila anayekwenda kuchota ndoo ya maji akachajiwa pesa kidogo ili mwisho wa yote ile asilimia 2.5 itapatikana na moja kwa moja itapelekwa kunakotakiwa.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sijamaliza hotuba yangu kama wananchi wa Dodoma hawatasikia nikiongelea kuhusu *CDA*. Naomba sasa nizungumzie kidogo kuhusu barabara pamoja na masuala ya *CDA*. Nashukuru barabara zimeanza kukwanguliwa, naomba barabara hizi zitengenezwe katika kiwango kinachotakiwa na ziweze ku-cover mji wote wa Dodoma, zisifanywe kiubaguzi. Maeneo mengi katika Mji wa Dodoma bado barabara hizi hazijafika, naomba zifike kote kwa sababu mabilioni ya pesa yaliyotengwa ni mengi mno.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba hata zile barabara za lami kwa mfano *Area C*, *Area D*, maeneo yote ya kuelekea Soko la Majengo na maeneo mengine, tusiweke virakaviraka katika Mji Mkuu wa Serikali. Lami yote iliyochakaa ifumuliwe kabisa na lami mpya iwekwe ili Mji wa Dodoma upate kupendeza.

Mheshimiwa Spika, nimalizie habari ya *CDA*. Mwaka jana nilichangia kuhusu mahusiano na *CDA*, nataka niwahakikishie wananchi wangu kwamba Serikali imesikiliza suala hili. Sasa hivi Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa wameshatambua kabisa upungufu mwingi uliopo *CDA*, Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Lukuvi amefanya kazi kubwa sana kuisahihisha *CDA* na sasa hivi ina mwelekeo mzuri. Wananchi wa Dodoma mttagawiwa viwanja vyote vilivyopo hapa ambavyo vilikuwa vimefungiwa toka mwaka 2008, sasa vitagawiwa na ninyi mtapewa. Kwa hiyo, nataka niseme watu wa Nzunguni na maeneo mengine yote yaliyopo hapa ambayo mlikuwa mmeweka msimamo kabisa kwamba hamtaki

kuonewa, sasa acheni waje wapime, mtapewa viwanja kama kawaida na hakuna atakayenyimwa na wale wengine wote wananchi mliopo hapa mliokuwa mnaomba viwanja pamoja na Misikiti na Makanisa mbalimbali pamoja na Waheshimiwa Mawaziri na Wabunge mliopita kwangu ambao mpaka dakika hii viwanja vilikuwa bado vimekaliwa, sasa mtagawiwa na wote mtapewa. Nataka niseme kwamba Mheshimiwa Lukuvi amesisitiza kabisa kwamba kuwe na utaratibu mzuri ikiwezekana hata litumike boksi kubwa la kuweka mle ndani na watu waje wapate kwa kura ili mtu asinyimwe. Nashukuru sana katika hili na naunga mkono hoja ya Waziri Mkuu, ananipenda na nitazunguka naye hapa Dodoma Mjini muweze kuona kwamba tupo pamoja. (*Kicheko/Makofi*)

**SPIKA:** Asije akawadanganya, mnagawiwa bure? Hamna bure siku hizi. Haya tunaendelea na Profesa Kapuya atafuatiwa na Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya na Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed ajiandae.

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA:** Mheshimiwa Spika, nianze na shukrani. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia kuwepo hapa leo kuweza kusimama na kuzungumza mbele ya Bunge hili. Pili nakushukuru Spika kwa kunipa nafasi. Tatu, nawashukuru sana wananchi wa Urambo Magharibi kwa kuniwezesha kuwa hapa baada ya kunichagua mwaka 2010, nashukuru vile vile kwa Wilaya ya Kaliua kuzaliwa.

Mheshimiwa Spika, kuzaliwa kwa Wilaya ya Kaliua kumenifundisha mambo mengi sana. Jambo la kwanza

ni kwamba kumbe ndiyo maana wahenga walisema mkulima ni mmoja lakini akiivisha walaji ni wengi, leo kuna mtu alisimama hapa akazungumza habari za Kaliua. Nashukuru kuzaliwa kwa Kaliua, lakini kama kulikuwa na wapingaji yeye alikuwa ni mmojawapo katika watu waliokuwa wakipinga sana kuzaliwa kwa Wilaya ya Kaliua, leo anashukuru na mimi nashukuru sana. (*Makofi*)

Mhehsimiwa Spika, namshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu yeye kwa kweli ndiye alipanga kipaumbele. Nimshukuru Waziri Mkuu alihangaika sana kuhakikisha kwamba Wilaya ya Kaliua inazaliwa. Nawashukuru Mawaziri wote wa TAMISEMI waliopitia katika Wizara ile na nikiwataja kwa majina ni Mheshimiwa Kombani, Mheshimiwa Mkuchika, Mheshimiwa Mwanri wote wale wanajua jinsi ambavyo walikuwa wakinisaidia kuhakikisha kwamba Wilaya ya Kaliua inazaliwa.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mkuu wetu wa Mkoa wa zamani, Mheshimiwa Mwinyimsa kupitia RCC zilivyokuwa ngumu lakini alihakikisha kwamba ajenda inakwenda mbele. Nawashukuru sana wananchi wa Urambo Magharibi kwa jinsi tulivyoshikamana, nawashukuru wananchi wa Urambo Mashariki kwa jinsi walivyokuwa tayari kuizaa Wilaya ya Kaliua.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, naomba sasa nijikite katika habari za Wilaya hii mpya. Waziri Mkuu, Wilaya inayozaliwa ni sawasawa na mtoto mdogo aliyezaliwa. Mtoto mdogo anapozaliwa katika

familia, familia ile huwa inahakikisha kwamba mtoto wao anapewa chakula ili aweze kukua bila kwashakoo. Naomba Waziri Mkuu Wilaya hii mpya sasa ya Kaliua rasilimali ziwekezwe huko ili kuhakikisha kwamba kweli inaanza vizuri.

Mheshimiwa Spika, nataka nikuhakikishie kwamba kama tukianza vizuri, sisi suala la njaa katika Wilaya ile mpya ya Kaliua halitakuwepo. Tumeshapoteza miaka miwili katika kusubiri uundwaji wa Serikali ya Wilaya, sasa tunaomba Halmashauri isichelewe kuanza kwa sababu kama mnavyojua mtekelezaji mkuu wa llani ambayo ndiyo llani ya CCM ni Halmashauri. Tunaomba ututajie Halmashauri yetu mapema na Mkurugenzi aletwe mapema pale kuhakikisha kwamba kazi zinaanza vizuri.

Mheshimiwa Spika, Wilaya hii ni kubwa, ina kilomita za mraba 16,000. Kwa hiyo, wananchi wake wanahitaji kufika katika Makao Makuu ya Wilaya na ili wafike tunahitaji barabara, hasa barabara ya kuelekea Ugala ambako tunapakana na Waziri Mkuu, kule hakuna barabara kabisa, masika wanakuwa kama wamefungiwa kabisa. Vilevile Waziri Mkuu barabara nyngine inaelekea kaskazini ambayo ndiyo inakwenda Uyoa, Makasi, Kashishi mpaka kufika Kahama kule. Hizi barabara zikitengenezwa, zitafungua uchumi wa wananchi hawa. Madhumuni ya kupata Wilaya mpya ni kuhakikisha kwamba tunasogeza huduma kwa wananchi, hatusogezi huduma kama barabara hizi hazijatengenezwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutangazwa kuwa tumekuwa Wilaya ilikuja Tume ya watalaam kutoka *REA*, wamefanya *survey* kubwa sana, wametuahidi kwamba tutapata umeme, lakini hizi zimebaki kuwa ni ahadi kama ripoti tu. Naomba Waziri Mkuu utekelezaji sasa uharakishwe sana. Kuna umeme tunaoupata wa *phase* moja unatokea Urambo mpaka Kaliua, lakini utashangaa unapita katika vijiji vya Isanjandunu, Kijiji cha Isimbi unapita wima tu, sasa wananchi wanashangaa hivi sisi tumepita hapa kama barabara tu? Kwa heshima, naomba vijiji hivi sasa katika umeme ule ambao upo, kazi hii ianze ya kutupatia umeme lakini viro vijiji vingine ambavyo nitamkabidhi Waziri wa Nishati ili aweze kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, katika suala la uwezeshaji wananchi, nikisoma kitabu hiki cha hotuba yako Waziri Mkuu umezungumzia kwamba mifuko ya uwezeshaji wananchi ambayo inaongozwa na Baraza la Uchumi la Taifa ndiyo ambayo kama mhimili mkuu na viunganishi ni *SACCOS*. Kuna *microfinance Institution* moja inaitwa SCULT, wananchi wa Kanoge walichanga kupitia *SACCOS* yao shilingi milioni 27, mwaka wa tatu huu hawajapata chochote. Nimezungumza na mtu wa SCULT ananijibu majibu ya ovyoovyo tu, bahati nzuri nilishazungumza na Mheshimiwa Nagu amenihakikishia kwamba atamwita hapa aje kuhakikisha kwamba tunafikia *solution*. Mambo kama haya yanawavunja moyo wananchi.

Mheshimiwa Spika, *TASAF*, kipo Kijiji kinaitwa Kazanaupate katika Kata ya Igadala...

## **MBUNGE FULANI: Kinaitwaje?**

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA:** Kinaitwa Kazanaupate, tulibuni mradi mwaka 2006/2007 wa ujenzi wa shule kwa jumla ya shilingi milioni 34, Serikali ichangie shilingi milioni 29 sisi wananchi tuchangie shilingi milioni sita (6). Wananchi walifyatua tofali, tuko tayari kuchota, mpaka leo hatujapata hata senti moja kutoka *TASAF*, ukiuliza unaambiwa ilikuwa *TASAF I*, *TASAF II* imekwisha sasa tunahitaji *TASAF II* na *TASAF III* nayo inakwisha tunaingia *TASAF III*. Waziri Mkuu naomba hawa wananchi wasipuuzwe kwa sababu itakuwa kazi ngumu sana kwenda kuwashawishi tena kuchangia katika mambo ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo, kilimo ndiyo uti wa mgongo, sehemu zingine mnasema asilimia themanini kwa Kaliua ni asilimia 99 shughuli zetu zote zinajikita pale na kilimo chetu kikubwa sisi ni tumbaku. Tunalo tatizo na wawekezaji hawa wa tumbaku. Wamechukua nafasi wakawa wanatupangia hata ni nani alime na nani asilime. Kila mwaka vijana wanamaliza darasa la saba na wanamaliza *form four* wanapotaka kulima, wanakatazwa mpaka Mzungu akubali, sasa unashangaa tutawezaje kuingia maisha bora kwa kila Mtanzania? Mwaka juzi tulizalisha tumbaku nyingi sana, wakakataa kuinunua, wakasema ni nyingi mno, mlipowabana wakasema tutanunua yote lakini wakateremsha bei ili kwa fedha zilezile waweze kununua tumbaku ileile. Hii kwetu haitusaidii kabisa. Naomba tusaidiwe kwa Serikali kuingia katika mazungumzo na nchi nyingine kama Uturuki, China na

kadhalika ili kuhakikisha kwamba wanunuzi wa tumbaku wanaongezeka.

Mheshimiwa Spika, zao lingine tunalolima sisi ni mahindi, inawezekana hatupo katika *the big four* lakini nataka nikuhakikishie kwa mvua tulizonazo sisi tunalima mahindi ya kutosha na ukizingatia na kanuni za kilimo kwanza tumeweza kuzalisha mahindi mengi sana. Lakini sasa ikaja sera ya kukataza kuza mahindi haya nje ya Wilaya, ilituathiri sana. Kwa hiyo, naomba Waziri Mkuu, sera hii ya kusema kwamba mahindi yazuiliwe kuuzwa kwa sababu sisi kweli wapo wanaolima tumbaku na wapo wanaolima mahindi kama zao la biashara, mnapowakataza inaleta balaa, wanashindwa kusomesha watoto wao, wanashindwa kupelekwa wagonjwa wao hospitali. Naomba sana Waziri Mkuu hili lizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la maji, limezungumzwa sana suala la *World Bank* hapa, sisi tuna vijiji vitatu pale Kaliua Mashariki, Kaliua Magharibi na Ushokora. Tulipata mradi wa *World Bank* lakini tumechimba visima 12, vitatu ndiyo vyenye maji. Sasa mkataba tunaowekewa tunaambiwa kwamba atakuja kuchimba visima 12, alipochimba 12 vitatu vina maji tisa havina maji akasema, mimi tayari, sasa tofauti ni *definition*. Kwa mwananchi wa kawaida kisima ni kile chenye maji, ye ye anasema nimeshakuchimbia mashimo yako kumi na mbili shauri yako, sasa inakuwa matatizo makubwa. Itatupatia matatizo makubwa sisi kuwachangisha tena milioni tano katika miradi mingine ambayo mtakuja kutuletea. Waziri Mkuu, tusaidie ili tufikie *solution* hapo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hifadhi, suala la hifadhi sisi ni tatizo kubwa sana. Kuna baadhi ya wanasiaya wanatumia hili kama mtaji wa kupatia kura. Wanawashawishi wananchi, wanakuja kuhamia mahali pale na wanaingia katika hifadhi, ukienda utakuta katika hifadhi zetu zote asilimia 99 ni kabila moja, asilimia 99 kazi ni moja, asilimia 99 wote Chama kimoja, unashangaa, Waziri Mkuu tusiruhusu mambo ya namna hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, katika bajeti mama ambayo Waziri wa Fedha alipitisha, tutaajiri wafanyakazi wapya 71,000, naomba asilimia kubwa iwe wafanyakazi wa Wizara ya Afya maana tuna matatizo katika zahanati zetu. Tuna sera ya kuanzisha vituo vya Afya, watatushangaa wananchi hawa tunaanza kujenga vituo vya afya kabla zahanati hazijajaa watumishi. Nakushukuru sana, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Rukia Ahmed na Mheshimiwa Moza Abedi wajiandae.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi angalau niweze kuchangia kidogo katika hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya nimeweza kusimama hapa ili niweze na mimi kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, nitaanza na usafiri wa reli. Kama unavyofahamu, Kigoma tuna matatizo sana ya usafiri, kuanzia usafiri wa anga, barabara zenyewe ndiyo hivyo hatuna. Kwa hiyo, tunategemea reli kwa kiasi kikubwa na ndiyo usafiri rahisi ambao Watanzania wengi wanaweza kuutumia hasa wa kutoka kwetu Kigoma.

Mheshimiwa Spika, nitaanza na treni yenewe, mabehewa kwa kweli yanasicitisha, yamechakaa mno, vyoo vyenewe ni vichafu, hakuna vioo kwenye madirisha, watu wanasafiri mchana vumbi lao, usiku baridi yao, kwa kweli ni usafiri ambao hauna staha. Viti vimechakaa, hakuna hata sponchi, mende, kunguni, kwa kweli ni usafiri wa ajabu sana. Napenda kujuua hivi tunahitaji mtaji kiasi gani kuweka tu sponchi kwenye vile viti, kusafisha yale mabehewa, kwa kufanya hata *fumigation*, inasikitisha mno kwa kweli. Usiende ukapanda ile treni hasa *second class* ambayo ni kukaa, utajionea maajabu. Naomba sana kama Waziri anayehusika hajalionna hili akaangalie tena. Nimeshawahi kumwona mara nyingi kwenye treni lakini sijaona akilisemea hili. Uchafu, kwa kweli mabehewa ni machafu mno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni tiketi, upatikanaji wa tiketi ni mgumu, nashindwa kuelewa. Naomba Waziri Mkuu kama Waziri wa sekta, nalo hili hajalionna, ulisemee wewe. Kwa mfano Kigoma watu wanatakiwa kukata tiketi siku hiyohiyo ya safari. Sasa wanatoka Kibondo, wanatoka Kasulu na maeneo mengine ya Mkoa kwa mfano treni ni siku ya Alhamis na siku ya Jumapili, wanalala pale, kama mtu anataka

kusafiri Alhamis, anaondoka kwake siku ya Jumatano, anakuja kulala stesheni ili alfajiri awahi kupata tiketi, matokeo yake sasa bei inakuwa ya kuruka, tiketi ni shilingi elfu kumi na tisa, mtu kama ana uwezo wa kutoa pesa kidogo ili asipange foleni, anawatumia walewale wafanyakazi wa pale stesheni, wanalipa tiketi mpaka shilingi 35,000, mimi sidhani hapo kama tunamsaidia Mtanzania, tunazidi kumrudisha nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kujua huyo aliyetoa hilo agizo ni nani kwani ni Quran au Biblia haiwezi kubadilishwa? Ninaomba utaratibu wa zamani urejeshwe. Tulikuwa tunakata tiketi kama unajua utasafiri wiki ijayo, mwisho wa mwezi umepata hela yako unaenda kukata tiketi tarehe fulani nitasafiri, siku ikifika unakwenda unasafiri kwa staha lakini sasa hivi watoto, akina mama wazee, wagonjwa wanalala pale stesheni kuhakikisha kwamba labda kesho yake watapata tiketi na ikitokea kama Jumatano hawakupata, kwa hiyo, maana yake Alhamis hatasafiri, wakati mwingine hawezi kurudi kwake Kibondo au Kasulu au maeneo mengine analala pale tena mpaka siku ya Jumamosi ili Jumapili aamkie pale aweze kupata tiketi, sasa mazingira ya stesheni pia yanakuwa mabaya, machafu. Kwa kweli tunaomba tubadilishiwe utaratibu, huu hautufai hata kidogo na sisi ni watu wastaarabu tunahitaji ustaarabu.

Mheshimiwa Spika, nitaongelea vilevile suala la maji, inasikitisha tunalo Ziwa Tanganyika lakini tunapata maji mara moja kwa wiki. Kama iliwezekana zamani watu walipata maji kila siku, inakuwaje sasa hivi

tushindwe? Nakumbuka Bunge la Tisa niliwahi kuongelea suala hili, nikajibiwa kwamba matatizo ni ya umeme, kwa hiyo pampu haiwezi kusukuma maji na wananchi wakaweza kupata na ndiyo maana watu walikuwa wanapata maji mara moja moja, lakini sasa hivi umeme upo, hata kama ni wa mgawo lakini angalau upo siyo kama zamani. Naomba kujua sababu ya msingi hasa ni nini?

Mheshimiwa Spika, majibu mengine ambayo yalikuwa yakinolewa ni kwamba mabomba ni chakavu, miundombinu ya mabomba inabadilishwa, kwa hiyo sasa hivi watu wataanza kupata maji safi na salama, lakini mpaka leo maji bado hayatoki, ukienda Gungu, ukienda Kisangani, ukienda Ujiji, na maeneo yote kwa kweli yanasisitisha maji hayapatikani. Vijana wenye nguvu ndiyo wamejajiri sasa wanaenda ziwani wanachota maji, wanawauzia watu, inategemea na umbali, dumu shilingi mia tano mpaka wakati mwingine 1500. Mimi naona hii siyo sawa kwa kweli. Maisha yenye magumu, mfumuko wa bei na kule kwetu kulivyo mbali mpaka kitu kifike, sementi tunanunua mpaka shilingi 25,000 mafuta ya petroli tunanunua mpaka shilingi 2600, 2700 na kuendelea, kwa hiyo maisha yetu yanazidi kuwa magumu, naomba mturahisishie kwa kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kujua ni lini tutapata maji safi na salama, kwa vile hili ni tatizo kubwa kwetu. Napenda tu niwaambie Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kama mtaendelea kuacha kero nyingi ziendelee kututawala wananchi wa Mkoa wa Kigoma, kama kuvamiwa, tunakamatwa kama siyo

raia na mengine mengi, inawezekana hata hayo Majimbo matatu yaliyobakia msiyapate tena, yote yaingie upinzani kwa sababu tumechoka, tuna ahadi nyingi lakini hazitekelezwi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niende tena kwa upande mwingine wa afya, tuna matatizo sana ya watumishi. Najua hili ni tatizo lipo nchi nzima lakini siwezi kuacha kulisemea kwa kweli tuna matatizo. Nikitolea mfano tu tunaye Daktari Bingwa mmoja wa watoto Mkoa mzima na anatumika kwa Wilaya zote ambazo tunazo za Kasulu, Manyovu, Kibondo, Kigoma Manispaa na maeneo mengine, tunamtegemea huyo Daktari Bingwa mmoja wa watoto na bingwa mmoja wa wanawake. Nikichukulia mfano mmoja mdogo wa Wilaya ya Uvinza na Wilaya ya Kigoma, kuna mahitaji ya watumishi wa afya 559, tunao 255 peke yake. Kwa hiyo, upungufu hapa ni kama 307. Katika hao *Clinical Officers* wanaohitajika ni 112 na *Nurse Midwife* ni 113. Kwa hiyo, tunaomba sana utaratibu wa kupanga watumishi ukifika, mtuangalie kwa jicho la huruma. Mlimsikia hata Mheshimiwa Buyogera hapa alielezea Kasulu hali ilivyo, tunahitaji sana watumishi katika ngazi hiyo ya afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile Hospitali ya Mkoa imeelemewa mno kwa sababu Hospitali kwa mfano Wilaya ya Kigoma na Uvinza ambayo tulikuwa tunaitegemea haijakamilika. Kwa hiyo, maana yake wagonjwa wa maeneo yote hayo wanatakiwa waende wakatibiwa katika Hospitali ya Mkoa ambayo kwa kweli hali yake nayo ni duni kwa sababu imeelemewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikienda upande mwingine wa elimu. Nkiangalia tu shule za msingi bado mazingira yake ni magumu mno, watoto wanajifunzia chini, madarasa mengine wengine wanasoma chini ya miti, hali siyo nzuri kwa kifupi. Matokeo yake ndio maana wanafunzi wanakuja kumaliza darasa la saba hawajui kusoma wala kuandika. Ni kwamba mazingira yenyewe ni mabaya. Wanafundishwa Tehama kwa kuchorewachorewa *computer* kwenye ubao, wataionaje wakati maeneo mengine kwanza hata umeme hakuna? Mimi naomba tufundishwe vitu vnavyoendana na mazingira yetu vilevile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini tunao upungufu mkubwa pia Walimu, mbali na hayo madawati, vitabu, sijui na vitu vingine, tuna upungufu mkubwa sana wa Walimu. Nimechukua tu kesi *study* ya Wilaya ya Kigoma ambayo ni Uvinza na Kigoma yenyewe, tuna upungufu wa Walimu wa shule za msingi kama 600. Kwa kweli mkipanga Walimu mkumbuke Mkoa wetu. Mazingira yetu ni mazuri, naamini wanaweza tu wakaja. Vilevile na Serikali iangalie uwezekano wa kuboresha mazingira ya kufundishia Walimu, iongeze hizo posho ili kuhakikisha kwamba Walimu wanaokwenda kwenye mazingira magumu waweze kuona wako sawasawa na Walimu wengine ambao wanafundisha mjini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naenda katika kilimo cha mchikichi. Ukurasa wa 18 na 19 wa Hotuba hii ya Bajeti, nimeona Waziri Mkuu ameongelea mazao mengine kama korosho, kahawa, pamba, sijui kwa nini mchikichi hajaona kama ni zao muhimu. Nakumbuka miaka ya

1960 katika kusomasoma, niligundua kwamba watu wa Malaysia walikuja hapa Tanzania kujifunza juu ya zao hili, sasa hivi zao hili ni zao kuu kwao na wanalilima katika mtindo wa kisasa. Sasa nashindwa kuelewa kwa sababu mafuta haya ni mazuri sana kiafya, yana vitamini nyingi, hayana *cholesterol*, kwa nini zao hili lisiboreshwe tukaanzia labda na wale wakulima wadogowadogo wakawezeshwa kufanya kilimo cha kisasa?

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna Gereza moja linaitwa Kwitanga wanalima sana mchikichi, wanazalisha kwa kiasi kikubwa sana. Mimi naomba Serikali basi ianzie hapo kuwa-*support* pamoja na kwamba nguvu kazi inayotumika pale ni ya wafungwa lakini pia kile ni Chuo cha Mafunzo siyo lazima kwamba nguvu zao ziendelee kutumika tu siku zote. Tunaweza tukawapelekea mafunzo, wakaweza kulima kilimo cha mawese cha kisasa. Vilevile Serikali ikaangalia uwezekano wa kuwakopesha matrekta ambayo yamewekwa pale, ya Mwenge na mengine yamewekwa pale kinachoitwa Kilimo Kwanza, waweze kukopeshwa ili waweze kuzalisha zaidi. Mimi nafikiri ni muhimu sana kuongeza uzalishaji wa mafuta nchini kwa sababu tuna mahitaji makubwa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.  
(*Makofii*)

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja hii katika Bunge lako Tukufu. Kabla ya kuchangia, naomba niseme kitu kidogo, katika Kitabu

cha Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, ukurasa wa 33 alisema kuwa CCM na Washirika wake wanakishutumu Chama kimoja ambacho ni makini kwa kusema kuwa chama hicho ni cha Kidini, Ukabila na Ukanda. Lakini napenda niseme kwamba Washirika wa CCM, nadhani kwa muono wangu mimi ninavyoona ni Mawaziri, Manaibu Waziri pamoja na Manaibu Waziri Kivuli. Nadhani hawa ndio Washirika wa CCM. Au tukiacha hilo kwa muono wangu basi Washirika wa CCM ni sote tulimo katika mjengo huu kwa sababu tunafanya mambo kwa pamoja kwa maslahi ya nchi yetu na kwa maslahi ya vizazi vyetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, naomba sasa niende kwenye hoja. Nataka nielezee ni kitu gani kinachowafanya Watanzania wakose imani na Serikali hii sikivu. Wakati tunapokuja hapa katika Bunge la Bajeti, Watanzania wote wanakuwa katika vyombo vyaa habari kusikiliza ni nini Serikali inawaambia na ambacho Serikali inategemea kuwafanyia. Watanzania hawa hujenga matumaini kwa lile ambalo wanalisikia katika vyombo vyaa habari. Katika kipindi cha Bajeti cha mwaka 2011/2012, Serikali wakati wa kuwasilisha bajeti yake wallsema wataongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo. Watanzania walijenga matumaini na wakaona kwamba hili litawafanya waondokane na hali ngumu ya maisha waliyonayo. Katika kipindi chote kile cha mwaka 2011/2012 nadhani hakuna kilichoongezeka isipokuwa hali ya maisha inazidi kuwa ngumu kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha bajeti hichohicho cha mwaka 2011/2012, Serikali iliahidi kuwa itaweza kushughulikia suala la wafanyakazi hewa. Wananchi wote walijenga matumaini, Watanzania wakasema sasa Serikali imeamua na watashughulikia suala hili la wafanyakazi hewa na fedha ambazo ni za Serikali zinazovuza zikienda katika mikono ya walaji hao zitapatikana na zitakwenda kuendeleza shughuli ya maendeleo katika nchi yetu. Matokeo yake hatukuweza kuliskia suala hili, Mheshimiwa Waziri wa Fedha juzi alizungumza katika bajeti yake hatukumsikia hata kulitaja. Katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri Mkuu sikuona hata sehemu iliyozungumzia suala hili la kushughulikia wafanyakazi hewa. Kwa kweli katika hali hii ikiwa Serikali itaendelea kuwa na mtindo wa kuzungumza mambo halafu matokeo yake katika utekelezaji haupo, hili linawafanya Watanzania wakose imani na Serikali hii sikivu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hichohicho cha Bajeti cha mwaka 2011/2012, Serikali ilisema kuwa itafufua umeme Nyakato - Mwanza wa MW 60, hatukuona umeme uliofufuliwa wala uliozikwa. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, napenda niishauri Serikali pale inaposema mambo iwe na uhakika wa kuyatekeleza. Sisi tunajua kama Bajeti yetu tunayokwenda nayo ni bajeti tegemezi. Pia tunajua kama bajeti yetu ni bajeti ya mali kauli. Bajeti tunaitaja kwa maneno lakini matokeo yake fedha tunakuwa hatuna. Basi mimi naishauri Serikali pale inapokuwa tumeshindwa kuyatekeleza yale ambayo Bunge hili liliambiwa, Serikali

irudi tena iliambie hili Bunge kwamba tulizungumza hili na hili lakini halikutekelezeka, tusubiri kipindi kinachokuja mambo haya yatakekelezwa, wananchi watajenga imani na hii Serikali tuliyonayo lakini tukienda katika hali hii ya kuwa na maneno mengi lakini vitendo ni vifupi, wananchi wanakosa imani na Serikali hii sikivu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nijielekeze kwenye mfumuko wa bei.

## TAARIFA

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka nimpe taarifa tu kwamba sisi hatuko kwenye Serikali kwa sababu amesema kwamba sisi wote humu ndani ni Washirika wa CCM, sasa nimeona nimpe taarifa kwamba sisi hatuko kwenye Serikali na kwa mujibu wa Kanuni zetu kuna Kambi ya Upinzani kwa hiyo sisi siyo CCM hata kidogo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Rukia umekubali taarifa hiyo?

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, kwanza siitaki taarifa yake hata kuinusa kwa sababu sisi sote tunashiriki katika Kamati za Bunge na tunafanya kazi kwa kuisaidia Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niendelee na kuzungumzia mfumko wa bei. Mfumuko wa bei umekuwa ni mkubwa sana, hali hii

imekuwa ni ngumu sana, Watanzania wanalia, Watanzania wanaishi katika mazingira magumu, maisha yamekuwa magumu, yanazidi kuongezeka siku hadi siku. Tukiangalia Julai mwaka 2011, mfumuko ulikuwa kwenye asilimia 13 hadi kufikia Septemba, 2011 tayari ulishafikia asilimia 16.8, hadi kufikia Desemba, 2011 mfumuko wa bei ulishafikia asilimia 19.8. Hii ni hali ya kutisha, ni hali kukaa Wabunge tukajiuliza nini tufanye kuisaidia Serikali ili wananchi waondokane na ugumu huu wa maisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Tanzania mtu ana watoto sita (6) ndani ya nyumba, ananunua mchele kilo ni shilingi 2000 mpaka 2600, hivi jamani tunaishi vipi? Tusione sisi tuliomo humu ndani tuna viyoyozi, tunajisikia lakini wenzetu wanalala na njaa. Imefika mahali wanaume wanakimbia nyumba zao kutokana ugumu wa maisha, tunaoteseka ni sisi wanawake na watoto. Baba akikimbia nyumba mwanamke anabaki na watoto hajui afanye nini, anachanganyikiwa. Tunazidi kuongeza idadi ya wajane na watoto wa mitaani. Naiomba Serikali ilione hili ni janga la kitaifa na kwa kweli tufanye iwayyo lakini maisha yashuke, wananchi wanalia kwa dhiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, haya yote yanatokana na matumizi mabaya ya Serikali. Mapato ya ndani ya Serikali ni shilingi trilioni 8.7 hayakidhi hata matumizi ya kawaida. Matumizi ya kawaida yanakuwa yanaongezeka kutokana na Serikali kuongeza matumizi ya kiutawala kuliko ya maendeleo, hili halitaki mwenge, sote tunalionia. Kuna Mikoa chungu nzima iliyoongezwa na Wilaya, yote hii inataka matumizi na

matumizi yaliyopo ni kuwa tunabana matumizi ya maendeleo, tunatumia fedha hizi kwa matumizi ya kiutawala. Naishauri Serikali ipunguze matumizi ya kiutawala na fedha ziende kwenye matumizi ya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la kama tungekubaliana hapa kuongeza katika sekta ya kilimo, tukaipa kipaumbele badala ya asilimia 2.92 iliyopangiwa ikapangiwa asilimia angalau 10 tukaweza kufanya uzalishaji...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza kabisa, ningetoa angalizo kabla ya yote kwamba sisi tumekuja hapa kwa dhamana ya wananchi na tunahitaji kuwawakilisha wananchi ili wajue kwamba ni nini kilichopo, kinachotakiwa kifanyike katika maeneo yetu. Hatukuja hapa kwa ajili ya malumbano kuona kila mara au Bunge likawa linaitwa kama huko mitaani wanavyoliita Bunge la Miongozo. Kwa hiyo, naomba tuwe na fikra za dhana kwamba tumetumwa kuja kuwawakilisha wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nielekee katika suala la maji, maji imekuwa kila anayesimama hapa

anazungumzia suala la maji, atakayeinuka anazungumzia suala la umeme, hili limekuwa kama janga la kitaifa katika nchi yetu ya Tanzania. Tunao watalaam wazuri kabisa ambao wamefundishwa na Serikali hii. Wakafundishwa mpaka wengine wamekuwa Maprofesa wa kilimo ambao hawana hata shughuli zozote, inawezekana kabisa wataalam hawa wakatumwa vizuri, wakatutengenezea mabwawa ambayo yatajaa maji yakaweza kutupa umeme na pia yanaweza yakasaidia wananchi na hali kadhalika yakatumika katika umwagiliaji. Nafikiri watalaam hao tunao na tumewafundisha sisi wenyewe katika Serikali hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda nizungumzie suala la elimu. Suala la elimu, kwa kuwa TAMISEMI imezidiwa na mzigo mkubwa au ina mambo mengi na kwa kuwa Wizara hii ya TAMISEMI iko chini yako Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kweli katika suala la elimu imezidiwa. Je, sasa hivi inawezekana Wizara hii kwa kuwa na Halmashauri zetu zinashindwa kuisimamia vizuri sekta ya elimu ingefaa kabisa itolewe katika Halmashauri ipewe kitengo maalum ili iweze kusimamia vizuri elimu, suala la elimu lazima liboreshwe. Hakuna nyumba za Walimu, Mwalimu huwezi kumtoa hapa ukampeleka kijiji kwa mfano kule kwangu umpeleke Changaa, umpeleke huko Hondonailo hakuna maji, umpeleke kilomita 10 kutoka Kondoa Mjini mpaka Tumbelo, hakuna maji, hakuna umeme na kumefumuka na madini pia, katika hali kama hiyo uchumi kama huo unajitokeza lakini tunashindwa kuuboresha sisi wenyewe katika Serikali hii ambayo si sikivu jamani naomba tuangalie palipo na matumaini tupeleke nia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo sasa nije katika suala moja ambalo limejitokeza hapa juzi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa Serikali imeunda chombo cha usalama ili chombo hiki cha usalama kiweze kulinda mipaka yetu, mali zetu pamoja na raia lakini kitu cha kusikitisha sana ambacho nimekiona kilicho jitokeza hapa juzi, kweli hivi kweli lori likatoka huko lilikotoka mpaka likafika katikati ya Mji ambao una dhana ya kuwa Mji Mkuu wa Tanzania, limesheheni watu mpaka watu wale wamekufa mpaka wengine wameharibikia wamekuja kuwashusha katika Mji huu wa Dodoma! Hivi kweli lori hilo lingebeba silaha na sisi Serikali ilikuwepo hapa, hivi kweli sisi tungekuwepo sasa hivi? Suala hili kwa kweli limeleta masikitiko makubwa na inaonyesha ni rushwa imejaa moja kwa moja, rushwa kubwa ambayo imeenea katika mageti yetu yote.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi mkulima akilima shamba lake, akitoa mazao yake kule kijiji kuyapeleka mjini, akifika tu njiani anakutana na geti, lazima afunguliwe, aangaliwe ana magunia mangapi, ahesabiwe atoe hela. Leo hii lori limebeba watu kama wale na watu wale hawawezi kuja hivihivi bila kuwa na mkalimani, lazima Watanzania na wenyewe wanashiriki humu. Je, Serikali inaliangaliaje suala hili, mbona ni hatari kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la uwekezaji. Tanzania kweli imejikita katika suala kubwa la uwekezaji. Suala la uwekezaji kwa kweli tunawekeza ndio kama hawa watu wengine wanaingia katika nchi

yetu bila sisi wenyewe kujua kwa ajili ya huruma zetu. Suala la uwekezaji utakuta kwamba mwananchi kajivunia mwenyewe, kafyeka shamba lake, kaliandaa vizuri limependeza au Kijiji, tayari imekuwa mwekezaji pale anakwenda yeye mwekezaji. Hebu tuangalie kwanza migogoro mingi ya ardhi inatokana na kile kilichokuwa kizuri kinatamaniwa na kinaunganishwa na watu kutoka ngazi za chini kama *chain* kuja juu kwa kuwapa wawekezaji. Tujiangalie kwanza sisi wenyewe tumetosheka na ardhi. Kama sisi tumetosheka na ardhi na tunayo ya kuwapa Wareno twende tuwarudishe. Tumewaondoa Wajerumani tuwarudishe, tumewaondoa Waarabu tuwalete ili wazidi kuja kututawala zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi inabidi Serikali kuwa makini zaidi kuangalia na kuratibu hata katika sensa zetu watu wanavyopita nyumba hadi nyumba kuangalia nani yupo na nani kaja hapa na kwa nini na ni kabilia gani. Ipo haja ya kufanya hivyo kutoka na wasiwasi uliopo, maadui wataingia mpaka hapa ndani. Mpaka hivi sasa tumeuona na tumesuhudia kwa macho, hii ndiyo Serikali sikivu ya Chama cha Mapinduzi ilipotufikisha hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, nina masikitiko makubwa kuhusiana na migomo ya Madaktari lakini kwa angalizo zaidi, hukumu hii wanayo wananchi wenyewe na wananchi kwa kweli ndiyo wanaopata adha kubwa na wanaona matatizo yanayowakuta. Naomba Serikali yetu ichukue njia zingine za haraka kwa ajili ya kuweza kuokoa maisha ya wanadamu. Wanadamu wale ndiyo ambao wanatusaidia sisi. Sisi

wenyewe pia tukiumwa hapa sasa hivi lazima tukamuone Daktari, kama inafikia hatua hiyo, kwa kweli hali inakuwa ngumu.

Mheshimiwa Spika, nimalizie na kwamba katika Mkoa wetu wa Dodoma, tulioko hapa, tumeshajenga wodi moja ya akina mama, hospitali tunayo hapa na hospitali hii ya Mkoa haina zana za kisasa hata moja, ni hospitali hii majeruhi wakitokea hapa lazima wapelekwe Muhimbili. Kwa nini zana za kisasa zisiwekwe zote hapa ikawa ni hospitali kama ya rufaa, watu wanaotoka Mwanza basi wakaishia hapa, wasiwe wanapitiliza tena moja kwa moja mpaka Muhimbili. Wametoka Kanda zote huko za Kati waishie hapa hapa Dodoma na huko Mbeya hali kadhalika ikatengenezwa hivyo. Mbona fedha nyingi zipo? Fedha ambazo zinapatikana sasa hivi ni nyingi na madini tunayo, uchumi mkubwa tunao nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho niongezee tu kwamba katika Wilaya yangu ya Kondoa kumefumka madini na madini yale kwa kweli wachimbaji wadogowadogo wameyavumbua na ni moja ya sura ya nchi katika Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kondoa pia ina mapango. Mapango yale pia yameanza kupauka katika ile michoro. Naomba katika Idara ya Mambo ya Kale iongezewe fedha ili ikaboreshe zaidi mapango yale na kuwavutia watalii kama ilivyokuwa zamani na kuwaingizia pato la Kitaifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sitaunga mkono hoja mpaka haya yote yatekelezwe na yafanyike kwa ufanisi zaidi ili tuweze kulijenga Taifa letu upya na wananchi wawe na imani na sisi kama jinsi ilivyo, ahsante. (*Makofi*)

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhuhana Wataallah* kwa kunipa afya ya kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba ruksa yako kidogo nikariri ubeti wa shahiri moja unaosema, ni haki sawa kwa watu wote kuendeleza itikadi yetu. Utajirishwe itikadi yetu, tukatae kuonewa. Siasa itumikie uchumi na mwiko huo uchumi kutumikia siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ubeti huu ni wimbo wa Taifa wa Chama cha Wananchi *CUF*. Naiomba Serikali ichukue hapo siasa itumikie uchumi na iwe mwiko uchumi kutumikia siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapo ndipo tulipojikwa na tukishajua tumejikwa wapi, ni rahisi kutatua. Tusiangalie kule tulipoanguka. Tulipojikwa ni kwamba siasa inatumikia uchumi.

Mheshimiwa Spika, nchi hii ina utajiri wa aina nyingi. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu na tulifanya ziara katika Mikoa ya Kusini na Nyanda za Juu nikajiona kwa macho. Nilikuwa najua kijeografia, lakini nimeona kwa macho yangu na wasema *seeing is*

*believing.* Nchi hii ina rasilimali kubwa, lakini tatizo ni kwamba uchumi unatumikia siasa. Kwa hiyo, tubadilishe hapo ili tuweze kujenga maisha ya watu. Tukibadilisha ikawa siasa inatumikia uchumi, tutaweza kuboresha kilimo cha wananchi wetu. Hivi sasa asilimia 75 ya Watanzania ambao ni wakulima wana hali ngumu sana za maisha kutokana na kwamba siasa inatumikia uchumi. Wananchi hawa asilimia 75 hawana nyenzo za kuendeleza kilimo, Serikali imetenga bajeti ndogo kwa ajili ya kilimo ambayo ni 192 billioni. Kwa kweli hii ni pesa kidogo sana. Wakulima hawa hasa wadogowadogo wakiwezeshwa, ndiyo tutakapoweza kujenga uchumi imara ambao ndiyo tutakuwa tumezunguza umaskini, maradhi na utapiamlo.

Mheshimiwa Spika, watoto asilimia 42 walio chini ya miaka mitano (5) wana utapiamlo, maradhi ya kwashakoo, hii yote inasababishwa na ukosefu wa chakula bora. Hii ni idadi kubwa ya watoto ambao ndiyo Taifa letu la kesho tunalolitegemea kuongoza nchi hii. Tuimarishe uchumi kwa kuimarisha kilimo ambacho ndicho tulikuwa tunaambiwa katika *slogan* ya nchi hii kwamba ndiyo uti wa mgongo wa Taifa hili. Kwa hiyo, illi iwe utii wa mgongo kweli, tuwasaidie wakulima wadogowadogo kuwapa nyenzo za kilimo, mbolea na pia kuwajengea miundombinu itakayowawezesha kufikia masoko, barabara, reli, bandari na pia Serikali isimame mbele kuwatafutia masoko wakulima ili mazao yao yaweze kuuzwa na kupata maisha yaliyo bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna neema imepatikana ya gesi ambayo tunaambiwa inachimbwa huko Mikoa ya Kusini na gesi hii ni utajiri mkubwa kwa kweli, tukiutumia vizuri utatunufaisha katika nchi yetu. Naiomba Serikali ichukue ushauri wangu wa siasa kutumikia uchumi, mapato ya gesi hii yajenge miundombinu ya nchi ya kiuchumi ikiwemo kuimarisha barabara, kujenga reli za kisasa, kujenga bandari na mambo mengine ya viwanda vitakavyoweza kuimarisha mazao ya kilimo ili kuiongezea thamani na wakulima wakapata maisha yaliyo bora. Hivi sasa Watanzania wanatumia asilimia 50 ya mapato yao kwa ajili ya chakula kutokana na maisha kuwa magumu, bidhaa zimepanda sana na pato la Mtanzania ni dogo, ni kutokana na mfumuko wa bei ulivyo ni kwamba hii asilimia 50 itaongezeka, itafika mpaka asilimia 65 au 67 ya mapato ya Tanzania kwenye chakula. Kwa hapa, utaona hatuwezi kuendelea au kuwainua watu wetu kiuchumi kwa sababu itakuwa ni watu wanaochumia tumbo tu, hawawezi kupata afya nzuri, nyumba nzuri, elimu nzuri hata nguo za kuva watakuwa wanaishia kuva mitumba tu ambayo inasababisha maradhi mengi ya ngozi, wataalamu wengi wamethibitisha hilo. Naishauri Serikali ya CCM ishirikiane na wataalam walioko katika chama cha *CUF* wa kiuchumi kuweza kuboresha uchumi wa nchi hii na wachukue wasia niliowapa wa siasa kutumikia uchumi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, twende kidogo katika jambo lingine la elimu. Hali ya elimu inatisha, wanafunzi wanaofaulu hawajui kusoma na kuandika, tatizo sijui ni nini labda leo hapa Serikali itueleze kwa ruksa yako

kwa nini, kuna tatizo gani Baraza la Mitihani? Wanafunzi wanafaulu hawajui kuandika, wenyewe uwezo wa kufaulu wanafutiwa matokeo, hili ni tatizo. Kwa hiyo, naiomba Serikali itueleze tatizo hili litakwisha lini na kumuondosha mtumishi mmoja wa Baraza la Mitihani si dawa kwamba ndiyo umetibu tatizo. Nashauri Baraza la Mitihani lifumuliwe, wapangwe wataalamu upya watakaoweza kuisaidia nchi hii kwenda mbele kielimu. Bila ya elimu na miundombinu iliyo madhubuti na *infrastructure* za kiuchumi, hatuwezi kupiga hatua, tutakuwa ni taifa siku zote la kuomba na tunaelekea sasa hivi kuwa Taifa la kusaidia. Tuna mwelekeo mkubwa wa kuwa *donor country*, lakini tukilegea, tukaendeleza mtindo wetu wa uchumi kutumikia siasa, tutakuwa *beggar country ila yaumul kiama*. Naiomba Serikali ya CCM, naishauri Serikali ya CCM ichukue nasaha ninazowapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nataka kulieleza hapa ni kuhusu utawala bora. Utawala bora ni jambo la muhimu ili kila mtu aweze kupata haki yake. Kumnyima mtu haki yake ni kurudisha nyuma maendeleo ya Taifa. Watu wanakuwa waoga kuijendeleza kiuchumi kwa sababu utawala bora unawazuia. Kila mtu akijitahidi kufanya kazi, vipingamizi vyta utawala bora vinamzuia. Kwa hiyo, utawala bora ni muhimu kuuimarisha kwa masilahi ya Taifa letu. Mimi pamoja na kwamba nipo katika Chama cha Upinzani, Chama cha *CUF*, lakini ni Mtanzania na nina imani kwa Tanzania na najivunia kuwa Mtanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mambo mazuri tunayowaeleza, tunawaomba au tunawataka

myachukue, myafanyie kazi na yale ambayo mnaona hayahitaji kufanyiwa kazi, mtuambie, tushauriane. Nchi hii ni nchi nzuri ambayo inatizamwa na wengi kwa jicho la ubaya. Tusije tukatumbukia katika shimo la kwamba tuko katika kutafuta mali, baada ya kupata mali hiyo, tukasema tugombane kwa kugawana mali hiyo, then tukaiacha mali hiyo bila kuitumia. Iko hadithi moja inasema "*The good, the bad and the ugly.*"

Mheshimiwa Spika, nashauri rasilimali tulizonao tuzifanyie kazi vizuri. Nchi iko katika *tense*, hali hatari. Tatizo ni kwamba vijana hawana ajira ambao ni zaidi ya asilimia 70 ambao wanaishi vijiji na ajira ni kilimo. Kwa hiyo, Serikali iongeze zaidi kwenye kilimo ili ajira za vijana zipatikane, wapate kazi na nchi ipate kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ahsante sana.  
*(Makof)*

**SPIKA:** Amenikumbusha Mheshimiwa Moza kwamba tunaitwa Bunge la Miongozo, sasa kutakuwa na Waheshimiwa Miongozo humu humu ndani maana wanajulika Waheshimiwa Miongozo.

Ahsante, sasa tuendelee na Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac, atafuatiwa na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba na Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu ajiandae.

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hotuba ya Waziri Mkuu.

Nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii iliyo adimu katika Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kuchukua nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema aliyeneweza kwenye kufanya na nguvu ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kuwawakilisha wananchi wa Tanzania ambao bado wanaendelea kutaabika na kuteseka kwa kukosa huduma bora za kimsingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sitakuwa nimewatendea haki wananchi wangu wa Mkoa wa Katavi na Rukwa kwa kuunga mkono bejeti hii. Nianzie na suala la elimu. Naongeza mbele ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa upande wa elimu kwa Mikoa yetu Rukwa na Katavi, kwa kweli ni masikitiko makubwa, bado tuko nyuma sana. Napenda sana Serikalli itoe kipaumbele kwa elimu ya msingi, kwa sababu elimu ya msingi ndiyo ngazi ya mwanzo hata kama mwananchi anajenga nyumba, kwanza anazingatia kuimarisha msingi ili kuwa na nyumba bora. Kwa hiyo, kabla hatujafika ngazi ya sekondari na elimu ya juu, kwanza tuimarishe msingi. Mimi ni mwepesi sana kama kawaida yangu huwa nikitoka Bungeni sikai mjini, huwa nazunguka kwanza Vijijini kuangalia Watanzania wenzetu wanaishi katika mazingira yapi, kwa kweli inasikitisha sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitolee mfano Tarafa ya Mpimbwe, shule ya Kata ya Majimoto, nilizungukia kule nilitamani kulia na ilibidi nipige picha na wanafunzi na Walimu kwa kumbukumbu. Shule wanazosoma, ni bora shule, bora elimu lakini sio elimu bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wanafunzi hawana madawati, wanakaa chini kwenye vumbi, ile vumbi afadhali kama ingekuwa ni sakafu, wamewekewa simenti lakini ni kwenye vumbi. Hatujui usalama wa afya za watoto wetu ndani ya sketi na kaptula zao, jamani inasikitisha sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania tunakokwenda badala ya kusonga mbele, tunazidi kurudi nyuma. Nawapa pole sana wazazi kwa kuwasomesha watoto, Watanzania wenzangu mnaonisikia, poleni sana wazazi wenzangu. Huduma ya maji wanafunzi hawana, mtoto ili afaulu vizuri anatakiwa ale chakula, anywe maji safi na salama ili akili ichaji, ifanye kazi, aweze kufuatilia masomo anayofundishwa lakini shule zetu za msingi kule hazina kisima hata kimoja. Mtoto tangu alivyotoka nyumbani kwa wazazi wake mpaka anatoka shule hajapata maji. Watoto wanahaha kwenye majumba ya Walimu kutafuta maji, lakini na Walimu nao ndiyo mkumbo mmoja wanahangaika kutafuta maji. Kwa hiyo, mtoto anasoma katika mazingira magumu, midomo imemkauka, maji hana. Nilijaribu kuongea na Walimu wanasema sasa hatuna jinsi ya kufanya. Nilienda kukagua vyoo vyao, kwa vyoo wamejitatihidi, vyoo ni vizuri, lakini kwa kuwa hawana visima vya maji wale watoto wanatumia karatasi au majani, jamani! Miaka hamsini ya uhuru? Tumefanikiwa, tunasonga mbele, sijui kweli? Tunasonga mbele hivi kweli? Mimi kwa kweli nashindwa kuelewa, naomba mnisamehe sana, lakini naongea ukweli kwa sababu nimezunguka na nimejionea kwa macho. Walimu hawana nyumba za kuishi, Walimu wanositisha, baba anapotoka na

kikoi chake kwenda kuoga huyo inabidi mama amfuate na kitenge kwenda kuziba ule uwa wa majani, ndiyo baba aoge, atoke. Anaoga huku juu linammulika, ndege wanamchungulia, jamani! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tunakokwenda ni kugumu sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu boresha Mkoa wetu Baba na nina imani unaweza kwa sababu sura ya Mji, nikiona pale Mjini, kweli sura imegeuka, Mji unaleta raha kiasi kwamba tukiendelea namna hiyo bado uko madarakani, tutakuwa ulaya. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Shule ya Mwese, hiyo ni Tarafa nyingine, sasa hapo nimetoka kwenye Jimbo la Waziri Mkuu, naenda Tarafa ya Mwese, shule la Mwese ambayo mimi nilisoma wakati baba yangu akiwa Mwalimu Mkuu pale. Nimesoma miaka ya sabini na lakini shule ile nilivyoitembelea, nimeikuta kama nilivyoiacha. Nikaingia na nyumba tuliyokuwa tunaishi, kama nilivyoiacha nikiwa shule ya msingi haijfanyiwa matengenezo wala ukarabati wowote. Watoto wanakaa chini, simenti zote zilishachimbuka, kuta zimepasuka hovyo kiasi kwamba ni hatari kwa maisha ya watoto wetu. Jamani tunakokwenda ni wapi? Mimi nashindwa kuelewa, sijui hili jibu atanijibu nani? Vyoo vimefurika, vimetapika, madawati hamna, Walimu wenyewe wanakalia kwenye madawati eti ndiyo viti vya Walimu ofisini, jamani! Kwa kweli hiki ni kitendo cha aibu. Mishahara yao haifiki kwa wakati, hawana usafiri wa kutosha wanapofuata mishahara yao Mjini ambapo ni maili 70, wanahangaika kudandia mabasi

kama ni masika barabara zetu zenyewe miundombinu mibovu, kwa kweli ni shida tupu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kwa kweli, Wizara zitakapoanza kutenga pesa, mimi naona tatizo liko kwenye ukaguzi. Naomba Wakaguzi wa elimu wapewe kipaumbele sana kwa sababu hawa Wakaguzi wa elimu wangepewa kipaumbele, wakapewa magari ya kusafiria, wangezikagua zile shule zetu na zikaboreshw. Nikiangalia Wakaguzi wana nia ya kufanya kazi, lakini unakuta wanategemea gari moja wanyang'anyane na Mkurugenzi na Mkurugenzi akijifanya ni Mungu mtu akipandisha mabegi juu basi yule Mkaguzi hawezi kupata nafasi ya kwenda kukagua shule. Naomba kwa kweli Wakaguzi wa elimu wapewe kipaumbele, wakague shule zetu, watoe taarifa na mara moja shule zile zipewe kipaumbele kufanyiwa ukarabati, watoto wetu wapate madawati wasipate magonjwa ya minyoo kwa kupitia sehemu za siri wanavyokaa kwenye vumbi. Jamani! Inasikitisha kweli. Walimu wetu mimi nikiwatembelea naona hata aibu kuwaangalia usoni. Nilitamani kulia walivyokuwa wakinilalamikia lakini sina jinsi, nitawasaidia nini? Ndiyo Serikali yetu hiyo ya Chama cha Mapinduzi, miaka hamsini ya uhuru, tumefanikiwa, tunesonga mbele na tutazidi kusonga mbele. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakuja kwenye suala la maji. Maji ni kilio kitupu hasa vijiini. Japokuwa na mjini kuna shida sana, tunategemea tanki lenye ujazo wa 100,000 yale maji hayatoshi kusambaza mji mzima. Watu wako laki, hebu ngoja, maana niende na takwimu.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mpanda wako 680,000 lakini lile tanki lenye ujazo wa lita 100, linatosheleza kwa watu 41,000 tu...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Wengine wote wanahaha juani kutafuta maji...

**SPIKA:** Ahsante, hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Spika, kengele ya pili! Lakini naomba Serikali jamani iwajali walimu, ituletee maji vijijini. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni ya leo. Lakini pia nichukue nafasi hii kuishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi nzuri ya kuwasilisha bajeti hii. Kwa sababu, ndani ya bajeti kwa kweli, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Busanda, niseme, umetupendelea sana kwa sababu, imezungumzia kuanzishwa kwa kituo cha kuwawezesha wachimbaji wadogo wa madini, Rwanagasa, lakini vile vile umetupa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Geita. Hii yote nina uhakika kabisa kwamba, unasogeza huduma kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa suala la nishati na madini, nikianzia na nishati, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Busanda, nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa

jinsi ambavyo imetuhudumia wananchi wa Busanda. Sasa hivi nguzo zimewekwa na nyaya katika Kata ya Bukoli, Rwamgasa, Nyarugusu na mpaka Katoro sasa wanaweka nguzo. Lakini vile vile katika Tarafa ya Butundwe, wameweka katika Kijiji cha Bukondo, Chikobe, Chigunga, kwa kweli, sisi wenyewe tunajivunia Serikali yetu. Nina uhakika kwamba, wananchi watanufaika na umeme huu. Lakini niombe tu kwamba, Serikali inieleze, ni lini utawaka umeme huu ili na wananchi wasikie, waanze kujandaa kwa ajili ya uwekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa habari ya madini. Kwa sababu, kinaanzishwa Kituo cha Uwekezaji cha kuwasaidia wachimbaji wadogo pale Rwamgasa, niiombe sasa Serikali, iwawezeshe wachimbaji hawa kwa kuwapa maeneo ya uchimbaji. Katika Sera ya Madini ya mwaka 2010, imezungumza wazi kabisa kwamba, Serikali itawapa maeneo ya kuchimba wachimbaji wadogo na kuwawezesha pia. Naona tayari Serikali imeshaanza hatua kwa kuanzisha maeneo kwa ajili ya kuwawezesha, lakini niombe sasa kwa ajili ya wananchi wa Nyarugusu, bado hawajapata maeneo ya kuchimba.

Mheshimiwa Spika, vile vile na pale Nyaruyeye, mwaka huu tunashukuru kwamba, kulitokea *brush*, *gold brush* na wananchi wanachimba kidogo kidogo. Lakini niombe sasa wananchi wa pale Nyaruyeye wapate maeneo ya kuchimba kwa sababu wanapowezeshwa nina uhakika kabisa kwamba, tutaweza kufikia malengo ya milenia kwa sababu, Jimbo la Busanda, tunategemea madini na Geita kwa

ujumla inaongeza kipato kupitia madini. Kwa hiyo, niiombe kabisa Serikali, iwave maeneo ya uchimbaji ili kuwawezesha wananchi hawa kufaidika na rasilimali tuliyonayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu. Ninayo changamoto kubwa katika shule za sekondari 16 katika Jimbo la Busanda. Hizi sekondari kwa kweli zina upungufu wa nyumba za walimu. Walimu wanahangaika sana. Niiombe Serikali kwa sababu suala la umeme sasa inalishughulikia, niombe pia hata nyumba za walimu wa Sekondari iweze kuzishughulikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile mazingira sio mazuri sana kwa watoto wetu, hasa wa kike ambao mara nyingi wanapata mimba kwa kwenda shule za mbali. Kwa hiyo, niombe pia Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha *hostel* kwa watoto wetu ili waweze kufanya vizuri katika masomo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, pia hatuna Chuo cha *VETA* katika Wilaya na Mkoa wa Geita. Kwa hiyo, Serikali pia ianzishe *VETA*; hatuna chuo kabisa japokuwa tuna shule nyingi za Sekondari, lakini Serikali kwa kweli, ituwezeshe basi na sisi tuwe na Chuo cha *VETA* ili watoto wetu wanaomaliza kidato cha /V, wapate nafasi ya kuweza kupata ujuzi. Hivi tunapata umeme sasa, wawe na ujuzi wa kuweza kufanya kazi zao vizuri kwa sababu watakuwa na ujuzi kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba, pia katika upande wa elimu ya shule za msingi, tunao Waratibu Elimu. Waratibu hawa wanahitaji usafiri, wapewe pipipiki pamoja na posho za kuwawezesha, ili waweze kufanya kazi zao vizuri. Unakuta Mratibu wa Elimu, anahudumia shule za msingi nne au tano, hana usafiri. Kwa hiyo, niombe sasa Serikali iangalie hata namna ya kuwakopesha ili waweze kufanya kazi zao vizuri na elimu ya shule za msingi iweze kuboreshwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vile vile katika Jimbo la Busanda na Geita kwa ujumla, tunategemea kilimo. Kwa vile, Jimbo limegusa katika Ziwa Viktoria, nilikuwa naomba kwamba, tuanzishiwe basi skimu za umwagiliaji hasa katika Vijiji vya Bukondo pamoja na kule Kasamwa, kwa kweli, wanajishughulisha na shughuli za kilimo. Kwa hiyo, tukianzishiwa skimu za umwagiliaji, nina uhakika kabisa kwamba, suala la njaa litakuwa ni historia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile kwa upande wa kilimo. Tunashukuru kwa ajili ya ruzuku ambazo zinatolewa kwa ajili ya wakulima wadogo wadogo. Pia niombe kwa upande wa mifugo, Serikali iangalie namna ya kuwasaidia wafugaji. Kwa sababu, wako wafugaji ambao wanahangaika sana hasa hasa kwa chanjo ambazo wanalipia hela nydingi sana. Ninaomba Serikali iangalie namna ya kuboresha suala la chanjo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vile vile kwa upande wa afya. Waziri Mkuu, aliniahidi gari la wagonjwa, Kituo cha Afya Chikobe. Naomba sasa Serikali, ilete gari hili, ili

wananchi waweze kufurahia huduma na Tarafa nzima ya Butundwe waweze kutumia gari hili la wagonjwa. Kwa sababu, Kituo hiki kiko mbali na wananchi wako mbali, takribani kilometra 50 kutoka katika Hospitali ya Wilaya ya Geita, kwa hiyo, wanahitaji gari ili waweze kupata huduma, hasa hasa akinamama wajawazito ambao wanahitaji huduma ili tuweze kupunguza vifo vya akina mama ambao ni wajawazito. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, labda tu nisahihishe kidogo kwamba, tunashukuru kwa Halmashauri ya Mji Mdogo wa Geita. Pia suala la ulinzi na usalama kidogo limekuwa ni tete katika Jimbo la Busanda, hasa hasa katika Vijiji vya Katoro, mara nyingi kunatokea matukio ya ujambazi. Lakini vile vile Kasamwa na Bukondo, kumetokea matukio ya ujambazi. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuweka ulinzi katika maeneo hayo ili wananchi waweze kuishi kwa amani na furaha na kuendelea na shughuli zao za kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, Mji wa Katoro ni mahali ambapo ni mji mkubwa ambao una shughuli nyingi sana za kiuchumi. Kwa hiyo, unahitajika ulinzi wa kutosha ili wananchi waweze kufanya kazi zao vizuri. Hata ikiwezekana Serikali iangalie namna ya uwezekano wa kutengeneza hiyo centre ya kibiashara kwa sehemu za Kanda ya Ziwa kwa sababu, kwa kweli, ni sehemu ambapo kuna biashara nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, niombe tu kwamba, kwa sababu Serikali inaendelea kufanya mambo mazuri hasa katika Jimbo langu, hasa kwa

kero mbalimbali ambazo zimekuwepo kwa muda mrefu, imeendelea kuzishughulikia na sasa nina imani kabisa kwamba, itaendelea kushughulikia suala ambalo nimelizungumzia, upungufu wa nyumba za walimu na pia itaendelea kuweka hizo skimu za umwagiliaji kwa ajili ya wananchi wangu. Lakini vile vile italeta gari la wagonjwa Chikobe. Lakini sambamba na hilo, itahakikisha ulinzi na usalama katika Jimbo la Busanda kwa ujumla na Geita yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache niombe kwamba, kwa pale Katoro Serikali iwekeze kwa sababu, ni *centre* kubwa ambayo, nina imani kabisa tukiwekeza nina uhakika tutafanikiwa. Kwa vile na umeme unakuja sasa, niiombe Serikali iwekeze, lakini pia hata wananchi wawekeze. Wawekeze mashine za kusaga, za kukoboa mpunga pamoja na shughuli mbalimbali ili kuweza kutengeneza ajira kwa ajili ya vijana wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru sana kwa nafasi hii, nikiamini kwamba, wananchi wa Busanda wanaendelea kunipa ushirikiano mkubwa. Pia nawashukuru sana kwa ushirikiano ambao wanaendelea kunipa mpaka sasa na niseme kwamba, nitaendelea kufuatilia kero moja hadi nyingine kwa kadri ambavyo itakavyokuwa na Serikali inaendelea kunisikiliza na naamini itaweza kushughulikia kero moja hadi nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru sana kwa muda huu ambao umenipa. Naunga mkono hoja

ya Waziri Mkuu, nikiamini kwamba, kwa kupitisha bajeti hii, mambo yatakwenda vizuri zaidi. (*Makofi*)

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini naomba niseme taratibu sana kwa sababu, kichwa changu, naona kama hakiko sawasawa.

Mheshimiwa Spika, lipo jambo nisipolisema nitakuwa sikutenda haki. Tarehe 18 Aprili, saa 12.00 asubuhi, nilipata ajali mbaya sana pale Milima ya Gairo. Namshukuru sana Naibu Spika, saa 3.00 alitoa taarifa, nikapata simu kutoka sehemu mbalimbali. Pia niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge watatu, madada zangu ma-Sharif wanaitwa, hawa wanajielewa, kwa sababu, wengine walikuwa nyuma yangu, wengine walikuwa mbele. Nilipopinduka mara tatu, nikaingia kwenye mtaro chini juu na nina uhakika zingezidi dakika 30 kwa sababu, hali ya hewa kule chini ilikuwa mbaya, ningeweza kupoteza maisha. Lakini walikuja, wakaita watu, wakanikaoa. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia nimshukuru sana *RC* wa Morogoro, kaka yangu Joel Bendera na *RAS* wa Morogoro, kwa jithada zao na Madaktari wa Morogoro na *RAS* wa Dar-es-Salaam kwa mapenzi makubwa. Vile vile niwashukuru Dokta Mareale wa Muhimbili na Dokta Mlawa, kwa mapenzi makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana sana wananchi wa Temeke, walikuwa wamejazana

nyumbani; nilikimbia Hospitali, ikabidi nije nyumbani. Nawashukuru sana kwa mapenzi na dua zao, pia wananchi wote wa Dar-es-Salaam, Wabunge wenzangu wote wa Dar-es-Salaam, mke wangu na watoto wangu na hasa Tamia wa miaka nane alikuwa akinitazama na kuniita baba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sidhani leo kama nina maneno mengi. Kwanza niseme mapema kwamba, siiungi mkono bajeti hii na sababu za msingi, ninazo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 16/8/2011 tukiwa hapa hapa ndani, Kitabu cha *Hansard* ninacho hapa, Dar-es-Salaam tuliongea matatizo yetu yote kwa ujumla, lakini ikatoka kauli hapa ndani kwamba, Wabunge wa Dar-es-Salaam, matatizo yenu tutakwenda kuzungumza kwa pamoja; kauli hiyo aliitoa Waziri Mkuu. Sisi tukaiamini kauli ya Waziri Mkuu wetu, lakini chakusikitisha tumefuatilia, tunesema, hatukupata nafasi ya kuzungumza naye. Sasa tunajaribu kujiangalia kweli, iko haja ya sisi kuendelea kuwa Wabunge wa Dar-es-Salaam? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama 85% ya mapato ya nchi hii yanatoka Dar-es-Salaam, lakini Wabunge wa Dar-es-Salaam hatupewi uzito, tunadharauliwa. Inasikitisha sana. Tuna masuala ya msingi pale Kurasini, wananchi wale wanapata shida toka 2005. Tunataka kupanua Bandari, tumechukua eneo lao, lakini kuwalipa fidia tunashindwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme ukweli, pale wanunuzi wapo wengi wanapalilia Kurasini. Isipotoka kauli hapa

ya kwenda kuwalipa wananchi wale, nikirudi nitatafuta wanunuzi, tunauza yale maeneo. Liwalo na liwe kwa sababu, zile ni nyumba zao na haki ni zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kaongea Ndugulile, *Kigamboni New City*, watu wanateseka. Wakati tunaomba ridhaa kwa wananchi, tulisema tutasimamia maisha bora na kila kinachomhusu mwananchi. Sasa matokeo yake yamekuwa sivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini wewe ni shahidi na nyote ni mashahidi, pamoja na kwamba tunapoongelea Dar-es-Salaam hapa, wengi hatukubali kuunga mkono, lakini wengi wetu tunaishi Dar-es-Salaam. Hali ya Dar-es-Salaam ya msongamano inatisha. Sisi Wabunge tuliopita, tulikuwa na mpango wa *fly over* na JAICA alifanya *feasibility study*, kila kitu kilifanyika. Wenzetu Kenya, walikuja nyuma, sasa hivi wana *fly over*. Lakini sisi sijui ni dharau, sijui ule mji unaonekana chuma ulete, hata haifahamiki. Hadi leo Dar-es-Salaam inasikitisha, hatujui sababu yake ni nini? Msongamano kupita kiasi. Inawezekana mliuona zamani msongamano, lakini sasa hivi kwa kuwa mnapelekwa na mapikipiki na magari, hamuuoni msongamano. Lakini hali inatisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yako mambo ya *National Housing*. Nampongeza sana *DG* wa *National Housing* ni rafiki yangu, timu yake inafanya kazi nzuri, naipongeza sana. Lakini yako mambo tuliongea ndani ya Bunge hili kuhusu nyumba za *National Housing*, zile za maghorofa ziuzwe kama *apartment*. Rais, akiwa Iringa nakumbuka na mimi nikiwa Mbunge, ilikubalika.

Lakini cha kusikitisha na cha aibu, leo *National Housing*, nyumba zile zile, ukienda Mchikichini, ukienda Chang'ombe, ukienda Ubungo, *National Housing* wamekwenda wamejenga mbele ya nyumba zile za zamani katika maeneo yale ambayo yalikuwa *open space* ya kupidisha *fire*. Halafu wana tangazo lao moja wanaonesha mtu anakimbiza kuku eti, kuna mabanda ya kuku, kuonesha kwamba, wao sasa ndio wamezuia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nyumba hizi wanazojenga watu wameshanunua, lakini zile ambazo tulikubaliana, iko hapa Naibu Waziri akizungumza na yeye. Naibu Waziri, alizungumza hapa kwamba, atakutana na Wabunge wa Dar-es-Salaam, kuzungumzia namna ya kuuza nyumba zile. Lakini lile tuliloazimia kwenye Bunge hili, halikuwa kwa Wabunge wa Dar-es-Salaam tu, zilikuwa nyumba zote za *National Housing* za nchi nzima; wauziwe watu wanaokaa katika nyumba zile, lakini mpaka leo halijafanyika. Natumaini katika Bunge hili, tutaambiwa utekelezaji wa suala hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Temeke kwenye Manispaa yangu kulikuwa na ubadhirifu. Namshukuru Waziri, dada yangu mama Ghasia, akatengeneza Tume. Tume ile ikafanya kazi nzuri, imeleta taarifa. Wale wabadhirifu mpaka leo bado wako pale ofisini. Sasa mimi niwaulize, hivi tukishafanya hiyo kazi kinafuatia nini? Au mnatutaka Wabunge, tufanye kazi hiyo sasa? Kwa sababu, majina tunayo, mkituruhusu, nikimaliza Bunge, nitakwenda mmoja mmoja namtoa Ofisini, wala sishindwi. Kwa sababu, hayo ni majukumu yenu,

kama hamfanyi ninyi mnatuachia sisi, sisi tutafanya.  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini liko jambo lingine ambalo sijui ni kwa nini lilitfanyika? Jiji la Dar-es-Salaam lilitfutwa 2010 na sisi tukiwa Wabunge, bila kushirikishwa. Kwa hiyo, tumefanya uchaguzi ule wa Meya, ni batili. Mikataba tulioingia ni batili. Nasikia Jiji limerudishwa 2012. Sasa mimi nauliza, lilitfutwa kwa nini? Kwa nini msituulize? Sisi ndio Wabunge, sisi ndio wawakilishi wa watu wa Dar-es-Salaam, mngetuuliza, mmefuta, sawa, mngetuuliza sisi tungesema sawa, acheni Manispaa tatu, lakini mmelirejesha; sasa mtujibu hapa, wakati mmefuta mpaka mmerejesha, ile Mikataba na mambo yote yaliyofanyika, tunahesabu yakoje? Yako sahihi au hayako sahihi? Ni lazima twende kwa utaratibu wa kueleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa *Ring Road*. Tulianza utaratibu mzuri pale Dar-es-Salaam, nakumbuka. Waziri Kawambwa, akiwa Waziri wa Miundombinu, tulikutana naye hapa, tukiomba bilioni tisa, tukapewa bilioni 20 tukaweka mpango mzuri kabisa wa kuondoa msongamano, wakati ule *RC* akiwa Mzee Kandoro, *TANROAD manager* akiwa Nyakabazi ambaye sasa hivi kahamishiwa Mbeya. Tulikuwa tunakwenda vizuri, sisi tunaomba tuendelee na utaratibu wetu ule, hatupendi utaratibu wa mtu kupanda juu ya jukwaa akatuambia anatupa daladala 25 kama hisani, tungependa twende na utaratibu ule ule ambao tulikuwa tunakwenda nao. Yule meneja wa *TANROAD* mtu mzuri sana, mkewe yuko hapa Mbunge, lakini tumeshangaa kaondolewa

kaelekwa Mbeya wakati alikuwa anatufanyia kazi nzuri ya kuondoa msongamano Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, lakini siungi mkono mpaka nipate majibu haya. (*Makofi*)

**MHE. KISYERI W. CHAMBIRI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja hii ya Waziri Mkuu na nashukuru kabisa kwamba, hoja hii leo nimeipata wakati mwafaka.

Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati tukiwa hapa Bungeni, Wapinzani wetu wa Viti Maalum wako huko Babati na wanatangaza kwamba mnaelewa Mbunge wenu hayupo ndani ya Bunge wala haonekani popote. Sasa kwa kuniruhusu nichangie, naamini sasa wananchi wa Babati wanania na wakilisha tena nawawakilisha vizuri kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kusema kwamba naunga mkono hoja. Bunge hili la mwisho nilikuwa natoka Arusha na basi la Mtei, tulipofika pale Minjingu kuna kijana wa miaka kama 23 wakati ule ndiyo tunafanya sherehe zile za miaka 50 akasema kwamba CCM miaka 50 haijfanya chochote, nikamuuliza kijana yule wewe una umri gani akaniambia nina miaka 23, nikanyamaza. Baada ya dakika 45 tukawa tuko Babati Mjini, kabla ya ile barabara ya lami haijatengenezwa tulikuwa tunatembea masaa manne kutoka Minjingu mpaka Babati Mjini. (*Makofi*)

Sasa nikauliza yule kijana kwamba bado unafikiri CCM haijafanya chochote, yaani imeongeza maisha yako kwa masaa matatu. Sasa matatizo makubwa tuliyonayo ndani ya Kambi yetu ya Upinzani nafikiri ni umri mdogo. (*Makofi*)

Wawakilishi wanaochaguliwa kuja ndani ya Bunge hili wana miaka 20, 25 mkubwa sana 30, hawaelewi nchi yetu hii huko nyuma ilikuwa namna gani. Wangeelewa nchi yetu hii ilikuwa namna gani hizi kauli za kusema kwamba hakuna kilichofanywa wangezizima kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, iko hadithi moja, Mzee mmoja alikosana na mke wake, kwa hiyo akaamua amfukuze. Wakaenda kwenye kesi akashinda, lakini mzee mmoja wa hekima akamwuliza yule kijana kwamba miaka yote 20 uliyokaa na mke wako hajakutendea jambo hata moja jema, yule kijana akafikiri sana mwishowe akasema mama huyu kwa kulima ni hodari sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo yule mzee wa hekima akamwambia sababu mama huyu ni hodari sana kwa kulima, basi kwa jambo hilo moja zuri mchukue mwendelee kuishi naye. Sasa hawa siku zote wanapinga tu kweli miaka 50 hakuna hata moja zuri ambalo CCM wameona imefanya ? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali sana...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Naomba tumuachie mtu afanye kazi anasema mambo yake, taarifa inatoka wapi. Mheshimiwa Chambiri, naomba uendelee kuchangia.

**MHE. KISYERI W. CHAMBIRI:** Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali sana sababu Mji wa Babati ni makutano ya barabara na sasa barabara zetu karibu zote zina lami, Minjingu-Singida saa hizi tuna lami mpaka Bonga na naelewa inaendelea itafika Dodoma. Lakini kizuri zaidi wameanza kutujengea barabara kwa Awamu kwenda Galapo, wanatuwekea lami, nawapongeza sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa nimkumbushe Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba wakati Rais alipokuja katika kampeni pale Babati Mjini alituahidi kwamba atatupa kilomita mbili za barabara ya lami. Sasa inakwisha miaka miwili hata harufu yake hatujasikia. Nataka sasa katika Bunge hili nielezwe kwamba hii barabara ya lami ambayo tuliahidiwa itajengwa lini ? Maana muda unakwenda haraka isije kwisha miaka mitano hii barabara haijajengwa. Nataka atueleze kwamba hii barabara itajengwa lini.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nataka ileweke kabisa kwamba kabla hii mikoa mitatu haijatangazwa sisi ndiyo tulikuwa mkoa kitinda mimba, Mji wetu ultoka kuwa Kijiji na kuwa Mji Mkuu wa Mkoa na Halmashauri bila kuititia zile taratibu za kawaida za kukua Mji. Kwa hiyo, hatuna miundombinu kabisa ndani ya mji wetu. Tutaleta maombi toka Babati kwamba tupate fedha za ziada kuweza kuboresha miundombinu yetu ndani ya mji.

Mheshimiwa Spika, sasa niingie kwenye ardhi. Kampuni ya Tanzania *Breweries* ilikuwa na shamba ambalo ni zaidi ya heka 3,000 katika maeneo ya Kata ya Babati Mjini, katika Kijiji cha Singu, wakati huo hii kampuni ilikuwa ni ya Serikali. Kwa hiyo, ile ardhi ilikuwa yetu sababu shirika lilikuwa Shirika la Umma. Ile ardhi ili hao *Breweries* wapewe ilitoka kwa wananchi. Sasa Breweries limekuwa shirika binafsi, naamini kwamba hisa nyingi si za Watanzania, lakini hawa Breweries japo si shirika tena la Serikali wamechukua ile ardhi wamemuuzia mtu bila sisi wenyе ardhi kupewa nafasi ya kwanza ya kununua au kuulizwa kwamba tutaihitaji ile ardhi.

Mheshimiwa Spika, sasa ombi langu ni kwamba, sababu hiyo ardhi ina eneo kubwa ndani ya mji wetu na tunapanga mji wetu. Sasa tuwakilishe ombi maalum na tunawakilisha ombi maalum kwa ofisi ya Waziri Mkuu kusudi hiyo hati miliki ifutwe, tuweze kutumia hilo shamba kwa kupanga mji wetu na kwa matumizi ya wananchi katika Kijiji cha Sigino na katika Kata ya Singu.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuwapongeza wananchi wa Babati Mjini katika hotuba ya Upinzani, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani alisema kwamba, kumeanza kujitokeza ukabila, lakini nawapongeza wananchi wa Babati Mjini sababu hilo tatizo hawana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wa vijijini hawana na wa mjini pia hawana, inaonekana hayo matatizo yako katika

maeneo mengine, lakini wamefanya kazi nzuri wametuchagua sisi Wabunge, nawashukuru sana wa mjini nawahakikishia kabisa kwamba, nitawatumikia kwa moyo mmoja kama ninavyowatumikia. Nitawafanya kazi nzuri na nitatumia uwezo wangu wote kuendelea kuwatumikia kwa manufaa ya Babati Mjini, kwa manufaa ya nchi yetu na kwa manufaa ya Chama chetu cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niendelee kukushukuru sana kwamba siku ya leo umenipa nafasi ya kuchangia wakati muafaka, nimeondoa mzizi wa fitina kwa yule aliyekuwa ananitangaza kwamba siko huko na sasa wamenisikia nimewaongelea, nawatetea na tupo pamoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Kanuni gani? Nyie ndiyo mnafanya hivyo kila siku, ninyi wawili ndiyo akina Mr. Utaratibu. (*Makofi*)

Utaratibu kifungu gani cha utaratibu.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nasimama kuomba Mwongozo wako kwa mujibu wa kanuni 64(g), naomba ninukuu kwa ridhaa yako: "Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge, fasili ya (g) hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ambaye amemaliza kuchangia ametudhalilisha Wabunge vijana wote wa Kambi ya Upinzani ambao tuko ndani, lakini siyo Wabunge tu kwamba wa Upinzani vijana ila ni pamoja na Wabunge vijana wa Chama cha Mapinduzi, kwamba hatujui kufikiri sawasawa na kwamba hatujui lolote ndiyo maana tunachangia changia tu hovyo hovyo. Maneno haya ni ya udhalilishaji namwomba kwa busara Mheshimiwa Mbunge ayaondoe maneno haya ya kuzungumzia kwamba Wabunge vijana hatujui lolote na namtaka akumbuke tunaweza kuwa tunafanya mambo mengi tu kuliko wazee wa umri wao mkubwa japokuwa kwamba umri wetu ni mdogo.

**SPIKA:** Sikiliza Mheshimiwa, utaratibu sasa ni upi uliovunjwa. Maana yake kuhusu utaratibu maana yake lazima useme utaratibu upi uliovunjwa, maana unanihutubia sasa, sijui sasa hata utaratibu ni upi?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nimeomba Mwongozo wako, nimesimama kuomba Mwongozo...

**SPIKA:** Umesema kuhusu utaratibu.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Hapana, nilisema Mwongozo Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie. Kwa hiyo, humu ndani tumekuja wote ni kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umri wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu umri wa kuwa Mbunge ni umri wa kuanzia miaka 21 kwa mujibu wa Katiba. Sasa Mbunge anapozungumza kitu ambacho anajua fika tuko hapa kwa mujibu wa sheria ni kutudhalilisha na inawezekana tutaanza kuhoji pengine uelewa wake na hawatendei haki kwa kweli wananchi wake waliomchagua. Kwa hiyo, tunamwomba afute kauli yake kwa sababu maneno aliyoyatumia siyo mazuri, tuko vijana wengi humu ndani wa Upinzani na wasiokuwa Wapinzani. Lakini pia villevile hata vijana wengine ambao wako mtaani amewadhalilisha sana...

**SPIKA:** Punguza Mwongozo usihutubie watu, *you can take ten minutes* kwa ajili ya mwongozo tu. Maneno uliyo-quote itabidi niyaone kwanza kwenye *hansard* kama ni sahihi. Nitaona kwenye *hansard* ya kwako na kwenye *hansard* ya Chambiri nitayaona. Tunaendelea Mheshimiwa Batenga, nilikuita, hayupo! Anayefuata Mheshimiwa Yahya Kassim Issa na Mheshimiwa Philipa Mturano ajiandae.

**MHE. YAHAYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nasema naunga mkono hoja hii. Sababu ya kuunga mkono hoja hii ninayo; kwa sababu waliioleta hoja hii ni wanadamu na hakuna mwanadamu aliyekamilika. Nakuja hapa ina maana kwamba, la mmoja haliwezi kukamilika kwa hiyo tuchanganye mawazo. Ndiyo maana nasema naunga mkono hoja mia juu ya mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitachangia mambo matatu, Muungano, Vituo vya Polisi Idunga, Chakwa na kuhusu sheria dhidi ya wapiganaji wetu Polisi.

Mheshimiwa Spika, kwanza tutarudi nyuma, napenda kunukuu baadhi ya hotuba ya Waziri Mkuu ya 2008, maelezo yake yanasema kwamba: "Kuratibu mgawanyo wa mapato na pande zote mbili za Muungano. Kufanya utafiti wa mambo ya Muungano na ya siyo ya Muungano kwa lengo la kudumisha Muungano. Pia akasema ili kufuatilia utekelezaji wa makubaliano hayo kwa karibu zaidi vikao vya pamoja vitafanyika kila baada ya miezi miwili chini ya Uenyekiti wa Makamu wa Rais." Mwisho wa kunukuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika 2011/2012, anasema kwamba: "Serikali itaendelea kuratibu vikao vya Kamati ya pamoja na Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kushughulikia masuala ya Muungano." Mwisho wa kunukuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kitabu chetu hiki cha mwaka huu, juu ya hayo yote aliyozungumza lakini anasema kwamba katika hoja 13 zimeweza kurekebishwa mbili. Nachukulia kama asilimia 15 na asilimia 15 natumai hata mtoto akiwa darasa la kwanza, huwezi kumpeleka la pili, kwa uzoefu nilionao. Kwa hiyo, inaonesha wazi kwamba utendaji kwa kweli haukidhi na kama vikao vinafanyika kila mara havileti tija inadhihirisha wazi kwamba mafanikio hayawezi kupatikana. Katika mambo mawili hayainishi kwamba yameleta uzito hususan kwa Zanzibar. Matatizo ya

Zanzibar yanaelewaka na yale yaliyokuwa muhimu kabisa hatuwezi kusema *Constituency Development Catalyst Fund* kwamba ni tatizo ambalo tumeliondoa haiingii akilini.

Mheshimiwa Spika, tunaelewa wazi kwamba kuna mambo ambayo hayo yanatuathiri kama tunavyosema yanayohusu mapato. Hivi juzi katika Kamati, ziko fedha kama bilioni 155 lakini kwa ile hasara ya 4.5 Zanzibar walipata asilimia nane, *eight billions*, hali hii tusitegemee kwamba Wazanzibar wataweza kuleta maendeleo au kupata maendeleo na haya ndiyo mambo ambayo yanaleta matatizo katika Muungano.

Mheshimiwa Spika, tunajua wananchi wetu wanapata matatizo katika kodi, unaondoa jambo lako au biashara yako kutoka Zanzibar ukifika bandarini pana matatizo na siku zote mnasema kwamba tunarekebisha, matatizo tutayaondoa lakini nasema tusiwe wasanii. Tusiwe wasanii juu ya mambo mazito kama haya, lazima tuwe wakweli, tunasema kwamba, tumeweka viongozi ili watekeleze majukumu ya wananchi ndiyo maana yake, lakini nadhihirisha wazi kwamba suala hili limepuuzwa. Niko katika Bunge hili kwa miaka 17, suala hili linapigiwa kelele mpaka leo hakuna kinachokwenda. Hili ni tatizo kubwa sana, ambalo halileti maana hata kidogo. Kwa hiyo, tunaomba hizi ghasia zimalizike na nasema Serikali kwa upande mwingine inachangia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa upande mwingine inachangia matatizo ya wananchi, hakuna Mzanzibar

aliyekuwa hataki Muungano, hakuna na anayesema kwamba labda Mzanzibar hataki Muungano, ndiyo wale walioondoka Zanzibar 1964 labda wakaenda Dubai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa labda wanatafuta njia ya kurejea, njia ipi wapite, mkono upi watumie ili waweze kurejea, lakini hakuna mzawa wa Zanzibar hasa halisi aweze kusema kwamba hataki Muungano si kweli. (*Makofi*)

Kwa hivyo ombi letu, yafanyike marekebisho katika matatizo ambayo yanawakabili wananchi, maana mimi hapa nasema kwa ajili ya Zanzibar, wenzetu sijakusikieni nyie mkatoa sauti ya aina yoyote kama nilikuwa na kijana mmoja wakati ule Waziri Mkuu, unamwambia hivi anaigiliza vizuri kabisa lakini hatekelezi hata moja. Kwa hivyo, inaonyesha ndiyo picha hii mnayotupa wenzetu kimyaal! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini huwezi kupata ufumbuzi *you don't know where is our reluctance*, naendelea.

Mheshimiwa Spika, nakuja kuhusu Vituo vya Polisi. Katika Jimbo langu nina vituo viwili Chakwa na Dunga mitini. Kituo cha Dunga Mitini wakati wowote kinaweza kuanguka na kuua. Kituo ni kibovu sana na suala hili napiga kelele kila mara lakini hakuna hatua zinazochukuliwa. Aliwahi kuja Naibu Waziri wakati ule Mheshimiwa Kagasheki alikuja na tukamtembeza sehemu zote na akaona hali halisi ilivyo, lakini mpaka leo hakuna lililofanyika. Hii ni hatari! Kituo hiki kwa kweli hakina sifa yoyote; kwanza hakina dari, seli hakuna,

kuta zote zimekatika. Kwa ufupi yule Mama ambaye ni Mkuu wa Kituo, Inspekte Mtumwa namshukuru sana kwani anajitahidi sana kwa sababu hata baadhi ya vifaa anajitahidi kutafuta kwa mbinu zake lakini Serikali haichukui hatua yoyote. Hili ni suala baya.

Mheshimiwa Spika, pia ina maana watafute gari za doria kwa njia ambayo haistahiki, ni magari ya kawaida tu ambayo si jambo la busara kabisa. Muda mrefu nalizungumzia suala hili kwamba, vituo hivi vipatiwe gari zao, gari ya *OCD* haisaidii kitu kwani *OCD* wakati mwingine ana matatizo yake, kuna mambo mengine anataka kufuatilia na huku limetokea lingine. Kwa hiyo, naomba wahusika mtusaidie ili tuweze kufanikisha masuala haya. Kituo cha Chwaka kiko kiamboni kabisa yaani kijiji kabisa, kimezingirwa na kijiji, Kituo cha Polisi hakiwezi kuwa katikati ya kijiji, haimkiniki. Nyumba kwa kweli hakuna, wanalala katika mazingira magumu kabisa, huamini kwamba hapa kalala binadamu na watoto wake, mambo mengine hayastahiki kuyasema.

Mheshimiwa Spika, dakika zangu nafikiri walizila wakati ule.

**SPIKA:** Haya, ahsante. Haiwezekani! Mheshimiwa Philipa Mturano.

**MHE. PHILIP A. G. MTURANO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijafika kwenye mada yenye kwanza napenda niwapongeze Mawaziri wote waliochaguliwa, lakini kwa dhati kabisa niwapongeze Mawaziri wanawake kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kwamba hakuna hata mmoja aliyeondolewa, wameendelea kwenye nafasi zao kama kawaida na hata walipobadilishwa lakini wamebaki kwenye Baraza. Wale ambao hawakuendelea basi karibu kundini.

Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru kwa Serikali kuamua kurudisha JKT, lakini naomba hii JKT isielekezwe tu kwa vijana kwa sababu hata watu wengine wanahitaji kuwa wazalendo, wanahitaji kuwa na nidhamu katika kazi na katika maeneo mbalimbali. Napendekeza mtindo uliokuwepo zamani kwamba mtu hawezi kupata ajira mpaka awe na cheti cha JKT, hatukuweza kuajiriwa sisi mpaka tulipokuwa na vyeti vya JKT. Watu wazima waliokuwa maofisini waliondolewa maofisini wakapelekwa Jeshi la Kujenga Taifa, tumehenya mwaka mzima. Kwa hiyo, kama kuna mfanyakazi yeote ambaye atakuwa hajapitia JKT haijalishi umri wake na yeche apite JKT ili ajifunze uzalendo wa nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tumesikia kwamba kuna fedha ya rada imekuja na itatawanywa katika mikoa minne ili kununua madawati. Naomba pesa hii ipelekwe katika mikoa yote ili tugawane kidogo kidogo kwa sababu pesa hii imetokana na kodi za Watanzania wote. Kwa kuwa, katika mikoa yote karibu Halmashauri zote zina upungufu wa madawati, basi tugawane kidogo kidogo kasungura haka ili wote tufaidi hii pesa ya Rada. Lakini

pia tuambiwe wahusika wamechukuliwa hatua gani kama vile wengine wanavyochukuliwa hatua na wao tuambiwe wamechukuliwa hatua gani.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye suala la Walimu wamekuwa wakitishia kufanya mgomo hivi karibuni kwa ajili ya kudai stahiki zao. Katika hotuba ya Bajeti ya mwaka 2012/2013, ukurasa wa 14 aya ya nne Serikali imesema kwamba, Wizara ya Fedha ilitoa shilingi bilioni 44 kama malipo ya Walimu. Lakini kwenye randama ya hotuba ya Waziri Mkuu wanasema kwamba ni bilioni 19.2, tunapenda kufahamu ni ipi iliyo sahihi? Pia ingesaidia kama tungefahamu hao Walimu waliolipwa ni akina nani kwa idadi yao na kwa majina ili waweze kujitambua, isije ikawa unatokea ujanja ujanja kwa sababu kuna baadhi ya watu ambao wanataka kujinufaisha na hilo.

Mheshimiwa Spika, nikizungumzia suala la msongamano wa Mahabusu Magereza. Hili limekuwa ni tatizo kubwa hasa kwa Magereza yaliyopo Mkoa wa Dar es Salaam. Hili nimeliona katika Magereza ya Keko na Segerea. Msongamano ni mkubwa sana na kama ilivyoelezwa jana na Mbunge mwenzangu aliyechangia, chumba kidogo kinalazimika kuwa na watu wengi tena wanachanganywa. Yanayotokea hapo ni mengi sana na sina haja ya kuyaeleza kwani yanaeleweka lakini itambulike kwamba hao watu mwisho wa siku baada ya kifungo wanarudi katika jamii. Kuna watu wanakuwa wameathirika kisaikolojia na wengine pengine wamepata magonjwa, wanaporudi kwenye jamii wanakuja tena kuleta matatizo mengine.

Mheshimiwa Spika, ningependa hili nalo lishughulikiwe, waangaliwe wale wenyewe makosa madogo madogo wapatiwe adhabu nyingine na si lazima kuwepo Mahabusu. Kwa sababu haiwezekani mtu amekwapua simu au ameiba kuku, *though* ni kosa lakini akakaa huko miaka miwili au mitatu wakati upelelezi unaendelea. Napenda hili lishughulikiwe.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba nizungumzie suala la wizi au uharibifu wa miundombinu katika Mkoa wa Dar es Salaam. Juzi nimelizungumza kwa kuuliza swali kwa Waziri, akanijibu lakini dukuduku langu halijakwisha, hili nataka Waziri Mkuu alisikie. Watu wa DAWASCO na DAWASA wamejitahidi sana kuweka mifuniko ya kuzuia mashimo ya maji taka, lakini kumetokea wajanja wachache wanachukua ile mifuniko wanapeleka wanakojua wenyewe. Mashimo yaliyopo Dar es Salaam yanatisha na viongozi walio wengi wanaishi Dar es Salaam na siyo kwamba walio wengi bali ni karibu wote tunaishi Dar es Salaam. Maeneo ya Posta na hata Upanga Kambi ya Jeshi mifuniko imeng'olewa, ukipita na gari unaweza ukatumbukia shimoni kama ni usiku na wakati mwingine hata mchana unatumbukia, utaweza kuvunja mguu au kupinduka.

Mheshimiwa Spika, tunataka kujua, kwanza hii mifuniko ni mizito sana, huyu mtu anawezaje kuinyanya yeye peke yake? Tunaomba uchunguzi ufanyike, kwani hapa kuna kitu kwenye vyuma chakavu, ule mfuniko ni mzito sana, mtu mmoja hawezи kuunyanua. Tunaomba uchunguzi ufanyike.

Mheshimiwa Spika, nikija upande wa elimu, kwanza na-*declare interest*, mimi nilikuwa Mwalimu na ni Mwalimu mpaka sasa, nasikitika sana kuona kwamba kuna wanafunzi ambao wamekwenda sekondari wasiofahamu kusoma wala kuandika. Nashangaa hii *selection* ilikuwa ni ya aina gani. Lakini ushauri wangu ni kwamba, naomba kama siyo lazima hakuna haja ya *second selection*, ni afadhali tupeleke wanafunzi wachache wenyewe uwezo kuliko tunapeleka wanafunzi wengi ambao hawana uwezo eti tu ili mradi tujaze shule zetu au tupate sifa kwamba tumefaulisha wanafunzi wengi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nataka nizungumzie kidogo kuhusu ulinzi na usalama. Katika Mkoa wa Kigoma mimi pia ni mwenyeji wa Kigoma na Wilaya ya Kibondo, mimi ni Muha. Mwezi uliopita nimenusurika kutekwa nikiwa kwenye gari langu, baada ya kupita ndani ya robo saa *Land Cruiser* ilikuwa inafuata watu walitekwa barabara ya Kibondo; kutoka Kibondo unakuja Dar es Salaam au Nyakanazi, *Land Cruiser* ilitekwa.

Mheshimiwa Spika, niliwahi kuongea na Mkuu wa Mkoa wa Kigoma kwenye Bunge la Bajeti Mheshimiwa Simbakalia kwamba labda sijui itumike mbini gani au labda tuombe Jeshi la Wananchi lifanye doria pale. Lakini tunaomba doria izidishwe kwani mimi binafsi naona Polisi wamezidiwa, pale vitendo vyatukaji vimekithiri sana kwani pori lile ni kubwa na inawezekana kuna hawa wenzetu kutoka nchi jirani ndiyo wanaojipenyeza yaani Burundi na Rwanda na

inaeleweka. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ilifanyie kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, linge kabla sijasahau ni suala la wauguzi. Tunatambua kazi yao ilivyo ngumu hasa Manesi ambao wanatusaidia akinamama kujifungua. Tunatambua kazi yao ni ngumu na tunaomba maslahi yao yaendelee kuboreshwa siku hadi siku. Lakini, masuala ambayo baadhi ya Manesi wanayafanya siyo mazuri na hayawezi kuvumilika hata kidogo. Wamekuwa na lugha ambazo si nzuri kwa akina mama wanapokuwa wanakwenda kujifungua na vitendo vyao vinakuwa si vizuri. Kati ya tarehe 18 mpaka 22 mwezi Mei katika Hospitali ya Amana Manesi walisababisha...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana nashukuru. Mheshimiwa Salum Barwany atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine na mwisho atamalizia Mheshimiwa Ngonyani.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nichukue nafasi hii kwa niaba ya Vyama vya Watu wenye *Albinism* katika Taifa hili kukupongeza wewe na kutoa shukrani zetu za dhati kabisa kwa kukubali kwako kuwa mgeni rasmi kwa maadhimisho ya sita ya siku ya wale mavu wa ngozi Tanzania. Kukubali kwako kumetufariji sana na pia zili kuwa taarifa za ghafla kwako lakini nasema ulijali na pia ultufikia kwa wakati muafaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mtu mzima akitoa machozi mbele ya watu inafaa watu wakakaa wakazingatia. Leo asubuhi Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegir chozi lake ambalo alilitoa katika jumba la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kudhihirisha dhahiri kabisa kwamba Maalbino katika Taifam, hili wameshapoteza matumaini ya kuishi kwa amani ndani ya Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba, jukumu la Bunge ni kuisimamia Serikali na mauaji bado yanaendelea kufanyika katika nchi hii. Hivyo ni jukumu la Bunge sasa kama msimamizi mkuu wa Serikali baada ya Serikali kushindwa kudhibiti mauaji kutoa tamko au Bunge lipate maelezo ya kutosha kutoka kwa Serikali kwa nini mpaka leo mauaji ya *Albino* yanaendelea kuwaathiri katika Taifa letu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu sasa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano, Mikoa ya Kusini inatajwa sana tofauti na awali, kila Mbunge anatoa shukrani zake kwamba Taifa limepata uchumi imara, Taifa sasa litaneemeka kwa sababu tayari kusini imepatikana gesi, gesi ambayo inasemekana kutakuwa na utajiri mkubwa katika Taifa hili. Lakini wenzangu wanatafunatafuta maneno hawasemi wazi, hebu niwaambie Wabunge wenzangu kwamba wananchi wa Mikoa ya Kusini hawapo tayari kuiona gesi yao inatoka Kusini kuja huku bila wao kufahamu wana maslahi gani ndani ya gesi hiyo. Hizi ndiyo salamu za wananchi wa Kusini.

Mheshimiwa Spika, tumeona rasilimali na uchumi wa Taifa hili ambao umefika katika mikono isiyo

salama, Serikali hii imeshindwa kuwanufaisha wenyewe katika maeneo husika. Hili siyo mzaha tena kwani tumeathirika sana kiuchumi katika Taifa hili hususan katika Mikoa ya Kusini. Kupatikana kwa gesi hii tumeona ni ukombozi kwetu, lakini tayari tunaona dalili za wazi kabisa ambazo zimejitokeza kwamba yale matarajio ya wananchi wa Kusini juu ya gesi hii hayaonekani kwa karibu. Tumeona katika vyombo vya habari juzi yanazungumzwa hapa kwamba mamilioni ya shilingi yamekamatwa katika mabenki ya Uswisi yakinasibishwa na upatikanaji wa gesi hiyo. Sasa huo ndiyo mwanzo tu.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu kwamba, tayari katika dunia nzima machafuko na migogoro inayotokana na kutokuwa na mgawanyo katika nchi hizi. Naamini kabisa kwamba matokeo mabaya yatakayotokea katika nchi hizi ni kule kutokuwa na mgawanyo rasmi wa rasilimali katika nchi hii. Mikoa ya Kusini tumeshiriki katika utumwa wa nchi hii miaka mingi, ni mikoa ambayo tayari inatoa mchango katika Taifa hili kwa zao la korosho ambalo ni zao la tatu katika utoaji wa mchango mkubwa katika Taifa hili, lakini baada ya miaka 50 ya uhuru hatuoni mafanikio ambayo yalipatikana kupitia zao la korosho.

Mheshimiwa Spika, ukanda wa Mtwara na Masasi kupitia Tandahimba na Newala ni ukanda ambao unatoa korosho za kutosha lakini nenda kawaangalie wananchi wa Tandahimba wanavyoishi katika mashaka na umaskini uliokithiri. Huwezi kukubali kwamba Mkoa wa Mtwara ambao unatoa zao la korosho kwa kiasi kikubwa hawana barabara ya lami,

hawana maji ya uhakika, hawana hospitali ya uhakika katika maeneo wala hawana maji ya uhakika. Tunaamini kabisa kwamba mapato yatakayotokana na gesi hayatakuwa na tofauti kabisa na rasilimali ya korosho ambayo tumeipata katika Mikoa ya Kusini. Wenzangu wanatafuna maneno, lakini nimeagizwa kabla sijaja katika Bunge hili, nimepita katika Wilaya zote wameniagiza kwamba Serikali ni lazima itafute jawabu la msingi kabisa la kuwaambia wananchi wa kusini kwamba, kwanza hata kaabla sera ya gesi haijatengenezwa, Serikali imeshaanza kuweka mikataba ya kinyemela, tunataka mikataba hiyo ije Bungeni na tuione ili tuweze kujiridhisha kama mikataba hiyo itakuwa na maslahi kwetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye Jimbo langu la Lindi Mjini. Tarehe 1 Julai, 2010, Serikali ilitangaza rasmi kwamba Jimbo la Lindi Mjini ni Manispaa likiwa na Kata 13, lakini baada ya kutangazwa rasmi kuwa Manispaa tukawa na Kata 18 yaani ongezeko la Kata tano. Kuonesha udhaifu wa Serikali katika maeneo yetu tulienendelea kupata ruzuku ya Kata 13 zile zile hata kama kuna zaidi ya Kata tano zilliongezeka.

Mheshimiwa Spika, ndani ya bajeti mbili, bado tunapata ruzuku ya Kata 13 wakati huo huo Lindi ni Manispaa ambayo tayari tuliambiwa kwamba kupatikana kwa Manispaa kutakuwa na maendeleo makubwa, lakini tunaona *cealing* ile ile ambayo ilipatikana ndani ya Kata 13, bado inaendelea kuwa katika Kata 18 ambazo tayari nyingine zimetolewa katika Halmashauri ya Wilaya bila ruzuku yake kuongezwa katika Manispaa ya Lindi. Hili linatukatisha

tamaa kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi haiko tayari kuona kwamba inanufaisha maeneo ambayo tayari walitangaza katika ilani yao kwamba itatumia nguvu kubwa kuhakikisha kwamba maeneo ambayo yapo nyuma kiuchumi yanapewa kipaumbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo yanatupa mashaka ndani ya Serikali hii, tuna mambo mengi ya msingi ambayo tulitarajia kwamba baada ya kupatikana kwa Manispaa ya Lindi tayari wananchi wa Lindi wataboreshewa maisha yao, lakini bado hali ni tete mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, tuna hospitali ya Sokoine ya Lindi ambayo ipo kabla ya Uhuru, naamini kwamba ndani ya uhuru huu tusingepata hospitali ile ambayo ilikuwa na majengo mazuri, lakini leo tunashuhudia jinsi gani hospitali ile ilivyodorora katika kutoa huduma zake. Hospitali ambayo tunaambiwa leo ni hospitali ya rufaa haina Daktari Bingwa hata mmoja, haina *x-ray*, haina Madaktari, haina watu ambao tayari tunaamini kwamba wanaweza kuwatumikia wananchi katika kuwapatia tiba. Hayo ndiyo matatizo ambayo tunakumbana nayo na kuwafanya wananchi wa Lindi kutokuwa na imani na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, stakabadhi ghalani. Inasikitisha tunapokaa hapa tunaona ni watu gani ambao wanaona kwamba, stakabadhi ghalani imewaletea maslahi wananchi, ni viongozi wa Serikali tu, lakini sijamsikia mwananchi anasema kwamba stakabadhi ghalani inamletea manufaa, ni watu ambao bado

hawajaona manufaa ya stakabadhi ghalani. Wakulima wa korosho ni wakulima wa daraja la chini. Amepata kiasi kikubwa ni gunia tatu au nne au tano, anakipesha zaidi ya miezi sita hajalipwa, anataka kutoa huduma kwa kupeleka watoto shuleni, anataka kuandaa mashamba yake, lakini ndani ya miezi sita mkulima huyu hajalipwa. Hivyo, inafikia mahali kwamba, mtu ambaye unamsikia kwamba stakabadhi ghalani imewasaidia wakulima ni mtu ambaye hana mkorosho na wala hategemei mapato kupitia mkorosho.

Mheshimiwa Spika, hivyo, nasema kwamba wale ambao wanasema stakabadhi ghalani imewasaidia wakulima, nasema stakabadhi ghalani haijawasaidia wakulima. Wakulima wa Tandahimba, Newala, Nachingwea na Liwale wanansikia hapa na naamini kabisa wanaunga mkono kauli yangu. Tusiite stakabadhi ghalani ili tuweze kuleta manufaa kwa wakulima wetu, tuseme malipo ghalani, malipo yawe ghalani na siyo stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nizungumzie Halmashauri zetu. Hivi sasa tayari kuna ukiritimba wa mabenki ambayo yanafanya kazi pamoja na Halmashauri, Halmashauri tayari wana uhusiano wa karibu kabisa na *NMB* ambayo tunaamini kabisa kuna ubadhirifu mkubwa wa fedha za wananchi. Pia kuna Halmashauri ambazo tayari hazina Uhuru, wanaamua kwenda katika Benki yoyote ambayo wanaweza kuweka fedha zao na kuzifanyia kazi.

Lakini kutokana na ukiritimba wa Serikali wanalazimishwa kwamba fedha zile wazipeleke *NMB*. Kuna mabenki ambayo tayari yana uwezo wa kutoa riba ambazo zingesaidia kuongeza mapato ya ndani ya Halmashauri zetu. Naishauri Serikali ushauri wa bure kabisa kwamba, Halmashauri wapewe uhuru wa namna gani wanaweza kuweka fedha zao katika benki ambazo zinaweza kutoa riba na kuwaletea maendeleo wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, nasema siungi mkono hoja.  
(*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilipokwenda kwenye sherehe ya siku ya *albino* wana maelezo mazuri sana. Tunawaona wenzetu lakini hatuwafahamu. Kwa hiyo tulikubaliana kwamba tukipata muda watakuja kutoa semina ili tuwaelewe wenzetu walivyo.

**MHE. STEVEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona na kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia, kwanza naomba niwashukuru wapiga kura wangu wa Korogwe Vijiji ni kwa kuniombea kwa muda mrefu nikiwa mgonjwa na hadi leo nimerudi tena Bungeni nikiwa na nguvu nyingi. Mungu awabariki sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vilevile nisiache kumpa pole Mwenyekiti wangu wa Halmashauri ya Korogwe Mjini ambaye alipata ajali mbaya sana juzi na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Korogwe Vijiji pamoja na Meya wa Mji wa Tanga. Sasa hivi ninavyozungumza wako Moshi wamelazwa katika Wodi ya mifupa na sijui kama

wanatibiwa      ukizingatia      kwamba      Madaktari  
wamegoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na nzuri sana aliyoifanya ya kuwateua Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wapya, hasa Mkuu wangu wa Mkoa wa Tanga ambaye amenifanya siku hizi hamnioni nikisimama na kulalamika kuhusu mambo ya mkonge. Mkuu wa Mkoa alituita tukajadili, tukashauriana na sasa mkonge kule tunauona una thamani kubwa sana. Mungu ambariki kwani sikutarajia kwamba haya yangefanyika, lakini vile vile amefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile nisiache kumshukuru Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, mama Sitta. Wakati nikiwa mgonjwa kila siku alikuwa anakuja hospitali kunipa matumaini kwamba nitapona. Mungu ambariki sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye Kilimo Kwanza. Narudi kwenye Kilimo Kwanza kwa sababu katika eneo letu la Mkoa wa Tanga tumezungukwa sana na mashamba ya Mkonge ambayo hayaendelezwi. Ukizingatia kwenye Jimbo langu la Korogwe Vijijini nina mashamba 15 ya mkonge na matatu (3) ya chai. Kwa , hiyo, jumla nina mashamba 18. Sasa kati ya hayo kuna mashamba ambayo hayaendelezwi. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu zile hati ambazo ziko mezani ambazo zinatakiwa kufutwa, ifanywe haraka zifutwe mara moja ili tuendeleze huo mradi wa Kilimo Kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu unapomwambia mkulima kuhusiana na mradi wa Kilimo Kwanza ni lazima awe na maeneo ya kutosha ya kulima na kujipatia riziki yake kwa kupanda mazao ya biashara na chakula. Sasa naomba haya, kwa sababu tuliambiwa hati ziko mezani kwa Mheshimiwa Rais na sisi watu wake na wanavijiji huko wanalia, basi, aangalie sana haya mashamba ambayo hayaendelezwi, hati zifutwe ili wananchi wetu waendeleze kilimo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vilevile katika Jimbo langu kuna huu utaratibu uliokuja wa mamilioni ya JK. Wananchi wangu wa Jimbo la Korogwe Vijijini hayo wanayasikia tu kwenye redio. Hawajawahi kuona hata mara moja na wala hawajui zinakwenda wapi. Kwa hiyo, kama kweli huo mradi upo basi ufutwe na itafutwe namna ambayo wale vijana, akinamama, wazee walioko vijijini kabisa ambao wanaweza kuendeleza miradi hii wajue ni wapi wanakwenda kuzichukua na watazirudisha namna gani, kuliko huu mradi kuingia kwenye miji tu na wanapewa wale watu wenye fedha, wale maskini kabisa hasa wa Korogwe Vijijini hawana msaada wa aina yoyote ambao wanaupata. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka nilisemee ni maji. Maji imekuwa ni kero kubwa sana, ingawa namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu jana kabla sijakuja kuchangia amenieleza hali halisi na nimefurahishwa sana kuona kwamba Mkoa wangu wa Tanga na yale mambo madogo madogo ambayo nilikuwa nayataka yote ameyapa kipaumbele. Kwa

hiyo, naunga mkono hoja mia kwa mia mia kweli kweli.  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna kitu ambacho kinanikera sana, hili suala la dharura ambalo limejitokeza jana, suala la Ulimboka ambalo limefanya hata mimi mwenyewe nimeshangaa Madaktari. Madaktari wamegoma kwa misingi kwamba hawatamhudumia mtu yejote kwa sababu hawakuelewana na Serikali. Kitendo hiki ni dhambi kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu wanachokifanya siyo kutukomoa sisi, wanawakomoa watu wadogo walioko kwenye...

**SPIKA:** Mheshimiwa Ngonyani!

**MHE. STEVEN H. NGONYANI:** Naam.

**SPIKA:** Hili suala liko Mahakamani. Tulishakubaliana asubuhi kwamba hatutaliongelea. Naomba tafadhali, hili suala liko Mahakamani.

**MHE. STEVEN H. NGONYANI:** Basi na yeye wasimtibu.

**SPIKA:** Aaah, hapana huwezi kuzungumza!

**MHE. STEVEN H. NGONYANI:** Wasimtibu Mheshimiwa Spika. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ngonyani, kwanza unatakiwa ukae nikisimama.

**MHE. STEVEN H. NGONYANI:** Sawa Mheshimiwa.

**SPIKA:** Kwa hiyo, endelea na mjadala mwingine, hilo liache. Lakini siku nyingine nikisimama wewe unakaa. Haya sasa endelea. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. STEVEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, samahani sana. Unajua ukiugua unachanganyikiwa kidogo ndani ya akili. Unajua licha ya kuugua pia nilitangaziwa kifo kwamba nimefariki. Sasa labda hiyo inanifanya pia nakuwa na *stress*. Kwa hiyo, pole sana.

**SPIKA:** Ndiyo maana nimekupa nafasi uzungumze...

**MHE. STEVEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kuna suala la maji kutoka Mkoa wa Kilimanjaro kuja Mkoa wa Tanga hususan katika Wilaya za Same, Hedaru, Mombo hadi kufika Korogwe. Huu mradi naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu tuuangularie na kama upo naomba utekelezwe haraka kwani Wananchi wa Korogwe wanapata sana shida ya maji na hasa ukizingatia kwamba tumeptitiwa na mradi wa majisafi pale, lakini hatuwezi kuyapata. Naomba sana hili suala liangaliwe kwa hali na mali kwa sababu ni kero kubwa inayowasumbua wakazi wa Korogwe Vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la elimu umeshaniambia na mimi nakuunga mkono na sitataka kuchangia sana kwa sababu niliyokuwa nataka kuyachangia, jana umeniambia ana kwa ana kwamba umenisaidia. Nikiwa hospitali umekuja kuniona, nilichokuwa nataka ni kukupongeza kwa kutuletea Mkuu wa Mkoa na

Mkuu wa Wilaya ambaye anatupa matumaini kwamba, safari hii Mkoa wa Tanga tutapanda bei kwa ajili ya zao la mkonge. Naomba wakulima wa mkonge wasipangiwe mtu wa kununua mkonge. Popote watakapoona kuna bei ambayo wanaridhika nayo waende wakauze tu huko badala ya wao kuwa wanaambiwa kwa sababu ni wakulima wadogo washikwe na wanaposhikwa wanakuwa hawana faida na mkonge. Huu mkonge ni sera ambayo tulishasema kwamba safari hii ni mwaka wa kupanda mkonge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu hii mikataba ya mashamba ya mkonge. Mashamba ya mkonge mikataba yake inapokuwa inapitiwa basi watafutwe watu ambao wataipitia na isitokee tu wachache waamue kwamba, mikataba ifanyike. Hili limejitokeza na inakuwa kero kubwa sana kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili, nimeona pale Hale *TANESCO* kwamba panajengwa. Korogwe nako pajengwe na uzuri ni kwamba Mkoa wa Tanga sasa hivi umeme unakatikakatika sana. Nashangaa mikoa mingine ambayo haina vituo hivyo vyta umeme, umeme haukatiki. Kwa nini Mkoa wa Tanga umeme unakatika wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu umeshanipa matumaini kabisa kwamba kila kitu kitaendelea vizuri? Naomba huyu bwana ambaye ametupa matumaini kwamba atashughulikia masuala ya *TANESCO* aangalie kilipo kiini cha umeme, lakini hakuna umeme. Wananchi wanapata shida, hawana maabara, hospitali hakuna dawa, Madaktari ni wachache katika

Kata na Vijiji vyetu. Haya ndiyo baadhi ya mambo ambayo tunayaomba sana kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika mjadala wake wowote na haya ayaweke ndani kabisa mia kwa mia ili na sisi tukizunguka Mkoa wa Tanga tuonekane.

Mheshimiwa Spika, safari hii sitachangia sana, nangoja hizo Wizara nyingine. Namuunga mkono mia kwa mia Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makof*)

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa napenda kuipongeza Serikali kwa kuja na bajeti ambayo tunaamini ikifuatwa vizuri na kama walivyoahidi kwamba katika sehemu mbalimbali watajaribu kubana matumizi na kufuata utaratibu wa matumizi ya fedha, tunaamini tutasonga mbele na tutaweza kupata maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuchangia katika suala la kuongeza posho ya Madiwani. Ni ahadi ya siku nyingi naipongeza Serikali kwa kufanya hivyo. Lakini pia naomba waangalie namna ya kuangalia pia viongozi wengine amba ni muhimu; Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Vitongoji pamoja na Mabaraza ya Ardhi. Naamini kwamba tukijipanga vizuri tutaweza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia napenda kuikumbusha Serikali kuhusiana na suala la kodi katika vipuri vyta Matrekta. Tulikwishapitisha mwaka jana katika bajeti kwamba iondolewe lakini hadi leo hii haijatekelezwa. Lakini pia tunaomba Serikali iangalie

namna ya kuondoa kodi katika matairi ya trekta, trela za trekta na pia katika vipuri vyatya vyombo vyatya umwagiliaji. Serikali pia iangalie namna ya kuboresha mfumo mzima wa kufikisha pembejeo nchi nzima ili wakulima waweze kupata pembejeo kwa muda muafaka na suala la kuchakachua lisiwepo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia naipongeza Serikali kwa suala la matrekta kupidia SUMA JKT. Serikali imekubali kuondoa ule uchangiaji wa asilimia 50 wakati unataka kununua trekta na kuipunguza kuwa asilimia 30 na ule muda wa kulipa lile deni badala ya miaka miwili kuongeza kuwa miaka minne(4). Nawapongeza kwa hilo na naamini wakulima wengi zaidi sasa watanufaika kutokana na hayo matrekta. Tunaomba Serikali iangalie katika maeneo ambayo hayo matrekta bado hayajafikishwa, basi utaratibu ufanywe ili yaweze kufika katika maeneo yote na haya matrekta yafanye kazi ili kuleta tija. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika suala la Jimbo la Babati Vijijini, kuna migogoro ya ardhi. Tunaomba Serikali iangalie namna ya kutatua hii migogoro ambayo ni ya muda mrefu na ambapo wananchi wengi wameshapoteza maisha na wengine kupoteza mali zao na wengi sasa hivi wanakaa bila kujua hatima yao kwamba watafanyaje. Serikali ilikwishaunda Tume, tunaomba hiyo Tume itoe taarifa yake vizuri ili hilo tatizo la ardhi litatuliwe hasa katika Bonde la Kiru, pia katika kijiji cha Mwada na wananchi ambao wanazunguka eneo la Tarangire katika vijiji ambavyo ni jirani na Tarangire kule Mamire, Gidajabong, Ayamango na Gedamari. Wananchi wa maeneo haya wanaishi kwa

mateso. Wapatiwe eneo mbadala na wamekwishakubali kuondoka, lakini wapatiwe maeneo mbadala ili wao pia waweze kuishi kwa amani kama Watanzania wengine.

Mheshimiwa Spika, pia tulikuwa tunaomba ahadi zile za Serikali zitimizwe; daraja la Mto Magara Serikali iliahidi kulijenga na ilishatenga fedha lakini hatuoni dalili zozote hadi leo hii kuhusiana na kujengwa kwa daraja hilo.

Mheshimiwa Spika, pia suala la umeme, tunaitaka Serikali iongeze fedha zaidi katika Mfuko wa Umeme Vijiji (REA) ili umeme uende kwa kasi zaidi vijiji ili kukuza maendeleo. Tunaomba mfuko huo uboreshwe zaidi. Tulikuwa tunashauri *TANESCO* ikubali katika maeneo ambapo nyaya za umeme zinapita juu katika baadhi ya maeneo ni ule uunganishwaji tu na gharama ndogo, ikubali kukopeshwa na wananchi ambao wanaweza kukopa kutoka *SACCOS* au *VICOBA* ili wafungiwe umeme. Halafu baadaye hiyo fedha irejeshwe kwa kukatwa katika ankara ya bill ili wananchi wale waweze kurudisha hizo fedha katika *SACCOS* na *VICOBA* mahali ambapo watakopa. Lakini pia tunaomba katika maeneo ambayo umeme ni muhimu sana na tunaweza kuongeza uzalishaji kwa sehemu kubwa umeme katika Kata ya Riroda, Magara, Mamire, Endakiso, Dabili na Maidunga, ufanyiwe namna uende haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tulikuwa tunaomba Serikali iangalie suala la *VICOBA*. Tunaipongeza kwa kuanzisha *SACCOS* na *VICOBA*, ndiyo mkombozi wa

wananchi, lakini *VICOBA* haiko kisheria. Tunaomba sheria hiyo itungwe haraka iletwe hapa ili *VICOBA* viweze kutambuliwa kisheria na rasmi ili hizo fedha ambazo zinakaa tu vijiji ni ziweze kuwekezwa katika taasisi za benki na *VICOBA*, hivyo viweze kukopa kutoka benki na waweze kusaidia hao wananchi. Tunaomba hicho kitu kifanywe kwa haraka kutokana na umuhimu wake.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu mbalimbali ndani ya Wilaya yetu kuna matatizo makubwa ya afya. Tulikuwa tunaomba Serikali iendelee kuboresha huduma ya afya kwa kuongeza huduma katika hospitali ya Dareda na kuiingiza hospitali ya Bashneti katika mfumo wa kupata ruzuku kutoka Serikalini kwa sababu inahudumia zaidi ya eneo la Babati na inahudumia pia Wilaya za jirani. Pia tulikuwa tunaomba ile ahadi ya kupatiwa gari la wagonjwa itimizwe ili liweze kuhudumia wananchi ambao wako vijiji.

Mheshimiwa Spika, muhimu kuliko yote Serikali iangalie namna ya kuboresha kilimo kwa sababu ndiyo mkombozi wa Watanzania walio wengi. Tulikuwa tunaomba fedha nyingi zaidi zitakazowekezwa katika Mfuko wa Pembejeo na *TIB* zipelekwe vijiji badala ya kukopeshwa watu wachache wenye uwezo. Hao wenyewe wanaweza kukopa hatia katika taasisi zingine, lakini hasa hizi *SACCOS* na *VICOBA* na vyama vya msingi ndivyo vikopeshwe fedha zaidi ili viweze kukuza kilimo katika maeneo mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia tulikuwa tunaomba Serikali iangalie suala nililosema la uanzishwaji wa mabonde

mapya. Ni muhimu sana, lakini pia yale mabonde ya zamani yaliyopo ndiyo yangeendelea kuboreshwa kwanza hasa katika maeneo mfano ya Babati ambapo tunazalisha karibu asilimia 80 ya mbegu ambayo inazalishwa Kanda ya Kaskazini. Maeneo haya yangeboreshwa ili badala ya kutegemea mbegu kutoka nje ya nchi tungeweza kuzalisha mbegu ndani ya nchi yetu hapa hapa. Mbegu ambayo itakuwa ya Kitanzania, badala ya kutoa ruzuku sasa hivi kwenda nje ya nchi kutokana na mbegu kuagizwa nje. Ruzuku hiyo itaendelea kubaki ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya kilimo na ufugaji, Serikali ingeangalia uwezekano wa kuwa na mpango maalum wa kusaidia wafugaji kwa kujenga mabwawa na majosho katika maeneo ambayo wafugaji wanatoka. Migogoro ya ardhi na uhasama kati ya wafugaji na wakulima itaondoka kama wale wafugaji wataweza kuondokana na ufugaji ule wa kuchunga na kuwa wafugaji bora. Katika maeneo ya Mkoa wa Manyara ambapo wafugaji wengi wanatoka, tungeomba Mabwawa yachimbwe katika maeneo mbalimbali. Pia katika Mkoa wa Manyara kuna masuala mbalimbali ya kuboresha kwa mfano, hospitali ile ya Hanang pale Katesh ingeendelea kuboreshewa huduma na pia mabwawa mengine yangechimbwa katika maeneo ya Hanang ambayo sehemu kubwa ni ya ufugaji.

Mheshimiwa Spika, kuna lugha ambazo zinatolewa hapa, tulikuwa tunaomba tuweze kupata takwimu sahihi. Kwa mfano, jana kuna mchangiaji mmoja alisema kuna wafanyakazi karibu laki nne

(400,000) katika mashamba ya *NAFCO*. Sasa nilishindwa kuelewa kwa sababu naamini katika Serikali yenewe wafanyakazi hawafiki hao laki nne. Sasa kama mashamba ya *NAFCO* wana watu laki nne, walikuwa wanaishi wapi, wanafanya kazi gani kwa sababu Hanang yenewe haina watu laki nne? Kwa hiyo, tunaomba maneno mengine ambayo yanasemwā tusiwe tunayasema kwa ajili ya kufurahisha watu, bali tuseme kwa kutoa takwimu ambazo ni sahihi. (*Makofī*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza Kiongozi wa Kambi ya Upinzani aliposema suala la vyama mbalimbali kuingia katika malumbano hasa katika ubaguzi wa rangi, dini, ukabila na aliitaja Babati. Nashukuru kwamba alitambua baadhi ya viongozi katika eneo langu wanavyofanya ubaguzi dhidi yangu kutokana na rangi yangu, ukabila au dini yangu. Namshukuru yeye kukemea suala hilo na kwamba liishe ili Watanzania tuweze kuishi kama Watanzania wote. Nampongeza kwa hilo. (*Makofī*)

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tunaiomba Serikali iangalie namna ya kuboresha *Procurement Act*. Leo hii zile Kanuni bado hazijaja huko katika Halmashauri zetu. Hizo kanuni ziletwe mapema kwani nia na lengo la kuibadilisha hiyo *Procurement Act* na kuiboresha ilikuwa ni kuhakikisha fedha zinatumika vizuri zaidi ili Watanzania waweze kupata maendeleo. (*Makofī*)

Mheshimiwa Spika, lingine muhimu lilikuwa ni suala la *PPP*. Ningeomba Serikali kwanza kabisa kabla ya kutoa haya maneno kwa wananchi ingekaa, Wizara

zote zipate elimu kuhusiana na suala la *PPP*. Wao wakiishaelewa ndiyo waje kwetu watufundishe ili suala la *PPP* liweze kuleta maendeleo. Naishukuru Serikali na nawapongeza kwa jitihada zote hizi. Tutaendelea kuchangia katika maeneo mengine. Ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani tumefikia ukomo wa wakati wetu. Dakika tano haziwezi kuruhusu watu wengine kujadili. Kwa hiyo, kwanza kabisa naomba kesho Waheshimiwa Wabunge muweze kuja na vitabu *Volume III* ambayo inahusu *Public Expenditure Supply Votes (Regional)*. Halafu mje na *Volume IV* ambayo inahusu *Public Expenditure Estimates Development Votes*. Kwa hiyo, hivi vitabu mkiishaleta vinabakia hapa mpaka tutakapomaliza kazi yetu mwezi wa Nane. Sipendi watu mnakaa hapa mnasema “Ndiyo” au “Siyo” kumbe hawasomi chochote. Mje navyo na vitabaki humu ndani kwa miezi yote tutakayokuwa hapa ndani.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, niwashukuru sana kwa kazi nzuri mliyofanya leo na mjiandae kwa ajili ya kesho kwani tutafanya kazi nzito zaidi ya kuingia kwenye vitabu. Kuna zile wanaita randama, zile ni *details* zaidi kuhusu vitabu hivyo. Ni vizuri mkazipitla hizo randama kwani zinajibu mambo yenu mengi sana.

Kwa hiyo, tunapowasilisha randama siku moja kabla ya Waziri kusoma lengo letu ni kwamba muweze kuzisoma na kuingia kwa undani zaidi. Hivi vitabu havisemi kwa undani zaidi, lakini randama zinakwenda *vote by vote*. Kwa hiyo, naamini hizo randama mnazo kwa sababu ziliwasilishwa hapa mezani na hivi vitabu

mnavyo kwa sababu mlipewa. Naomba vihamie humu ndani kwa sababu ya kazi tutakayokuwa tunaianza. Basi niwatakie jioni njema na hivyo naahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.42 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,  
Tarehe 29 Juni, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*